30 MEI, 2013

**BUNGE LA TANZANIA**

---

**MAJADILIANO YA BUNGE**

---

**MKUTANO WA KUMI NA MOJA**

**Kikao cha Thelathini na Nane - Tarehe 30 Mei, 2013**

*(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Naibu Spika (Mhe. Job Y. Ndugai) Alisoma Dua*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge leo ni Kikao cha Thelathini na Nane kinaendelea, Mkutano wa Kumi na Moja.

**HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI**

Hati Zifuatayo Ziliwasilishwa Mezani na:-

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI:**

Randama za Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi, kwa Mwaka wa Fedha 2013/2014.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA:**

Hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa kwa Mwaka wa Fedha 2013/2014; na

Taarifa ya Mwaka na Hesabu zilizokaguliwa za Kituo cha Kimataifa cha Mikutano cha Arusha kwa Mwaka 2012 *(The Annual Report and Audited Accounts of Arusha International Conference Centre (AICC) for the Year 2011/ 2012).*

**MHE. JUMA S. NKAMIA (K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA):**

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa Kuhusu Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa kwa Mwaka wa Fedha 2012/2013, Pamoja na Maoni ya Kamati Kuhusu Makadirio ya mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2013/2014.

**MHE. LETICIA M. NYERERE (K.n.y. MSEMAJI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI WA WIZARA YA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA):**

Taarifa ya Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani wa Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa Kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2013/2014.

## MASWALI KWA WAZIRI MKUU

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri Mkuu karibu sana.

**MHE. FREEMAN A. MBOWE-KIONGOZI WA KAMBI RASIMI YA UPINZANI BUNGENI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru sana kunipa nafasi ya kumuuliza Mheshimiwa Waziri Mkuu swali la kwanza.

Mheshimiwa Waziri Mkuu, ni dhahiri kwamba uwajibikaji wa Baraza la Mawaziri ni jambo la msingi sana katika kutekeleza majukumu ya Serikali na hivyo kuwezesha mazingira ya nchi katika masuala yote ya uchumi pamoja na utawala kuwa salama. Kwa kuwa hivi karibuni, Bunge lako lilipitisha mpango wa *Big Results Now* ambapo katika mpango huo unasemekana Mawaziri Sita wataweza kupewa mikataba maalum kupima uwajibikaji wao na kwa sababu uwajibikaji wa Mawaziri umekuwa ni kitu kigumu kufanyika katika nchi hii kwa muda mrefu hata pale makosa ya dhahiri yanapoonekana kutekelezwa.

Je, Mheshimiwa Waziri Mkuu, utakuwa tayari kuhakikisha Serikali ambayo wewe ndiyo kiongozi wake hapa Bungeni, inaweka wazi aina ya tathimini ambayo Mawaziri hao watafanyiwa na mikataba hiyo pengine iweze kuja hapa Bungeni ili Bunge litekeleze wajibu wake pale Mawaziri wanapokuwa kwamba hawataki kuwajibika, kwa sababu Serikali imeonekana haitaki kuwawajibisha Mawaziri? (*Makofi*)

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kumjibu Ndugu yangu Mheshimiwa Mbowe, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba Serikali imebuni utaratibu ambao tuna amini utasaidia sana katika kuhakikisha kwamba miradi ambayo ina buniwa inatekelezwa, lakini katika kutekelezwa huko, ufuatiliaji unakuwa ni jambo moja la msingi sana, kuanzia Waziri, Katibu Mkuu, pamoja na wasaidizi wao wote ndani ya Wizara inayohusika.

Kwa hiyo, kwa maana ya uwajibikaji, matarajio yetu ni kwamba kila Waziri atatimiza wajibu wake kulingana na maelekezo ambayo yatakuwa yametolewa na Rais ambaye ndiye atakuwa anasimamia hilo zoezi.

Sasa, mfumo ulivyo, ni kweli kabisa kwamba, unamtaka Waziri ambaye amepewa hilo jukumu atimizi jukumu hilo ipasavyo, Mwenye Mamlaka sasa ya kuamua kama ametimiza au hakutimiza, ni Rais wa Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania kwa mujibu wa utaratibu. (*Makofi*)

Kwa hiyo basi, kama Bunge linataka kumwajibisha huyo Waziri, kwa kufikiria hayo ambayo Mheshimiwa Mbowe anafikiria, ataweza kufanya hivyo kwa kupima sasa matokeo ya utekelezaji wa miradi inayohusika, kama kutakuwa na makosa, Bunge linaweza likatoa maelezo au fikira zake na pengine kumtaka Waziri husika awajibike, lakini kwa mfumo ulivyo, hatutakiwi kuleta ile tathimini ambayo Rais anaitumia kumpima Waziri wake mbele ya Bunge, kwa sababu ni kwa ajili ya kumsaidia yeye katika kuongoza taifa letu.

**MHE. FREEMAN A. MBOWE-KIONGOZI WA KAMBI RASIMI YA UPINZANI BUNGENI, WAZIRI MKUU NA TAMISEMI:** Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri Mkuu, ni kweli Rais ndiye mwenye Mamlaka juu ya Baraza lake la Mawaziri, lakini vilevile Katiba ya Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania imetoa Mamlaka kwa Bunge, kuisimamia Serikali, na wewe ni kiongozi wa Serikali Bungeni, wewe kama kiongozi wa Serikali Bungeni, unapokuwa huna mamlaka ya kuwasimamia na kuwaajibisha Mawaziri.

Je, huoni hili ni tatizo kubwa ambalo pengine ingesitahili ninyi kama Serikali ama wewe kama Mtendaji Mkuu wa Serikali, ushauri kupitia Tume ya Katiba, kuhakikisha kwamba Serikali sasa ina waajibisha kwa Wabunge na siyo kwa Rais peke yake?

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Mbowe mimi nafikiri si sahihi sana kusema kwamba Bunge hili halina namna yoyote ya kumwajibisha Waziri, Waziri Mkuu, hata Rais mwenyewe, bado Bunge hili mmepewa nafasi kubwa sana.

Kikubwa hapa ni amefanya jambo gani ambalo Bunge linaona sasa ni wanadhani ni muafaka kwao kuchukua hatua za kumwajibisha, kwa sababu kila jambo utataka liwe ni sehemu ya mjadala mkubwa hapa Bungeni, hata kidogo. Yako mambo mengine ya kiutekelezaji tu, mengi ni ya kiutendaji, kwa hiyo, mimi nadhani itategemea tu hali au hali ya tatizo hilo, ambalo pengine wewe na Wabunge wenzako mnaona ni sahihi.

Mimi sidhani kama kuna tatizo katika jambo hili hata kidogo, kwani ni mara ngapi mnatubana hapa, hata Waziri Mkuu mwenyewe mnafika mahali mnasema tutakupigia *vote of no confidence* kama *you are not performing well.*

Sasa kwa hiyo, fursa zipo tu, kwa hiyo, mimi sidhani kama ni sahihi sana kusema kwamba pengine Bunge halina, na kadhalika.

Lakini ametoa rai kwamba pengine tuiombe Tume, kwenye Katiba kule tuongeze kipengele hiki, mimi nafikiri ngoja, maama tulipofika hapa kura za maoni zote zimeshafanyika, wameshakusanya na rasimu imeandaliwa, pengine kwa maana ya mawazo, kama unaona hiyo, hata wewe unaweza ukashiriki katika mchakato unaobaki ukachomekea hayo mawazo kwa nia njema tu ya kutaka kuona kama litakubalika.

**MHE. JAMES F. MBATIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninashukuru, Mheshimiwa Waziri Mkuu, Taifa lolote lile haliwezi likapata maendeleo kama lina migogoro, na kwa kuwa Sayansi na Teknolojia ya dunia ya leo ni kwa ajili ya maendeleo endelevu.

Hapa kwetu Tanzania tumepokea Teknolojia hii na hasa ya kimitandao ya kijamii, zikiwemo simu ambazo kwa kiasi kikubwa zinachochea mifarakano katika jamii ya Tanzania na hususan masuala ya Kidini, ambapo milio kwenye simu inawekwa mambo ya dini ambayo ni mambo binafsi, mengine pande zote za dini zinashindana kwa kutumia milio ya simu, na nyingine zinakashifu dini nyingine.

Je, huoni ni busara kwenye maeneo ya simu hata kwenye mabasi na maeneo yote ya *public* ambayo inabidi watu kuvumiliana, tupige marufuku kutokutumia imani za dini ambao sio wahusika wa kusimamia dini hizi ili kuondoa *tension* iliyoko katika jamii sasa hivi, na simu hizi ndiyo zinaongeza mifarakano zaidi kwenye jamii?

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba tu nikubaliane na Mheshimiwa Mbatia kwa hili jambo alilolisema ambalo na mimi naliafiki kabisa ni kweli yako matumizi, mimi nayaita mabaya, ya mfumo huu wa mtandao kwa njia ya simu, na pengine si kwenye maeneo ya dini tu, mitandao hii inatumika hata kwenye mambo mengine tu ya kisiasa, ambayo *basically* ni ya kiuchochezi, mengine yanaashiria tu uvunjifu wa amani, mengine ni mgawanyiko. Kwa hiyo, kuna watu ambao kusema kweli wanatumia vibaya hii fursa ambayo imepatikana kutokana na TEKNOHAMA. Sasa, rai yangu kwa watanzania wote, nchi hii ni yetu sisi wote na suala la amani kwetu ni la msingi sana, TEKNOHAMA hii isiwe chanzo cha kusababisha mfarakano katika Taifa letu, hiyo ni kwa upande mmoja, lakini kwa upande wa pili, Serikali imeanza kuchukua hatua kuhusu eneo hili. Kwa hiyo, tumeshakaa, Rais amekaa na vyombo vinavyohusika.

Kwa hiyo, mimi naamini kwabisa baada ya muda si mrefu, hatua sitahiki zitachukuliwa kuhakikisha tu kwamba tunailinda nchi yetu, na mimi nitaomba sana watu wasije wakaanza kupiga kelele hapa, ooo! Mmetuingilia, mmetuingilia, hapana, ni kwa nia njema ya kuinusuru nchi yetu isiingie katika matatizo kwa sababu ya matumizi mabaya ya TEKNOHAMA.

**MHE. JAMES F. MBATIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninashukuru, kwa kuwa kufanya biashara tunakubali wafanyabiashara hawa ni kuongeza mapato ili waweze kupata faida, ndiyo maana ya biashara yenyewe, lakini biashara isitumike katika kulifarakanisha Taifa, kwa sababu amani na usalama wa taifa inabidi ulindwe kwa gharama yoyote ile. Kwa nini Serikali isitoe kauli nzito badala ya kuwabembeleza bembeleza wafanyabiashara, kupitia *TCRA*, waagizwe waondoe milio yote kwenye simu ambayo inafarakanisha Taifa la Tanzania na masuala ya imani yabaki kuwa ni mambo binafsi. (*Makofi*)

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba hii mitandao inatoka kwenye vyombo mahuhusi, ama itakuwa ni Kampuni ya *Tigo*, *Vodacom, Celtel*, itakuwa ni Kampuni nyingine yoyote. Kwa hiyo, kama anavyosema, vyombo hivi vinao wajibu wa kuhakikisha kwamba mitandao hiyo haitumiki vibaya, haitumiki kwa maslahi tu ya biashara, lakini katika kufanya hivyo tunaleta mfarakano ndani ya Taifa, lakini kama nilivyokuambia, hatua zimeanza kuchukuliwa tayari. Kwa hiyo, mimi nadhani wakati ukifika mzuri, basi Serikali itatoa kauli, lakini ikiendana sambamba na hatua ambazo zitakuwa zimechukuliwa.

**MHE. RASHID ALI ABDALAH:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana, tumeshuhudia matokeo mbalimbali ya hujuma na mauaji katika Taifa letu, mauaji yaliyosababishwa na imani za kidini, za kishirikina, kuna mauaji yaliyosababishwa kule Arusha, lakini pia kuna mauaji ya hivi karibuni kule Mtwara. Mheshimiwa Waziri Mkuu, waliouawa ni Watanzania, sasa Serikali ina mikakati gani ya kuzuia hujuma hizi za Watanzania?

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu swali la Mheshimiwa Rashid Abdallah ni pana, maana mauaji ameyachanganya mengii, ingekuwa ni aina fulani hivi ingekuwa rahisi sana kwangu kuweza ku - *focus* kwenye hilo eneo, lakini kwa maana ya mauaji, maana uliyoyataja wala si yote, yako mauaji vilevile mengine ya makusudi tu na yenyewe ni mauaji.

Yako mauaji mengine ambayo yanatokana na matatizo tu ya mapenzi, na yenyewe ni mauaji tu, kwa hiyo, kwa sababu umepanua eneo hili la mauaji limekuwa kubwa, ninachoweza kusema ni kimoja tu, kwamba, Serikali bado inania njema kabisa ya kuhakikisha inasimamia kwa mujibu wa sheria. Mauaji yoyote yale yatakayofanyika hapa nchini na mtu yeyote yule, sababu ndilo jukumu tulilokabidhiwa la kulinda usalama wa raia.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kwa upande mwingine, ni lazima vilivile watanzania nao tuwaase, mauaji mengine si ya lazima hata kidogo, lakini yanasababishwa tu na mitazamo tofauti ndani ya jamii, vitu ambavyo, watu wazima, watu wenye kujipenda, watu wanaoamini katika ubinadamu tulio nao wanapaswa kujua tu kwamba, unamwuaje binadamu mwenzako, kwa sababu ni Albino, kwa sababu ni mwanamke, kwa sababu ya hiki na kile, unaona havina sababu hata kidogo. Kwa hiyo, mimi nadhani kama Serikali tutaendelea, bahati nzuri sheria zipo, tutahakikisha kwamba wale wote wanaohusika na mauaji wanakamatwa wanafikishwa kwenye vyombo vya sheria.

**MHE. RASHID ALI ABDALAH:** Mheshimiwa Naibu Spika, nimshukuru Mheshimwa Waziri Mkuu kwa majibu yake, Mheshimiwa Waziri Mkuu, mauaji yaliyotokea kule Zanzibar, Serikali ilipeleka kikosi cha *FBI* wakishirikiana na Makachero wetu ili kufanya uchunguzi wa mauaji yale, lakini hadi sasa, hakuna taarifa yoyote iliyotolewa na Serikali. Je, Mheshimiwa Waziri Mkuu, sasa unaweza kutoa taarifa hizi kwa wananchi?

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nafikiri huko ndiko alitaka twende tangu mwanzo, ni kweli kwamba yalitokea yale mauaji, nadhani unazungumza ya Padri Mushi, katika mazingira ambayo yalihitaji kweli uchunguzi wa kina, uchunguzi wa uhakika. Sasa ninachoweza kusema tu kwa sasa ni kwamba, uchunguzi ule umechukua muda mrefu kwa sababu ya hali halisi ya tatizo lenyewe lilivyotokea, na maelezo yaliyopatikana ni maelezo ambayo bado yanahitaji kuthibitishwa vizuri zaidi kwa mujibu wa taratibu.

Kwa hiyo, hata pale ambapo mtu amekamatwa, amepelekwa mahakamani, bado uchunguzi lazima ukamilike kikamilifu ili tuwe na uhakika kwamba, mwisho wa yote ataweza kutiwa hatiani.

Kwa hiyo, kwa kweli mambo mengine yanakuwa na ugumu wenyewe tu kwa namna yanavyojitokeza, lakini imani yangu ni kwamba tutafika pazuri, *Inshallah* na mambo mengine tutayarikisha inapotakiwa.

**MHE. SUSAN A.J. LYIMO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru sana.

Mheshimiwa Waziri Mkuu, Waziri Mkuu wa Malaysia, alipoingia madakakani Mahathir Mohamad, mwaka 1981, alipoulizwa vipaumbele vyake vitatu. Alisema kipaumbele nambari moja ni elimu. Kipaumbele nambari mbili ni elimu na kipaumbele nambari tatu ni elimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Waziri Mkuu, ni ukweli ulio wazi kwamba elimu yetu hapa nchini inaendelea kuporomoka na kwa kasi sana. Sababu moja kubwa inayopelekea na viashiria tunavyoviona ni kwamba watoto wetu wanamaliza kidato cha nne, darasa la saba, hawajui kusoma wala kuandika. *(Makofi)*

Wataalam wamesema na hata tatifi zinaonyesha, na hata Tume uliyoiunda mwaka 2010. Ilisema moja ya sababu ni kwamba kitengo au Idara ya Ukaguzi, imetelekezwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni wazi kwamba katika Bajeti zote, kwa mfano ya mwaka 2012. Kanda ambayo ina zaidi ya Shule 430, imekuwa ikipewa Shilingi milioni 4 tu kwa ajili ya Ukaguzi.

Sasa Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwa kuwa Idara hii ya Ukaguzi, kazi yake kubwa ni kufuatilia ubora wa Elimu. Na kwa kuwa ilivyo sasa hivi ..

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mbunge, sasa uliza swali.

**MHE. SUSAN A.J. LYIMO:** Ndiyo. Kwa kuwa ilivyo sasa hivi Kitengo hiki hakifanyi kazi na Wakaguzi wako Maofisini kwa sababu ya changamoto kubwa zinazowakabili ikiwa ni pamoja na upungufu mkubwa sana wa Bajeti.

Je, Mheshimiwa Waziri, kuna mikakati gani Serikali imejiwekea ya kuhakikisha kwamba Kitengo hiki sasa kinafanya kazi yake vizuri ili ubora wa Elimu uweze kurejea? *(Makofi)*

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Naibu Spika, nadhani huo ni mtazamo wa Mheshimiwa Susan Lyimo. Kuhusu sababu za msingi, au chanzo cha msingi cha elimu Tanzania kuonekana inashuka. Lakini mimi nina hakika tungelikaa tukaanza kujadili sidhani kama wote tutakuwa tunao mtazamo huo. Kwa nini.

Kwa sababu hata kama leo ningeliongeze pesa Ukaguzi. Pale kwenye Idara ya Ukaguzi. Lakini kama Walimu huko hawako. Kama vitabu huko haviko. Kama shule zenyewe pengine hazina madawati. Kwa hiyo ni mambo mengi sana, ambayo unapaswa kuyatizama unapotazama tatizo la elimu hapa nchini.

Hicho ulichokisema ni sehemu tu, na ni lazima kije katika mazingira ambayo tayari yameboreka ili uweze kumuwezesha Mkaguzi kutimiza wajiibu wake inavyotakiwa. Lakini vinginevyo nina kubaliana na wewe kwamba hiyo ni moja ya maeneo ambayo yanapaswa kutazamwa kwa ujumla wake katika jitihada za kujaribu kuboresha elimu. *(Makofi)*

Sisi Serikalini, tunalitazama hilo. Tulikuwa tunafikiri hata uwezekano, pengine wa kuunda Wakala Maalum kwa ajili ya Ukaguzi wa Shule za Msingi na Sekondari. Ili kukiwezesha chombo hiki kuwa na upeo mpana zaidi wa ukaguzi na fursa kubwa za kuweza kusimamia eneo hili la ukaguzi kwa nguvu zaidi. *(Makofi)*

Kwa hiyo kwa maana hiyo ninachoweza kusema tu ni kwamba Serikali tunajitazama kwa upana zaidi kuliko Idara hiyo moja. Ndiyo maana kwenye *Big Result Now,* Sekta ya elimu ni moja wapo, na moja ya jambo ambalo litatazamwa ni pamoja na hilo. Lakini zaidi haya mengi ambayo nimeyataja. *(Makofi)*

**MHE. SUSAN A.J. LYIMO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Mheshimiwa Waziri Mkuu, nashukuru kwa majibu. Ni kweli kwamba katika Sekta ya Elimu kuna matatizo mengi sana. Lakini nili-*pin out* hilo moja la Ukaguzi.

Mheshimiwa Waziri Mkuu, niseme tu kwamba wakati Mheshimiwa Rais, akiongea na Wakuu wa Shule za Sekondari kule Mbeya mwezi Aprili, 2013. Alielezea suala zima la kuwa na Wakala wa Ukaguzi. Mheshimiwa Waziri wa Elimu kwa miaka miwili mfulululizo amesema kwamba kuna mpango wa kuanzisha Wakala wa Ukaguzi. Nilitaka kujua Wakala huyu anaanzishwa lini kwa sababu muda unakwenda na Mheshimiwa Rais naye ameliona hilo, na ametoa tamko kule Mbeya.

Je, sasa Serikali inajpanje ili kuwa na Wakala ambao sasa itaifanya Ukaguzi iwe chombo huru, ambacho kitaweza kufanya kazi zake vizuri? *(Makofi)*

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Naibu Spika, mchakato ule wa kuanzisha vyombo kama hivi Serikalini, kidogo ni mpana na mrefu. Lengo ni kujaribu kupata chombo ambacho kweli kitakidhi mahitaji yote. Yako mambo mengi sana ndani ya hilo wazo ambalo itabidi yaendane pamoja na maeneo mengine.

Kwa hiyo ninachoweza kukuambia Mheshimiwa Susan ni kwamba kauli hizo si kwamba ni kauli tu. Lakini hatua zimeishaanza kuchukuliwa na mimi imani yangu ni kwamba pengine katika muda ujao jambo hili litakuwa limekamika. Kwa hiyo tutabidi pengine kuja kuzungumza na Wabunge vile vile. Kupata *in puts* zaidi kidogo.

Ili tuone kwamba je, mfumo huo utasaidia katika kuboresha elimu au hapana? *(Makofi)*

**MHE. MURTAZA A. MANGUNGU:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninashukuru.

Mheshimiwa Waziri Mkuu, kumekuwa na hali ambayo inakinzana sana, kuhusu muda wa kazi na utoaji wa huduma, katika Taasisi na Idara za Serikali. Hasa ukizingatia, kila Idara na Taasisi inatoa muda wake wa kufanya kazi. Kama Ardhi ambao wanafanyakazi muda wa kuanzia saa 03.00 asubuhi hadi saa 6.00 mchana tu.

Je, nini muda wa kazi kwa huduma Serikalini?

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Naibu Spika, labda niombe arudie. Ametaja mfano kwamba kuna Idara au Wizara, sikumpata vizuri.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mangungu, fafanua vizuri.

**MHE. MURTAZA A. MANGUNGU:** Muda wa kazi, na utoaji huduma katika Tasisi, Idara na Ofisi za Serikali ni upi?

Kwa mfano, Idara ya Ardhi ambao wanafanya kazi kuanzia saa 3.00 asubuhi, hadi saa 6.30 mchana tu. Ambayo inasababisha usumbufu kwa wananchi, ambao wanatoka katika maeneeo mbali mbali nchini kwenda pale na wanasumbuka. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Una maana ya sehemu ya malipo ya Ardhi, au Idara ya Ardhi nzima?

**WAZIRI MKUU:** Amesema Idara, sasa sina hakika.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri Mkuu.

**WAZIRI MKUU:** Maana pale wana Kurugenzi nyingi kidogo. Lakini labda nimjibu tu swali la msingi.

Kwa utaratibu wetu hapa nchini. Mfanyakazi au mtumishi wa Serikali ndani ya Serikali na Taasisi zake, na Idara zake anafanyakazi kuanzia saa 1.30 asubuhi mpaka saa 9.00 alasiri. Huo ndiyo utaratibu.

Sasa kama Wizara ya Ardhi, kuptia kwa Profesa Anne Tibaijuka, wao wanafanya saa 3.00 asubuhi – mpaka saa 6.00 mchana, kwangu mimi hilo ni jambo jipya. Hilo ni jipya kabisa, maana haipo katika utaratibu wetu hata kidogo. Pengine nitamuomba Mheshimiwa Profesa Anne Tibaijuka pengine apate muda zaidi hata kutoa maelezo kinachotokea kwenye Wizara hiyo.

Sisi bado tunaheshya wao wanaanza saa 03.00 asubuhi, wakifika saa 6.00 mchana, baada ya masaa matatu waliyofanya kazi wao wanaondoka, itakuwa ni jambo la kuchekesha sana. Lakini Waziri mwenye dhamana yupo ninafikiri anaweza akalijibu vizuri zaidi kwa wakati utakuokuwa tumempangia. *(Makofi)*

**MHE. MURTAZA A. MANGUNGU:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kabsa Mheshimiwa Waziri Mkuu, hili unaweza usilifahamu. Lakini wanatumia nguvu kabisa, kuzuia watu kuingia katika ofisi yao.

Sasa ninaomba utoe tamko kwamba Idara, Taasisi na sehemu zote za Serikali, muda wake wa kazi kama ulivyotamka ni huo na hakuna mtu anayeweza kupinga. *(Makofi)*

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Naibu Spika, mimi ninafikiri, kubwa ni kumwambia Mheshimiwa Profesa Anne Tibaijuka. Waambie watumishi wako wafuate taratibu za Serikali. Maana yeye ndiye anayesimamia Sekta hiyo. *(Makofi)*

**MHE. MENDRAD L. KIGOLA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninashukuru sana kwa kunipa nafasi ili niweze kumwuliza swali Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Katika hotuba ya Bajeti ya jana ya Wizara ya Kazi na Ajira. Ilitagaza kima cha chini cha Mshahara, kwa Mashirika ya Watu Binafsi. Sasa imetokea mchanganyiko kwa wananchi bado hawajaelewa vizuri. Kwamba kima cha chini kilichotangazwa jana, kimewekwa katika *percentages.* Sasa wananchi wanauliza kwamba tunasema imepandishwa mishahara kwa kiasi gani.

Sasa walikuwa wanaomba baada ya kuweka *percentage.* Serikali itamke kwa kuweka tarakimu, ili iweze kueleweka. Kwa mfano tumesema kwamba Viwanda na Biashara, imepandishwa asilimia 43.8. Tukienda masuala ya Hoteli na wafanyakazi wa ndani ni asilimia 53, huo ni mfano tu. Sasa wananchi hawaelewi, inapanda kwa kiasi gani, kwa tarakimu.

Mheshimiwa Waziri Mkuu, unaweza ukawatangazia wananchi ili waweze kuelewa vizuri?

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba nijaribu kulieleza kidogo, sina hakika kama nitaliweza sana. Lakini uelewa wangu juu ya jambo hilo ni nini.

Upande wa Serikali na Taasisi zake. Tunapotangaza kima cha chini, kwa kawaida kinakuwa ni kima ambacho unakiona kwa maana ya kiwango cha fedha. Kwa sababu wote tunakuwa katika *level* moja. Kwa maana ya Kima cha chini kwa hiyo huwa hatuna tatizo.

Kwa upande wa Sekta binafsi. Hali haiko hivyo. Sekta binafsi imegawanywa katika makundi mbalimbali ya uzalishaji na uwezo wa kila sekta na wenyewe unatofautiana kati ya sekta moja na nyingine.

Kwa hiyo, kinachotokea pale wanakaa wadau wote wanaohusika na hiyo sekta. Wanatazama kima chini kilichotangazwa mara ya mwisho. Wanazungumza mpaka wanakubaliana. Mwajiri, Mwajiriwa pamoja na upande wa Serikali, wakishapata hicho ndicho kima cha chini kwa sekta hiyo.

Kwa hiyo unachokisema ni kweli. Kwamba, ni rahisi zaidi nikilieleza kiasilimia kwa kuwa yule mfanyakazi mwenyewe kwenye sekta hiyo anajua kima chake ilikuwa ni Sh.70,000/= ukisema ni asilimia 50 maana yake zimeongezeka kwa kiasi fulani. Lakini kwa kuwarahisisishia Watanzania hawa ambao wanashauku ya kujua ni kiasi gani.

Ninataka nikubaliane na wewe kwamba tutamshauri Waziri mwenye dhamana. Hii asilimia ambavyo inatajwa. Pengine inaweza isiwe na mvuto kwa mtu yeyote hata kutaka kuajiriwa huko. Kwa hiyo tumwombe tu aseme, hiyo asilimia 41.

Kwa maana ya fedha, kwa maana ya kima cha chini cha mara ya mwisho, zimeongezeka kwa kiasi gani. Hiyo ndiyo kidogo *message* inaweza ikafika kwa urahisi zaidi, na mimi naamini pengine ni jambo ambalo linawezekana tu. Kwa hiyo tutamshauri afanye hivyo. *(Makofi)*

**MHE. MENDRAD L. KIGOLA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninashukuru sana kwa majibu ya Waziri Mkuu, nadhani wananchi wataelewa. Lakini kufuatana na melezo mazuri Kwamba katika Sekta, kwamba wanakaa pamoja wanajadiliana halafu wanaweka kiweka kiwango cha chini cha mshahara. Lakini katika sekta unaweza ukaona kwamba imechanganyika. Kwa mfano, Mashirika haya, Mashirika ya Chai.

Katika Sekta ya Mashirika ya Chai, kuna Mashirika makubwa, kwa maana Viwanda Vikubwa, na Viwanda Vidogo Vidogo vya Wakulima wadogo, na hao wanakaa pamoja wakijadili mishahara ya kiwango cha chini.

Sasa utaona viwanda vikubwa vinapewa, vilipe mshahara kiasi kidogo sana. Kwa mfano Mashirika ya Chai wanalipa Sh.70,000/= sasa Viwanda vidogo vidogo na vyenyewe vimeweka mshahara Sh.70,000/= wakati viwanda vikubwa vile ..

**NAIBU SPIKA:** Tatizo Waheshimiwa, badala ya kuuliza Maswali, mnahutubia, na mko wengi hapa. Kwa hiyo, matokeo yake kwa vyovyote vile kuna Wabunge ambao hawatapata nafasi ya kuuliza Maswali.

Ni wakati wa Swali Jibu. Swali Jibu. Badala ya hotuba. Malizia Mheshimiwa.

**MHE. MENDRAD L. KIGOLA:** Swali langu ni kwamba. Je, Waziri Mkuu, unaweza ukawaambia kwamba, Viwanda Vikubwa vitofautiane na Viwanda Vidogo Vidgo, katika kupanga kima cha chini cha mshahara?

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba tu niseme kwamba hilo linawezekana kabisa. Kama utakuwa umesoma pengine maelezo ya Waziri, utaona yako maeneo ambayo imefanyika hivyo. Kwa mfano kwenye Sekta ya Ujenzi.

Sekta ya Ujenzi, Makampuni Makubwa, yako mengine ya kawaida na kadhalika. Kwa hiyo, ni kitu kinawezekana. Lakini nalo hili lazima litokane na mjadala wa wadau wenyewe kulingana na mazingira wanavyoyaona kwenye hiyo Sekta. Lakini ni ushauri mzuri, nadhani Waziri atakuwa amesikia tuone pengine katika kulitazama, baadaye weweze kuona kama inawezekana. *(Makofi)*

**MHE. VINCENT J. NYERERE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante.

Mheshimiwa Waziri Mkuu, Jeshi la Polisi limekuwa katika kashfa za kushiriki kwenye uuzaji wa Madawa ya Kulevya. Kubambika Kesi na Mauwaji wa Raia. Kambi Rasmi ya Upinzani, imekuwa ikiitaka Serikali, kulitengeneza upya au kuliunda upya Jeshi la Polisi, kunusuru hali hii.

Je, Serikali iko tayari kufanya hivyo katika kipindi kifupi?

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Naibu Spika, hawa Polisi, ni binadamu. Wanaweza vile vile wakafanya makosa, kama ambavyo sisi wengine kama binadamu tunafanya makosa. Utakachokikuta pale ndani ya Jeshi hili ni utaratibu waliojitengenezea wa kuchukua hatua kwa wale wote ambao wanakiuka taratibu zao za kazi. Kwa kupitia Mahakama Maalum ya Kijeshi.

Hizo hatua zinafanyika. Askari wengine wanafukuzwa kazi. Wengine wanateremshwa vyeo na kadhalika na kadhalika.

Kwa hiyo ni kitu ambacho kinao utaratibu tayari, wa namna ya kushughulikia mambo haya. Lakini rai unayoitoa si mbaya kwa Serikali. Mimi ninafikiri wacha Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, alitazame hilo aone kama taratibu zilizopo hazitoshelezi bado anaweza bado akatengeneza mfumo wa ziada kujaribu kuboresha zaidi jitihada za kudhibiti nidhamu ya Askari.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Waziri Mkuu. Tunashukuru, muda wa Maswali kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu, umeisha. Tunakushukuru sana kwa majibu ambayo tumeyapata asubuhi ya leo.

Kwenye orodha yangu amebakia mtu mmoja Mheshimiwa John John Mnyika na sababu yake ni ile ya kwamba, wale walnaouliza mara ya kwanza wanatumia muda mwingi sana katika kutoa hotuba badala ya kuuliza maswali ya moja kwa moja. Katibu tunaendelee.

## MASWALI NA MAJIBU

Na. 306

### Ujenzi wa Madaraja ya Kyoruba na Mori

**MHE. NYAMBARI C. M. NYANGWINE** aliuliza:-

Je, Serikali inatoa kauli gani kuhusu ujenzi wa madaraja ya Kyoruba (Kata ya Pemba) na Mori (Kata ya Nyandoto) Wilayani Tarime ambayo yamekuwa kero sehemu hizo kwa muda mrefu?

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge. Kabla Mheshimiwa Mwanri hajajibu. Ninaomba niwakumbushe Wenyeviti wa Kamati za Bunge. Hizi ni Kamati Mbali Mbali za Bunge. Kikao kile cha Kamati ya Uongozi kinakutana hivi sasa. Ninawaomba waelekee huko.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI)** alijibu:-

Mheshimwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Nyambari Chacha Mariba Nyangwine, Mbunge wa Tarime, kama hivi ifutavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na usumbufu na kero wanayopata wananchi wa maeneo wa Kata ya Pemba na Kata ya Nyandoto ambao unatokana na kutojengwa kwa madaraja ya Kyoruba na Mori, Halmashauri ya Wilaya ya Tarime kwa kushirikiana na *TANROADS* Mkoa wa Mara imefanya upembuzi yakinifu na kubaini kwamba zinahitaji shilingi milioni 610.2 ili kujenga daraja la Kyoruba na shilingi milioni 398.9 kwa ajili ya kujenga daraja la Mto Mori.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na ufinyu wa bajeti, Halmashauri inakusudia kuweka katika mpango wa Bajeti ya mwaka 2014/2015 miradi yote miwili ili kupata fedha zitakazowezesha kutekelezwa kwa miradi hiyo. Halmashauri ya Wilaya ya Tarime katika bajeti yake ya mwaka 2013/2014 imeidhinishiwa jumla ya shilingi milioni 560 kwa ajili ya matengenezo ya barabara za Halmashauri.

Aidha, Halmashauri inashauriwa kuangalia upya vipaumbele vyake. Hii ikiwa ni pamoja na kupata mapato ya ndani ya Halmashauri ili kupata fedha kwa ajili ya ujenzi wa madaraja hayo mawili na kuwaondolea usumbufu wananchi katika maeneo hayo.

**MHE. NYAMBARI C. M. NYANGWINE:** Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu ya Naibu Waziri, ambayo kwa kweli yanaweza kuwakatisha tamaa wananchi wa Tarime. Ninayo maswali mawili ya nyongeza.

Ni dhahiri kabisa kwamba Halmashauri ya Wilaya ya Tarime haiwezi kupata pesa, hata kutokana na mapato ya ndani hata kutoka nje, kujenga hayo madaraja mawili. Ninaomba kauli ya Serikali, inawashauri nini wananchi wa Tarime hasa wa Kata hizi mbili, kuhusiana na ujenzi wa Madaraja hayo?

Swali la pili, Halmashauri zetu nyingi, imeonekana dhahiri kwamba, zinashindwa kuendeleza sekta hii ya usafiri na usafirishaji, kutokana kutokuwa na hela za kutosha, za kujenga madaraja ambayo yamekuwa ni kero kwa wananchi wengi katika Halmashauri zetu. Kama kule Ngara na Tarime.

Je, Serikali inatoa kauli gani kuhusu madaraja ambayo ni kero kwa Halmashauri zetu?

**NAIBU SPIKA:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri wa TAMISEMI!

**NAIBU WAZIRI, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI):** Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nimekwenda Tarime na haya madaraja mawili anayoyazungumzia Mheshimiwa Chacha mimi nayafahamu, na anaposema kwamba haridhiki namwelewa pia kwa nini haridhiki.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini nataka niliambie Bunge lako hapa kwamba madaraja haya mawili anayoyazungumzia Mheshimiwa Chacha ni Shilingi bilioni moja na hii Halmashauri ya Tarime tunayoizungumzia hapa ambayo tumeipelekea, ukiangalia sasa hivi hapa fedha zilizotengwa kwa ajili yao ni Shilingi milioni 500 yote *overall.* Fedha tunayopeleka pale ya *Road Fund* ni kwa ajili *ya sport improvement* na *periodic maintenance.* Hawezi kuanzisha barabara mpya wala hawezi kuweka daraja pale.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimekwenda nikatafuta, nikaangalia katika maombi maalum kwamba wameomba nini. Hawakuomba barabara, waliomba hosteli na wakapata Shilingi milioni 500. Sasa mimi nataka niseme jambo moja hapa kwamba daraja linalozungumzwa moja katika haya madaraja yamejengwa wakati wa Mjerumani. Limetengenezwa *structure* pale*,* lakini anachozungumzia ni ile *run way,* na nimekwenda pale nimeiona ambayo inahitaji Shilingi milioni 610.

Hili lingine analolizungumza ni daraja ambalo lipo katika Halmashauri ya Mji kwa maana pale tumeshatenga sasa, kuna Halmashauri *DC* kwa maana ya *District Council* na kuna Halmashauri kwa maana ya Mamlaka ya Mji 310 ambayo tutaiingiza katika mpango wao. Sasa rafiki yangu Mheshimiwa Chacha, mimi naomba tusaidiane kitu kimoja, walete katika maombi maalum. Ukisema watatekeleza hapa kwa kutumia fedha za Halmashauri kwa mfumo huu wa kawaida, sahau! Haipo! Kama nilivyosema hapa, tumecheki kote huko anakosema, hakuna mahali popote!

Sasa mimi nikijibu hapa, nikasema hivi, 'bilioni moja itapatikana' Mheshimiwa Waziri Mkuu kakaa hapa nyuma yangu, ataniuliza, Bwana wewe umemwambia utampa Shilingi bilioni moja ziko wapi? Nasi hapa tumeshapitisha bajeti ya Mheshimiwa Waziri Mkuu. Naomba alete hili jambo na aje ofisini tukae wote kwa pamoja ili tuzungumze habari ya maombi maalum kuhusu haya madaraja mawili.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Kiongozi wa Upinzani Bungeni!

**NAIBU WAZIRI, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI):** Mheshimiwa Naibu Spika, samahani sikumalizia swali lake la pili.

Swali lake la pili amesema kwa Halmashauri zote, sasa hili najua Mheshimiwa Mbowe ananiangalia hapa, akipewa nafasi najua ataniulizia daraja lake la Hai. Wote hawa twende kwenye *special request* kwa maana madaraja, mwulizeni Mheshimiwa Magufuli atawaambieni, ni kwamba madaraja yanabeba fedha nyingi sana za Halmashauri na Halmashauri haziwezi kubeba habari hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nachukua nafasi hii kusema kwamba *TANROADS* wametusaidia sana katika hiki kitu tunachokizungumza hapa. Hii pia ni pamoja na kwenda kumwomba Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi kumwambia kwamba, Bwana tusaidie. Wametusaidia madaraja mengi sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, hilo ndiyo jibu! *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Kiongozi wa Upinzani Bungeni nilikuona. Swali la nyongeza!

**MHE. FREEMAN A. MBOWE – KIONGOZI WA KAMBI YA UPINZANI BUNGENI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kumwuliza Mheshimiwa Waziri swali la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli. Kitendo cha Mheshimiwa Waziri kutambua kwamba nitamwuliza swali hilo, ni kweli nitamwuliza maana yake, nina hakika analijua.

Je, Mheshimiwa Waziri, utakubali vilevile katika huo mpango maalum vilevile liweze kuingizwa daraja la Kikuletwa pamoja na daraja la Mnepo katika Halmashauri ya Wilaya ya Hai, Daraja la Mnepo katika Kijiji cha Mijongweni ambalo linaunganisha Hai na Moshi Vijijini na limekuwa kero kubwa sana kwa wananchi wa Kijiji cha Mijongweni pamoja na Kata nzima ya Machame Weruweru?

**NAIBU SPIKA:** Majibu Mheshimiwa Naibu Waziri (TAMISEMI)

**NAIBU WAZIRI, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI):** Mheshimiwa Naibu Spika, si nilikwambia? Si unaona sasa! *(Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kusema kwamba Mheshimiwa Mbowe alikuja tukazungumzia madaraja yote mawili, na Mheshimiwa Mbowe nilichomwambia ni kwamba, nimezungumza na Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Hai, anaitwa Bwana Humbee. Nikamwambia Humbee, madaraja haya yanataka kunivunja shingo. Mbona ninyi hamleti kwenye bajeti? Akasema tukiweka kwenye bajeti ina-*bust*! Tukajibu, nikamwambia na Mheshimiwa Mbowe, na ninataka aniangalie vizuri. mimi hapa *once upon a time* Halmashauri ya Wilaya ya Siha ilikuwa ni sehemu ya Hai.

Kwa hiyo, haya madaraja anayoyazungumza mimi nayafahamu. Acha mambo mengine yote, mimi ninachotaka kusema ni kwamba tunachoomba Halmashauri ya Wilaya ya Hai pamoja na zile nyingine zote ambazo mmesimama mnataka kuja hapa, hatuna namna nyingine ambayo tunaweza tukapitisha hizi bajeti hapa, kuacha kupitia kwenye kitu kinachoitwa maombi maalum. Hicho kitu nimemjibu Mheshimiwa Freeman Mbowe, nafikiri anataka iingie sasa katika *Hansard* ili akanikandamizie hapo.

Sasa nasema hivyo kwamba tulete maombi maalum ili kwa pamoja tushirikiane. Hii ni pamoja na kwenda kwenye Wizara ya Fedha, Wizara ya Ujenzi, pia kuzungumza naye kwa sababu *Road Fund* yote Mheshimiwa Magufuli ndio anayesimamia pale. Lakini tutashirikiana na Mheshimiwa Mbowe kuhakikisha kwamba kupitia maombi maalum tunaweza tukapata fedha kwa ajili ya haya madaraja mawili. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, swali la Mheshimiwa Aliko Kibona.

Na. 307

**Dhana ya Polisi Jamii**

**MHE. ALIKO N. KIBONA** aliuliza:-

(a) Je, dhana ya Polisi Jamii ilianzishwa au kuigwa kutoka nchi gani na kwa malengo au faida gani?

(b) Je, ni kwa nini watu wanazidi kuwa sugu katika suala zima la kutii sheria wakati huu wa Polisi Jamii?

(c) Je, Serikali haioni kuwa sasa ni wakati muafaka wa kufanya utafiti ili kubaini iwapo dhana ya Polisi Jamii imechangia watu kuwa wakaidi na wasiotii sheria?

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Majibu ya swali hilo, Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya nchi.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Aliko Nikusuma Kibona, Mbunge wa Ileje sehemu sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, dhana ya Polisi Jamii kwa mara ya kwanza ilianzishwa nchini Uingereza na Sir

Robert Peel mwaka 1829. Nia na madhumuni ilikuwa ni kupunguza wasiwasi wa jamii juu ya uhalifu na kujenga uhusiano mzuri baina ya Polisi na Jamii kwa ujumla ili kufikia malengo ya Jeshi la Polisi katika ulinzi na usalama wa raia na mali zao.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, suala la baadhi ya watu kuwa sugu katika uhalifu halina uhusiano na dhana ya Polisi Jamii, bali ni matokeo ya kutotaka kutii sheria kwa hiari kama ilivyofafanuliwa na Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ibara ya 26(i). Jukumu hili ni la wananchi wote na kuna haja ya kuunganisha nguvu ili kutokomeza vitendo viovu. Jeshi la Polisi litaendelea kutoa elimu juu ya umuhimu wa kutii sheria pasipo shuruti itakayoiwezesha jamii kubadilika.

(c) Mheshimiwa Naibu Spika, tafiti nyingi zilizofanywa ndani na nje ya nchi zimeonyesha kuwa matumizi ya dhana ya Polisi Jamii yanaleta faida nyingi kuliko hasara. Jamii imeanza kuelewa kuwa wao pia ni sehemu ya ulinzi wa maisha na mali zao kama ilivyoelezwa kwenye ibara ya 27 na 28 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania toleo la mwaka 1977. Aidha, kushiriki kwa jamii katika kutoa taarifa za uhalifu na wahalifu kwa njia mbalimbali kumechangia kudhibiti uhalifu kabla na baada ya kutendeka. Pia, uanzishwaji wa vikundi vya ulinzi shirikishi kwenye maeneo ya jamii ikiwemo Jimbo la Mheshimiwa Kibona kumechangia kwa kiasi kikubwa kupunguza matukio ya uhalifu.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Aliko Kibona, swali la nyongeza.

**MHE. ALIKO N. KIBONA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru. Naomba niulize maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, siku za karibuni tumeshuhudia vifo vingi vya raia wetu vikiripotiwa kusababishwa na Jeshi la Polisi. Tumeshuhudia pia vifo vingi vya Askari wetu vikisababishwa na raia. Lakini pia tumeshuhudia *Traffic* wetu barabarani wakipigwa makofi na raia. Vitu hivi hatukuvizoea katika Taifa letu. Je, siyo wakati

muafaka sasa wa kuangalia upya tumetoka wapi, tupo wapi, tunakwenda wapi na tufanye nini ili tufike salama tunakokwenda katika mustakabali mzima wa usalama wa Taifa letu?

Pili, utafiti aliosema Mheshimiwa Naibu Waziri anasema unaonyesha kwamba zipo faida nyingi za Polisi Jamii. Napenda kuuliza, Waingereza walitawala nchi yetu tangu mwaka 1918 – 1961 takriban miaka 43. Kipindi chote hicho hawakuthubutu ku-*introduce* au kuanzisha ulinzi shirikishi au Polisi Jamii. Je, hatuoni sasa kwamba siyo vizuri kuiga vitu vilivyofanyika Ulaya tukavi-*introduce* au tukaviingiza katika nchi yetu?

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante!

**NAIBU SPIKA:** Ajibu Naibu Waziri wa Nchi, Mheshimiwa Silima.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA:** Mheshimiwa Naibu Spika, vifo vingi ambavyo vinatolea vinasababishwa zaidi na mmomonyoko wa maadili yetu pamoja na baadhi ya Maaskari ambao tunao. Jitihada tuzifanye, tuhakikishe kwamba tunajua hili ni tatizo na tujirekebishe. Pamoja na hilo, Jeshi la Polisi linajipanga kufanya utafiti wa kutaka kujua kwa nini kunatokea haya yanayotokea. Tunawashukuru watu wa *COSTECH* wametupatia fedha kwa ajili ya utafiti huo na baada ya utafiti pengine tunaweza tukazaa mbinu nyingine ambayo itatusaidia zaidi.

Swali la pili kuhusu Waingereza kutoanzisha Polisi jamii; kwanza, niseme kwamba lengo la Waingereza lilikuwa siyo kupata uhusiano mzuri na jamii na ndiyo maana hawakuanzisha. Lengo la Polisi wakati ule ilikuwa ni kuhakikisha kwamba mtawala anatawala na anawatumia watawaliwa kama *subjects* kwa ajili ya malengo yake. Asingeweza hata siku moja kuwatumia wananchi ambao anawatoza kodi za vichwa na kadhalika kwa ajili ya kumpa taarifa za kiulinzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya uhuru Jeshi la Polisi ni la wananchi. Kwa hiyo, kuwasogeza na kuwatumia wananchi kusaidia ulinzi, ni wajibu kama ilivyosema kwenye Katiba yetu. Kwa hiyo, hiyo ni tofauti kubwa.

**NAIBU SPIKA:** Wizara ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia, Mheshimiwa Dkt. Mary Mwanjelwa.

Na. 308

**Mwingiliano wa Mawasiliano ya Simu**

**MHE. DKT. MARY M. MWANJELWA** aliuliza:-

Mawasiliano pekee yaliyopo Kata ya Katumba na Ngonga Wilayani Kyela Kata za Lubanda, Sanje, Ngukalembo, Bupigi na Malangali Wilayani Ileje yanasema: "*Welcome to Malawi*." Je, Serikali ina mkakati gani wa kuondoa mwingiliano huo wa simu ambao watu hawasikilizani?

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Mary Machuche Mwanjelwa, Mbunge wa Viti Maalum kutoka Mbeya kama ifuatavyo:-

Uingiliano wa mawasiliano kati ya nchi mbili au tatu yanaweza kutokea iwapo kuna makubaliano ya muungano wa mawasiliano, yaani *roaming agreement* baina ya nchi hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo linalotokea katika sehemu zilizotajwa na Mheshimiwa Dkt. Mary Mwanjelwa linatokana na makubaliano ya kampuni ya simu ya *Airtel* kati ya nchi hizi mbili ambapo wateja wa *Airtel Tanzania* wanaweza kutumia mtandao wa *Airtel Malawi* na pia wateja wa Malawi wanawezwa kutumia mtandao wa *Airtel Tanzania* kwa gharama za nchi zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na hivyo, Serikali kwa kutambua umuhimu wa kuwa na mawasiliano thabiti katika maeneo ya mipaka ya nchi yetu, imeagiza Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote yaani, *UCAF* kuweka kipaumbele na kupeleka mawasiliano katika maneo yote ya mipakani hata pale kusikokuwa na mvuto wa kibiashara, kwa lengo la kuboresha mawasiliano, hususan katika kuimarisha usalama wa nchi yetu.

Kwa mfano, maeneo ya mpaka kati ya Tanzania na Burundi na Rwanda kule Ngara kwa Mheshimiwa Ntukamazina, maeneo ya mpaka kati ya Tanzania na *Mozambique,* kule Peramiho kwa Mheshimiwa Mhagama; Maeneo ya Manyovu kwa kwenye mpaka wetu na Burundi kwa Mheshimiwa Obama, katika mwambao wa Ziwa Tanganyika, katika mwambao wa Ziwa Nyasa kwa Mheshimiwa Capt. Komba na Wilaya ya Kyela na Ngorongoro kwa Mheshimiwa Ole Telele ambapo wananchi wanapa *signal* za *Safari Com* na maeneo mengine ambayo sikuyataja.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Mary Mwanjelwa, maswali ya nyongeza.

**MHE. DKT. MARY M. MWANJELWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kwamba sijapata majibu kulingana na kanuni, lakini hata hivyo, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri na kwa kuwa tatizo hili lipo kwenye Wilaya za Kyela na Ileje ambapo ni mpakani na Malawi, lakini naomba niseme tu kwamba pia tatizo hili lipo katika Wilaya ya Mbozi, Momba, Chunya hasa sehemu zile za Msangano, Chitete, Mamba, Lwalaje, Ntanila, Matwiga, Mafyeko, Mafiga na hata Kambikatoto; na unakuta kwamba katika maeneo haya mikonga ipo lakini wananchi inabidi wapande kwenye miti, kwa sababu mawasiliano hakuna kabisa.

Kwa hiyo, namwomba Mheshimiwa Naibu Waziri atoe tamko hapa, ni lini mawasiliano ya uhakika yatafika katika maeneo husika?

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana! *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mawasiliano, Sayansi na teknolojia, majibu; ni lini?

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOKOJIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kama unavyofahamu, Serikali imekuwa na mpango na tumekuwa tunarudia hapa Bungeni mara nyingi na ninadhani mpaka Waheshimiwa Wabunge wametuchoka tunapotaja mfuko wa *UCAF*, lakini napenda kuwaalika Waheshimiwa Wabunge wote Jumamosi kwenye Semina ya Wizara pamoja na Mfuko, pamoja na Makampuni ya Simu ambapo tutatoa taarifa ya kina na orodha kwa kila Mbunge na eneo lake na lini mawasiliano yatafika kwenye eneo hilo kupitia Mfuko wa *UCAF,* lakini kupitia na makampuni ya simu.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge, tuendelee, kwa sababu ya muda, bado nina maswali matatu. Wizara ya Nishati na Madini, swali la Mheshimiwa Susan Kiwanga.

Na. 309

**Rasilimali ya Madini Nchini**

**MHE. SUSAN L. A. KIWANGA** aliuliza:-

Ni ukweli usiopingika kuwa nchi yetu ina rasilimali kubwa sana ya madini aina mbalimbali, lakini kama nchi, inaonekana haielewi hazina tuliyonayo, badala yake wageni toka nje ya nchi wanajua ni wapi kuna aina gani ya madiani na kwa kiasi gani. Je, kama Serikali ina takwimu za aina ya madini tuliyonayo katika nchi yetu, ni juhudi gani zimefanywa za kuwaelimisha Watanzania kuhusu utajiri huo ili wasiendelee kutapeliwa na watu wanaojiita wawekezaji?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Susan Limbweni Kiwanga kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kuwa nchi yetu ina utajiri wa madini ya aina mbalimbali yakiwemo madini aina ya Chuma ambayo yanakadiriwa kuwa tani milioni 103, Dhahabu tani milioni 2,222, Shaba tani milioni 13.65 na Nikel tani milioni 209. Madini ya vito kama Almasi, tani milioni 50.9 na Tanzanite tani milioni 12.6, makaa ya mawe tani milioni 911 na madini ya Viwandani kama chokaa tani milioni 313.0 kwa takwimu za mwaka 2011.

Utafiti kuhusu upatikanaji wa madini haya umekuwa ukiendeshwa na wataalamu wa Wakala wa Jiolojia Tanzania, yaani *Geological Survey of Tanzania – GST*, ambao ni Wakala wa Serikali. Tokea enzi hizo za Ukolini wataalamu hao wamefanya utafiti katika maeneo mbalimbali na taarifa zilizopatikana zimewekwa katika machapisho ya aina mbalimbali kama vile ramani, majarida na vitabu. Taarifa hizo zimekuwa zikitumiwa na wawekezaji wa ndani na nje ya nchi kuendeleza utafiti wa kina katika maeneo mbalimbali nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kwa kushirikiana na wadau mbalimbali imekuwa ikitoa elimu kwa umma kuhusu hazina ya madini nchini. Elimu hiyo hutolewa kupitia jarida la Wizara ya Nishati na Madini na machapisho mbalimbali, ambapo *GST* kwa kushirikana na kitengo cha Habari za Wizara wamekuwa wakitoa machapisho na taarifa kwenye vyombo vya habari. Aidha, mbali na machapisho, Wizara ina kitengo cha kusaidia wachimbaji wadogo kinachofanya kazi kwa kushirikiana na Shirika la Madini la Taifa, yaani *STAMICO* katika kutoa elimu na kusaidia wachimbaji wadogo kiufundi kadri inavyowezekana.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunatoa wito kwa wananchi wenye nia ya kupata taarifa kuhusu rasilimali za madini wasisite kuwasiliana nasi. Taarifa hizo zinapatikana pia

kwenye tovuti ya Wizara na *GST* na machapisho mbalimbali yanapatikana katika Ofisi za *GST* na Ofisi za Madini na Wizara.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Susan, swali la nyongeza.

**MHE. SUSAN L. A. KIWANGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Majibu ya Mheshimiwa Waziri nimeyapata, lakini hayajanitosheleza. Nilikuwa nategemea leo angetueleza madini yaliyopo nchini Tanzania ukichukulia Mkoa wa Morogoro tu kuna Green Tomarin, Rubi, Safaya lakini hapa katika maelezo yake hakuna.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pamoja na majibu haya, anasema wanatoa elimu kwa umma: Je, Serikali haioni sasa kuna haja ya kupeleka elimu hiyo ya madini katika Shule zetu za Msingi na Sekondari ambapo ndipo vijijini yalipo madini haya na Watanzania wajue kwamba hapa nilipo kuna gesi au kuna mafuta au madini ya aina fulani ili kuepuka kuuza ardhi anaona anauza ardhi tu ya juu lakini chini kuna utajiri mkubwa? Hilo ni swali la kwanza; hawaoni kwamba kuna umuhimu elimu itolewe?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, kwamba elimu inatolewa kwenye tovuti ili watu wawasiliane. Namwuliza Mheshimiwa Waziri, hivi ni wananchi wangapi wa Tanzania wanaoishi vijijini wanaoweza kuwasiliana na Wizara au kuingia kwenye *website* au mtandao? Je, hamwoni kwamba hiyo ni kuwanyima Watanzania haki yao kuelewa ni nini kilichopo ndani ya nchi yao ili wajipange katika kuingia ubia na wawezekazaji wanaokuja kuchukua maeneo yao? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Majibu Mheshimiwa Naibu Waziri wa Nishati na Madini, Mheshimiwa Simbachawene.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE):** Mheshimiwa Naibu Spika, katika jibu langu la msingi na hata swali lenyewe lilitaja tu kwamba ni madini mbalimbali. Kama Mheshimiwa Mbunge angetaka kujua ni madini gani; madini yamegawanyika katika sehemu kuu kama tano hivi. Kuna madini ya viwanda, *metallic*

*minerals, energy minerals, germ stones* ndiyo unakuta hapo kuna Tanzanite, rubi; hapo kuna elimu kubwa kweli kweli! Ili uweze kuipata hiyo inabidi uanze leo *degree* ya kwanza mpaka upate *Ph.D* ndiyo unaweza ukayamaliza, na kuna Maprofesa wa madini. Kwa hiyo, hapa kuna kazi kweli kweli!

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kwa faida ya swali hili, ni kweli kwamba yapo madini mengi na hadi sasa tumeweza kuchimba kiasi ambacho hata haifiki asilimia 10 ya madini yote yaliyopo nchini.

Kwa hiyo, utaona bado ni sehemu ambayo inahitaji kuendelezwa sana. Sasa kwanini tusitoe elimu kwa Shule za Msingi na Sekondari? Ni kweli kumekuwa na mjadala huo, nasi kama Serikali wazo hili tunalipokea, lakini mchakato huu upo na bahati nzuri nimewahi kupata mawazo ya wataalam, tunajaribu kuona ni namna gani tunaweza kulitekeleza, na kwa sababu shughuli hii inafanyika sana, basi tuone namna ya kuwafundisha vijana wa Shule za Msingi na Sekondari wanaoweza kujiajiri huko huko mapema, waweze kuelewa hii *industry* ikoje.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kuhusu machapisho, tovuti niliitaja tu kama sehemu mojawapo ya kisasa ya ku-*access* kwa haraka kuweza kupata ni madini gani yapo, kwa sababu pia kuna ramani mle na mambo kadhaa.

Pia nilizungumzia machapisho kwa maana ya vipeperushi, lakini pia zipo ramani. Wakala wa Jiolojia Tanzania *(GST)* wapo hapa Dodoma, wana mambo mengi. Karibuni sana Waheshimiwa Wabunge mfike mtembelee Wakala huu ndipo mtakapopata elimu na kujua kuna mambo gani katika nchi yetu mazuri na makubwa.

**NAIBU SPIKA:** Tuendelee na swali la jirani yake Mheshimiwa Susan Lyimo. Kutoka swali la Mheshimiwa Suzan Kiwanga sasa ni Mheshimiwa Susan Lyimo - Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika.

Na. 310

**Serikali kuagiza Mchele Nje ya Nchi**

**MHE. SUSAN A. J. LYIMO** aliuliza:-

Mchele wa Tanzania ni mzuri sana kwa ubora na utamu; na wakulima wa mpunga nchini wamevuna mchele wa kutosha kwa matumizi ya ndani.

Je, ni kwanini Serikali inataka kuingiza mchele kutoka nje kwa kisingizio cha soko huria huku kuna wakulima wakiwa na mchele wa kutosha?

**NAIBU SPIKA:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Susan Anselm Jerome Lyimo, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali haitafuti visingizio vya kupatia ufumbuzi matatizo ya msingi ya maisha ya wananchi wake. Aidha, vigezo vya kuagiza mchele, mahindi au bidhaa yoyote ile ni mapana zaidi yenye kuzingatia viashiria vya kiuchumi na kijamii na siyo suala linalofanyiwa maamuzi kwa wepesi bila kurejea masuala muhimu yakiwemo ya uzalishaji wa nafaka nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kuwa mchele wa Tanzania ni mzuri kwa ubora na utamu kwa walaji. Wakulima wa mpunga nchini wamekuwa wakivuna mpunga wa kutosheleza matumizi ya ndani kwa kipindi kirefu sasa. Tathmini iliyofanywa kwa mwaka 2012/2013 imeonesha kuwa uzalishaji wa mchele ulikuwa tani milioni moja na laki moja kama na thelathini hivi, wakati mahitaji yake yakiwa tani 816,000. Hivyo nchi kuwa na ziada ya tani kama 312,000.

Hata hivyo, kutokana na Serikali kuruhusu uuzwaji wa mazao ya nafaka nje ya nchi, akiba hii imekuwa ikiuzwa kiholela, na kwa sababu ya bei kubwa za masoko ya nje, wakulima wakauza hadi kile ambacho kingeelekezwa kwenye masoko ya ndani.

Aidha, baadhi ya wafanyabiashara wasio waaminifu walinunua mpunga kwa wakulima kwa bei ya kulalia na baadaye kuhodhi nafaka ya mchele katika maghala yao na kusababisha uhaba hewa kwa maana ya *artificial shortage,* hali iliyopelekea bei ya mchele kutoka wastani wa Sh. 1,800/= kwa kilo hadi kufikia Sh. 2,800/= kati ya Agosti, 2012 na Desemba, 2012.

Mheshimiwa Naibu Spika, dhamira ya Serikali ya kuagiza mchele kutoka nje ina lengo la kukidhi upungufu pale unapojitokeza na kudhibiti mfumuko wa bei ya bidhaa hii ambayo hupendwa na wananchi walio wengi. Utaratibu huu unalenga kumpunguzia mwananchi makali ya maisha pale ambapo bei zinaongezeka katika kiwango ambacho baadhi ya wananchi wanashindwa kumudu kwa ajili ya matumizi ya familia zao.

Aidha, mchakato wa kutathmini hali hii ya uhaba wa mchele umechukua muda na tathmini za kina na kufikia maamuzi Januari, 2013. Hivyo basi, mwezi Januari, 2013 hakuna mchele unaovunwa Tanzania na hivyo suala la wakulima kuwa na mchele mwezi Januari halina ukweli kwa kuwa halina nafasi.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Suzan, swali la nyongeza.

**MHE. SUSAN A. J. LYIMO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana na niseme kwamba sikuridhishwa na majibu ya Waziri kwa sababu bado wakulima wengi wana mazao mengi ndani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nina maswali mawili. Kwa kuwa Serikali imekiri kwamba nafaka zimekuwa zikiuzwa kiholela nje na kuna wafanyabiashara wakubwa ambao

wamekuwa wakihodhi nafaka hizo, nilitaka kauli ya Serikali: Je, wafanyabiashara hao ambao ndio wamesababisha adha hiyo, wamechukuliwa hatua gani? *(Makofi)*

Swali la pili. Kwa kuwa, panapokuwa na uhaba wa chakula wananchi hukataliwa na Serikali wasiuze mazao yao nje ya nchi, lakini vilevile ni ukweli kwamba Serikali hii haijawasaidia wakulima kwa kuwaboreshea miundombinu yao ya barabara na reli na hivyo kusababisha mazao yao kuwepo ndani ya nyumba au maghala yao: Je, sasa Serikali iko tayari kuwatafutia wakulima wake masoko mazuri ili waweze kuuza mazao yao nje na ndani ya nchi? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Majibu, Naibu Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika, Mheshimiwa Malima.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza mimi sikusema wafanyabiashara wakubwa, nimesema wafanyabiashara walanguzi. Hivi ninavyozungumza, Sumbawanga wameanza kuvuna mpunga na jana tulipata taarifa na tumefuatilia na Mheshimiwa Mbunge, namshukuru sana, walikuja na Mheshimiwa Malocha wakaniambia hivi sasa kuna watu wanakwenda kwa wakulima na wananunua mpunga gunia la kilo 100 kwa Sh. 24,000/=. Ukikoboa kwa Sh. 6000/= unapata kilo 60 za mchele kwa Sh. 30,000/=. Sasa hawa sio wafanyabiashara wakubwa! Huu ni utaratibu wa ulanguzi ambao umo katika mfumo wa soko ambao sisi tunapambana nao kuudhibiti. Lakini hapa wanapokwenda kwa wakulima wanakwenda waki-*abuse* ile hali ya ugumu wa uchumi uliopo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, tulichojipanga kufanya ni kwamba tunataka tuwaombe Wakuu wa zile Wilaya husika, pamoja na Bahi juzi tulikwenda, tumekuta wameanza kuvuna mpunga, wananunua kwa Badwell, gunia Sh. 30,000/=.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, Wizara ya Kilimo na Tawala za Mikoa tunataka kujipanga ili wanunuzi

watakapoingia kununua mpunga pale, wanunue kwa utaratibu unaoleweka. Tatizo ni kwamba, watakapoingia, baadhi yetu sisi wenyewe hapa tunahusika katika mambo hayo. Utaanza kusikia ooh, sasa unajua vibali vimekuwa vigumu, biashara imekuwa ngumu, soko huria.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, bei ya wastani ambayo mkulima akipata inakuwa kidogo ni afadhali, kusema ukweli ni Sh. 50,000/=. Kwa hiyo, katika hali hiyo tunataka tutoe mwongozo ili wakulima wafahamu.

Mheshimiwa Naibu Spika, hili la pili la kusema Serikali haijawasaidia wakulima, haijajenga miundombinu; napata taabu kidogo kwa Mheshimiwa Susan kwa sababu sielewi kama anaona ninachoona mimi. Kwa mfano, kwa hawa wakulima wa Sumbawanga barabara zinajengwa, zinakwenda kule mpaka Mpanda na kadhalika. Usafirishaji wa kuondoa mazao, hata kwake Ifakara barabara inajengwa. Kwa hiyo, kweli tunaweza tukawa tunafanya mapenzi ya siasa, lakini kazi ya Serikali ya Chama cha Mapinduzi iko pale pale.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Swali la mwisho la nyongeza, Mheshimiwa Sanya nilikuona.

**MHE. IBRAHIM MOHAMED SANYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Nataka niulize swali moja dogo la nyongeza kwa Mheshimiwa Waziri.

Kwa kuwa, nchi ya Kenya huagiza mchele mwingi kutoka Pakistan; na kwa kuwa Jumuiya ya Afrika Mashariki, Tanzania na Kenya walikubaliana kwamba Kenya isiagize tena mchele kutoka Pakistan na badala yake wanunue kutoka Tanzania; na kwa vile ongezeko la ziada la tani 312,000 kwa kila mwaka na ukulima wa mpunga ni dogo ukilinganisha na soko la Kenya peke yake ambao tumewazuia wasinunue kutoka Pakistan: Je, Serikali imefikia wapi na italitatuaje tatizo hili la kuiuzia Kenya mchele badala ya Kenya kuagiza kutoka Pakistani? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Sijui kama Mheshimiwa Waziri wa Ushirikiano wa Afrika Mashariki amelifikia hili swali. Mheshimiwa Naibu Waziri, Kilimo, Chakula na Ushirika, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, Tanzania uzalishaji wetu wa mchele *geographically*, tuna uzalishaji mwingi maeneo ya Kyela, Idodi, Bahi na kadhalika. Masoko yale pia pamoja na kwamba tuna tani laki tatu, hatuna tatizo la masoko ya kuuza nje. Ndiyo maana unakuta hata ile akiba yetu inachukuliwa nje kwa sababu ya ubora wa mchele wetu.

Sasa hii *facility* iliyokuwepo Kenya na kwa maana hiyo ya makubaliano yaliyopo kwenye *East African Community,* ni kweli kwamba kuna hayo makubaliano. Lakini hata hizo tani laki tatu siyo kwamba tumekosa soko la kupeleka, bado kwa mfano kwa mchele wa Shinyanga kule kwa akina Azza mchele wao mwingi unakwenda Rwanda na Burundi, wala hawana sababu ya kuupeleka Kenya.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, tunachosema ni kwamba pamoja na makubaliano yetu, sisi mkakati wetu ni kwamba, uzalishaji wetu ni tani 1,200,000, lakini kama Taifa tunaweza kufikisha hata uzalishaji wa tani milioni tatu. Kwa hiyo, tunatengeneza mikakati ili wakulima wetu wakubwa na wadogo wafikie hizo tani milioni tatu za uzalishaji ili tuwe na soko la kuuza kwanza ndani na pia *excess* ya kufika mpaka *South Sudan,* Kenya, Somalia na popote tukitaka waje kuchukua huu mchele ambao unakolea nazi vizuri zaidi kuliko ule wa Pakistan.

**NAIBU SPIKA:** Swali la mwisho kwa siku ya leo, Mheshimiwa Badwel.

Na. 311

**Kusaidia Kiwanda cha Kusindika Alizeti – Bahi**

**MHE. OMARY A. BADWEL** aliuliza:-

Wananchi wa Kijiji cha Chibelala Wilayani Bahi kupitia kikundi cha CHIWONA wamejenga kiwanda cha kusindika alizeti kwa msaada wa *UNIDO*, lakini mpaka sasa yapata miaka minne imepita kiwanda hicho hakifanyi kazi licha ya kukamilika:-

(a) Je, Serikali itatembelea lini kiwanda hicho ili kujua matatizo yaliyopo?

(b) Je, Serikali ipo tayari kusaidia wajasiriamali hao wa CHIWONA kutatua matatizo yanayokabili kiwanda hicho?

**NAIBU SPIKA:** Majibu ya swali hilo, Naibu Waziri wa Viwanda na Biashara, Mheshimiwa Gregory Teu.

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Omary Ahmed Badwel, Mbunge wa Bahi lenye (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kwamba wanakikundi cha CHIWONA wa Kijiji cha Chibelala Wilaya ya Bahi Mkoani Dodoma walipata msaada wa mashine ya kusindika mafuta ya alizeti kutoka *UNIDO* mwaka 2009. Lakini miaka zaidi ya minne imepita kiwanda hiki kidogo hakifanyi kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kusaidia na kujiridhisha mwenyewe, mimi binafsi pamoja na *SIDO* Mkoa tumetembelea kiwanda hiki kidogo tarehe 27 Mei, 2013 kwa lengo la kujua matatizo yaliyopo. Hata hivyo, *SIDO* Mkoa wa Dodoma walishatembelea kiwanda hiki tarehe 13 Oktoba, 2012 ili kubaini matatizo yaliyopo.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kutembelea na kuongea na kushauriana kwa pamoja na uongozi wa kiwanda na kupata taarifa ya sababu zilizopelekea kiwanda hicho kutofanya kazi kwa muda mrefu, Wizara yangu imechukua hatua zifuatazo:-

(i) Wizara yangu imeandika barua kwenda Halmashauri ya Bahi Mkoani Dodoma na kuwataka watoe ushirikiano wa kutosha wa kumaliza ujenzi wa madirisha ya jengo la mradi hadi yakamilike ipasavyo kulingana na mkataba wa jengo ulivyokuwa.

(ii) Ni wajibu wa *SIDO* Mkoa wa Dodoma kubuni teknolojia, kutengeneza na kutoa mafunzo na ushauri. Hivyo mafundi wa *SIDO* Mkoa wa Dodoma niliokwendanao katika kiwanda hiki kidogo tarehe 27 Mei, 2013 kwa kushirikiana na wanakikundi wa CHIWONA, niliwagiza washirikiane kukamilisha kazi ya ukarabati na kufufua jenereta ya zamani iliyoharibika kwa kutimia vifaa au vipuli vilivyokwishanunuliwa na *SIDO* Mkoa wa Dodoma kwa fedha ambazo zilitolewa na *SIDO* Mkoa kama mkopo kwa kikundi cha CHIWONA na kuiwasha jenereta hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa ya mafundi wa *SIDO* kupitia Meneja wa *SIDO* Mkoa wa Dodoma niliyoipokea jana tarehe 29 Mei, 2013, inasema kuwa jenereta hiyo imeishawaka na mashine hiyo inafanya kazi. Hivi sasa kikundi cha CHIWONA kinawaandaa vijana wawili wa kuendesha mashine hiyo ili wakapate mafunzo na ushauri kutoka *SIDO* kabla ya kuanza uzalishaji.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Badwel, swali la mwisho kabisa siku ya leo.

**MHE. OMARY A. BADWEL:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili madogo ya nyongeza.

Pamoja na majibu mazuri na kwa kweli kwa kazi nzuri iliyofanywa na Mheshimiwa Naibu Waziri na hatimaye kiwanda kilichokuwa kimekwama kwa miaka zaidi ya minne, jana kimewashwa, nampongeza sana. Lakini pamoja na hayo, nina maswali madogo mawili ya nyongeza. *(Makofi)*

Swali la kwanza, kwa kuwa Mheshimiwa Naibu Waziri ametembelea yeye mwenyewe kiwanda kile na ameona

tatizo kubwa lililokwamisha kiwanda hicho ni ukosefu wa nishati ya uhakika hasa umeme, lakini tayari Serikali imepeleka umeme mpaka kijiji cha jirani kama kilomita tatu kutoka pale ambapo kiwanda hiki kipo.

Je, Serikali iko tayari kuchukua juhudi za kupeleka umeme pia kwenye kijiji hicho pamoja na huduma nyingine, lakini kiwanda hicho pia kipate umeme? Hilo ni swali la kwanza. *(Makofi)*

Swali la pili, kwa kuwa Naibu Waziri ametembelea mwenyewe na ameona tatizo kubwa pia ni ukosefu wa mtaji wa kutosha kwa kikundi kile: Je, Wizara yake ina mpango gani wa kuviwezesha vikundi kama hivi kupata mikopo au ruzuku ili viweze kukuza mitaji yao?

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Madwel, Mbunge wa Bahi. Majibu, Naibu Waziri wa Viwanda na Biashara, Mheshimiwa Gregory Teu.

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa, ni tatizo la umeme kama alivyosema Mheshimiwa Mbunge kwamba, umeme ni tatizo. Lakini baada ya kufika pale nimeona kwamba kweli kabisa Kijiji hiki cha Chibelala pamoja na kikundi kile cha CHIWONA kilichopo pale, Kijiji kile kimekuwa kikubwa sana, kina Shule ya Sekondari, Zahanati na kikundi kikubwa hiki.

Sasa hivi imefikia wakati mwafaka wa kijiji hiki kupata umeme. Ni bora nimshauri Mheshimiwa Mbunge kwamba, kwa kusaidiana na Halmashauri ya Wilaya ya Bahi na yeye mwenyewe pamoja na kikundi kile, wamwone Meneja wa *TANESCO* Dodoma ili aweze kufunga umeme pale. Kwa sababu inawezekana kabisa, umbali wa kijiji chenyewe ni kutoka barabara kuu ya Dodoma – Iringa, pale Mpunguzi na kwenda kule ni mwendo mfupi sana. Kwa hiyo, inawezekana kabisa kwa kumtumia Meneja wa *TANESCO* Dodoma umeme ukaweza kufungwa hapo. Kwa hiyo, Halmashauri, Mbunge mwenyewe na wanakikundi wakimwona Meneja, hilo litafanikiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili ni kuweza kupata mtaji ili kikundi hiki cha CHIWONA kiweze kuendelea. Niseme tu kwamba mtaji kwa sasa hivi unawezekana kwa njia ya mkopo. Uko Mfuko wa Taifa wa Maendeleo ya Wajasiriamali ambao ni *NEDF,* unaweza kutoa mkopo kwa Kijiji hiki. Mikopo inayotolewa pale ni kwa aina mbili; ya biashara na uzalishaji ambapo inawezekana kabisa umoja au ubia huu wa CHIWONA kupata mkopo huu.

Masharti ya mkopo ni madogo; mkopo wenyewe unaweza kutoka kwa masharti ya uwezo wenyewe wa kikundi kutoa au kuendesha miradi, kuwepo mahali pa kufanya kazi ya mradi wenyewe, vilevile na leseni ya biashara ambapo ninaamini kwamba kikundi hiki cha CHIWONA wanatimiza masharti haya. Kwa hiyo, njia ya mkopo wa *NEDF* inawezekana.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri. Maswali yamekwisha. Kama mtakavyoona, tumechota kidogo muda ambao hatukupaswa kuugusa kabisa kwa sababu leo ni Wizara ya siku moja.

Wageni waliopo Bungeni leo ni pamoja na Wajumbe wa Kamati ya Ushirikiano wa Kimaendeleo ya Bunge la Ujerumani, ambao unaongozwa na Mheshimiwa Balozi wa Ujerumani, Clauds Peter Blandes - *The Germany Ambassador in Tanzania,* na wenzake ambao nadhani siwaoni pale, ambao ni Wabunge kutoka Ujerumani. Tunawakaribisha sana, Helga Daub, Johannes Selle, Thilo Hope, Claudia, Verheneyen, Kate Adams, Felister Rugambwa ambaye ni Afisa wa Dawati la Ulaya, Mambo ya Nje.

Tuna Mheshimiwa Balozi Juma Halfan Mpango - Balozi wa *DRC* na Kiongozi wa Mabalozi wanaoziwakilisha nchi zao hapa nchini. Ahsante sana, na karibu sana kaka yangu. *(Makofi)*

Balozi Ambrosio Lukoki, Balozi wa Angola hapa nchini. Ahsante sana.

Ahsante sana Balozi Vicente Veloso Balozi wa Msumbiji hapa nchini. Karibu sana Mheshimiwa Balozi wa Msumbiji unakaribishwa Kongwa. Ukombozi wao ulianzia huko msishangae. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Filbeto Ceriani Sebregondi - Balozi wa Jumuiya ya Nchi za Ulaya hapa nchini, karibu sana; na Bibi Dorcas Membe, mke wa Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Nje ya Nchi na Ushirikiano wa Kimataifa. Ahsante sana.

Kuna Wageni waliofika Bungeni kwa ajili ya mafunzo, Wajumbe 37 kutoka Jimbo la Mtama na Mchinga. Wale wageni wetu wa Mtama na Mchinga waliokuja kujifunza masuala ya Bunge wako wapi? Oh, mko huko pembeni, karibu sana. Madiwani 19 kutoka Jimbo la Muyuni Zanzibar. Waheshimiwa Wabunge Madiwani kutoka Zanzibar, karibuni sana. Wanafunzi mbalimbali kutoka Vyuo Vikuu vya hapa Dodoma, *UDOM*, *Saint John* na *CBE*. Wanafunzi wote *UDOM*, *Saint John* na *CBE* simameni. Ahsanteni sana. Karibu sana wanafunzi wote, karibuni sana mjifunze masuala ya Bunge, mnakaribishwa wakati wowote mwingine tena kufika. Katibu tuendelee.

## MWONGOZO WA SPIKA

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mkosamali na Mheshimiwa Mbatia. Kuna mwingine? Ni wawili hao, Mheshimiwa Mkosamali.

**MHE. FELIX F. MKOSAMALI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba mwongozo kwa mujibu ya kanuni 68(7), kwa ajili ya muda, naomba nisinukuu kuhusu majibu aliyoyatoa Mheshimiwa Waziri Mkuu wakati wa maswali kuhusu swali la Mheshimiwa Mbatia.

Mheshimiwa Mbatia aliuliza kuhusu hatua zinazochukuliwa na Serikali kudhibiti kauli Serikali ikataze milio ya simu. Sasa Serikali imejibu kwamba suala hilo imeliona inaendelea kulichunguza. Sasa tunataka tujue: Kwa sababu haya ni majibu mepesi, Wabunge wanauliza maswali kwa Waziri Mkuu, anajibu majibu ambayo ni kama vile tu ya

kuridhisha, kupoozapooza, siyo ya kuagiza watu, siyo ya kuchukua hatua kwa mambo ambayo yanakuwa *serious* na yanazidi kuleta machafuko kwenye nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa naomba mwongozo wako, nimesoma nyongeza ya sita na kanuni ya 38, ni hatua gani zinaweza kuchukuliwa na Mbunge endapo haridhiki na majibu yanayotolewa na Mheshimiwa Waziri Mkuu?

**NAIBU SPIKA:** Mwongozo wangu ninaokupa ni kwamba, shirikiana na Ofisi ya Katibu wa Bunge, kuna wataalamu pale watakushauri namna ya kwenda kwenye mazingira kama hayo. Mheshimiwa Mbatia.

**MHE. JAMES F. MBATIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutumia kanuni ya 67(8) ya mwongozo, lakini kwa kuokoa muda nisiisome. Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ibara ya 63(2) inasema: "sehemu ya pili ya Bunge itakuwa ndicho chombo kikuu cha Jamhuri ya Muungano ambacho kitakuwa na madaraka kwa niaba ya wananchi kusimamia na kuishauri Serikali ya Jamhuri ya Muungano na vyombo vyake vyote katika kutekeleza majukumu yake kwa mujibu wa Katiba hii."

Mheshimiwa Naibu Spika, ibara ya 19(2) inasema: "Kazi za kutangaza dini, kufanya ibada, kueneza dini itakuwa ni uhuru na hiari kwa mtu binafsi na shughuli za uendeshaji wa Jumuiya za Kidini itakuwa nje ya shughuli za mamlaka ya nchi." Ya tatu inasema: "Hifadhi ya haki zilizotajwa katika ibara hii itakuwa chini na taratibu zilizowekwa na sheria ambazo ni muhimu katika jamii ya kidemokrasia kwa ajili ya usalama wa jamii, amani katika jamii, maadili ya jamii na Umoja wa Kitaifa." Ibara ya tatu inasema: "Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni nchi ya Kidemokrasia na Kijamaa isiyokuwa na dini yenye kufuata Mfumo wa Vyama Vingi vya Siasa."

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa ombi langu na heshima kubwa niliyonayo kwa Waziri Mkuu, wawekezaji wote, biashara zote zinazowekwa, mikataba tunayosaini,

hawatakiwi kuvunja Sheria za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na utaratibu wa kueneza dini uko ndani ya Katiba. Wafanyabiashara hawajapewa ruhusa ya kutangaza dini na wanatumia mitandao hii kulifarakanisha Taifa la Tanzania na hii ni kinyume na Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba mwongozo wako au tuitake Serikali kabla Bunge hili waje na kauli ya kuondoa fujo hizi kwenye jamii. Tusipoziba ufa sasa, tutakuja kujenga ukuta kwa gharama kubwa ya kulisambaratisha Taifa lote la Tanzania.

**NAIBU SPIKA**: Mheshimiwa Mbatia umeuliza swali kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu, naona ndiyo hili hili la Mheshimiwa Mkosamali. Sasa tunafika mahali ambapo tunataka sisi Wabunge kila tunachokisema, lazima kifanyiwe kazi saa hiyo hiyo, wakati huo huo. Jibu limetolewa kwamba Serikali imelisikia jambo hilo na inalifanyia kazi. Nafikiri tungewapa nafasi na muda, kama baada ya muda fulani jambo hilo linaonekana kama bado halikufanyiwa kazi, tukisimama tena kweli itakuwa na hoja. Lakini tukifanya hivyo, itakuwa siyo sawasaswa.

Kwa hiyo, mwongozo wangu ni kwamba tuvute subira. Kama hatuvuti subira, basi tutumie taratibu nyingine za kikanuni zipo za kuendeleza jambo hilo kuliko utaratibu ambao tunautumia sasa.

## HOJA ZA SERIKALI

### Makadirio ya Matumizi ya Serikali Kwa Mwaka 2013/2014 – Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa

**NAIBU SPIKA:** Sasa naomba nimwite Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa, Mheshimiwa Bernard Membe kusoma hotuba yake. Karibu sana Mheshimiwa.

**WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kufuatia taarifa iliyowasilishwa leo Bungeni na Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Kudumu ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa, naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu likubali kujadili na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa kwa mwaka wa fedha 2013/2014.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa ridhaa yako naomba nitangulize kusema kwamba kinachosomwa hapa ni ufupisho wa hotuba yangu katika vitabu ambavyo vimesambazwa. Hivyo yote ninayoyasoma hapa yapo kwenye kitabu hicho.

Mheshimiwa Spika, napenda kutumia fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa uongozi wake mahiri wa Serikali ya Awamu ya Nne. Chini ya uongozi wake Taifa letu limeendeleza utamaduni wetu wa kudumisha amani, usalama na mshikamano wa kitaifa pamoja na kuimarisha ushawishi wa Tanzania katika nyanja za kikanda na kimataifa kupitia diplomasia thabiti na imara.

Hii inatukumbusha kuwa ni wajibu wa kila Mtanzania kutumia kila uwezo alio nao kuendeleza urithi waliotuachia waasisi wa taifa hili wa kudumisha amani, usalama, umoja na mshikamano wa Kitaifa bila kujali rangi, kabila, dini au itikadi zetu za kisiasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda pia kuwashukuru Mheshimiwa Mizengo Peter Pinda - Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania pamoja na Mheshimiwa Stephen Masatu Wasira, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Mahusiano na Uratibu kwa hotuba zao nzuri. Hotuba zao sio tu zimechambua kwa kina masuala ya kiuchumi, kijamii, kiusalama na kisiasa na hivyo kutoa dira ya Taifa letu katika mwaka ujao wa fedha bali pia zimegusia mambo kadhaa ya msingi yanayohusu Wizara yangu na hivyo kufanya kazi yangu leo kuwa nyepesi zaidi. Pia, niwashukuru Mawaziri wenzangu ambao wameshawasilisha hotuba zao, ambazo

kwa njia moja au nyingine pia zimegusa maeneo yanayohusu Wizara yangu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nitumie fursa hii kutoa shukurani zangu za dhati kwa Waheshimiwa Wabunge wote ambao ni wajumbe wa Kamati ya Bunge ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa, chini ya uongozi wa Mheshimiwa Edward Ngoyai Lowassa, Mwenyekiti wa Kamati, kwa kazi nzuri waliyoifanya ya kuchambua na kushauri kuhusu bajeti ya Wizara yangu wakati wa vikao vya Kamati. Uchambuzi na ushauri walioutoa utakuwa nguzo muhimu katika utekelezaji wa bajeti hii na majukumu ya Wizara yangu na hivyo kusimamia utekelezaji wa diplomasia ya uchumi kwa ukamilifu zaidi kwa manufaa ya nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitumie fursa hii kuwashukuru kwa dhati Mheshimiwa Mahadhi Juma Maalim - Naibu Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa; Bwana John M. Haule, Katibu Mkuu; Balozi Rajabu H. Gamaha, Naibu Katibu Mkuu; Wakurugenzi, Mabalozi na Wafanyakazi wote wa Wizara yangu waliopo Makao Makuu, Ofisi yetu ya Zanzibar na katika Balozi zetu mbalimbali duniani kwa kunisadia na kuniwezesha kutekeleza vyema jukumu la kuiongoza Wizara na kutetea maslahi ya Taifa letu ndani na nje ya nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, shukurani za pekee ziwaendee wananchi na viongozi wa Mkoa wa Lindi, Wilaya ya Lindi na hasa wananchi wote wa Jimbo la Mtama. Napenda pia nimshukuru mke wangu Mama Dorcas Membe na watoto wetu kwa kunivumilia, kunitia moyo na nguvu katika kutimiza majukumu yangu ya kuitumikia nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa masikitiko na majonzi makubwa, kwa niaba ya wenzangu wote Wizarani naomba niungane na Wabunge wenzangu walionitangulia kutoa salamu za pole na rambirambi kwako, kwa Bunge na kwa familia ya Marehemu Salim Hemed Khamis, aliyekuwa Mbunge wa Chambani na Mjumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa

aliyefariki dunia katika kipindi cha mwaka huu wa fedha. Kwa kuwa ametutangulia mbele ya haki, wajibu wetu ni kumwomba Mwenyezi Mungu ailaze roho ya Marehemu mahali pema Peponi. Amina.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile, kwa masikitiko makubwa, napenda kutoa pole kwa Mhashamu Baba Askofu Josephat Lebulu wa Jimbo la Arusha kutokana na kitendo cha kigaidi cha kulipua bomu wakati wa sherehe za ufunguzi wa Kanisa la Mtakatifu Joseph Mfanyakazi, Parokia ya Olasit na kusababisha vifo na kujeruhi watanzania wenzetu. Nampa pia pole Mhashamu Baba Askofu Fransisco Padilla, Mwakilishi wa Papa nchini, Maaskofu na Mapadre pamoja na Waumini wote waliokuwepo siku hiyo kwa kunusurika katika tukio hilo. Aidha, natoa salamu za pole kwa Waumini wa Parokia hiyo na pia kwa wale wote waliopoteza ndugu, jamaa na marafiki zao. Tunawaombea Marehemu wote kwa Mola apumzishe roho zao mahali pema peponi. Amina. Tunawatakia majeruhi wote wapone haraka ili waweze kurejea katika shughuli za kujenga maisha yao na taifa letu kwa ujumla.

Mheshimiwa Naibu Spika, Napenda kuwakumbusha Watanzania wenzangu kuwa sifa moja kubwa tuliyonayo duniani ni kuwa na nchi yenye amani, usalama, mshikamano na upendo. Wote tunao wajibu wa kukataa, kukemea na kujiepusha na vitendo vyovyote vinavyoweza kuvunja amani na usalama wa Taifa letu. Tukatae udini, ukabila, ubaguzi wa rangi na jinsia.

Mheshimiwa Naibu Spika, tathmini ya Hali ya Dunia, kwa mujibu wa taarifa mbalimbali za Umoja wa Mataifa ni ya kutia moyo. Katika kipindi cha miaka kadhaa, dunia na hasa nchi zinazoendelea, zimeendelea kukabili kwa kasi kubwa matatizo ya ufukara na njaa, Elimu ya msingi, Unyanyasaji wa kijinsia, vifo vya watoto, Afya ya uzazi, magonjwa, uharibifu wa mazingira na vita vya wenyewe kwa wenyewe.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu ufukara na njaa duniani, tafiti nyingi zilizofanywa zinaonesha kuwa maeneo

mengi yaliyokumbwa na ukame au mafuriko, hasa katika nchi zinazoendelea yamekumbwa pia na matatizo ya njaa na ufukara. Katika Bara letu la Afrika, nchi za Kusini mwa Jangwa la Sahara zimeathirika kwa kiwango kidogo. Uwiano wa watu wanaoishi chini ya dola 1.25 kwa siku imeshuka kutoka asilimia 47 mwaka 1990 hadi kufikia asilimia 24 mwaka 2008. Hii ikimaanisha kushuka kutoka kwa watu zaidi ya bilioni mbili na kuwa chini ya watu bilioni 1.4. Kama hali hii itaendelea hivi, basi hali ya umasikini ya duniani itakuwa imepungua zaidi ya nusu kabla hata ya kufikia 2015.

Mheshimiwa Naibu Spika, lipo suala la elimu ya msingi kwa wote. Mpaka sasa namba ya watoto walioandikishwa kwenda shule hasa shule ya msingi imeongezeka kwa asilimia 58 mpaka 76 ya mwaka 1999 na mwaka 2010. Hii imekwenda sambamba siyo tu kwa waliondikishwa lakini pia kwa kumaliza shule. Vile vile uwiano wa kuandikishwa kati ya wavulana na wasichana umeongezeka kutoka asilimia 91 mwaka 1999 na kufikia asilimia 97 mwaka 2010.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo la unyanyasaji wanawake na kukoseshwa haki sawa kwenye elimu, kazi na uwezeshwaji bado limeendelea kuwepo na hatua mathubuti zinahitajika kuhakikisha hali hiyo inabadilishwa duniani kote.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye tatizo la vifo vya watoto walio chini ya miaka mitano duniani, Taarifa ya Dunia inaripoti kupungua kwa vifo hivyo kutoka zaidi ya vifo milioni 12 mwaka 1990 mpaka vifo milioni 7.6 mwaka 2010. Kwa nchi za Kusini mwa Jangwa la Sahara, hali imeendelea kuimarika kutoka asilimia 1.2 kwa mwaka kati ya 1990 - 2000 na kufikia asilimia 2.4 kati ya mwaka 2000 - 2010.

Mheshimiwa Naibu Spika, kumekuwa na mafanikio makubwa katika kutatua tatizo la Afya ya Uzazi duniani. Idadi ya vifo vinavyotokana na uzazi vimepungua karibu ya nusu ikilinganishwa kati ya mwaka 1990 na mwaka 2010. Pamoja na mafanikio haya, bado kunahitajika maboresho makubwa katika huduma za afya ya uzazi na watoto duniani.

Mheshimiwa Naibu Spika, bado dunia ina tatizo kubwa la Magonjwa hasa VVU na UKIMWI, Malaria na Kifua Kikuu. Kwa upande wa Ukimwi, mpaka kufikia mwisho wa mwaka 2010, takriban watu milioni 6.5 walikuwa wanapatiwa huduma za dawa za kupunguza makali ikiwa ni ongezeko la watu milioni 1.4. Ufahamu na uelewa wa ugonjwa huu umeonekana kuongezeka duniani kwa watu kujikinga, hivyo kupunguza maambukizi haya. Mafanikio pia yameonekana katika kupunguza vifo vya Malaria na Kifua Kikuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika tatizo la uharibifu wa Mazingira, hali ya uharibifu imepungua. Hii ni kutokana na nchi nyingi kuanzisha na kupanua maeneo ya misitu na vilevile kuweka na kutekeleza mikakati ya kuepusha uharibifu wa misitu iliyokuwepo. Hivyo, katika kipindi cha miaka 20 iliyopita, uharibifu umeshuka kutoka hekta milioni 8.3 kwa mwaka mpaka hekta milioni 5. 2 kwa mwaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati nikiwasilisha bajeti ya Wizara yangu mwaka 2012/2013 nililiarifu Bunge lako Tukufu kuwa hali ya kiuchumi kisiasa na kijamii duniani ilikuwa ya mashaka makubwa kutokana na mtikisiko wa uchumi ulioikumba dunia. Hali hii iliathiri ukuaji wa uchumi na utoaji wa huduma kwa nchi mbalimbali.

Kipindi hiki tunachokutana tena kwenye Bunge hili la Bajeti la Mwaka 2013/2014, hali ya uchumi duniani imeanza kutulia na kuleta matumaini. Matumaini haya yapo pia kwenye Bara letu la Afrika ambapo kati ya nchi kumi ambazo chumi zake zinakua kwa kasi duniani, nchi sita zinatoka Bara la Afrika, ikiwemo Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na utulivu huo wa kiuchumi, bado dunia inakabiliwa na hali tete ya migogoro ya kisiasa kwenye baadhi ya maeneo ya Afrika na Mashariki ya Kati. Migogoro hii pamoja na kuathiri ukuaji wa uchumi pia imesababisha mauaji ya watu wasiokuwa na hatia na wengine kwa maelfu kulazimika kuyahama makazi yao na kuwa wakimbizi ndani ya nchi zao au nje ya nchi.

Aidha, pamekuwepo na uharibifu mkubwa wa mali na miundombinu na hivyo kusababisha kuendelea kuongezeka kwa umasikini miongoni mwa wananchi wa nchi hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, hali ya kudorora kwa uchumi katika Bara la Ulaya imeendelea kuwa mbaya. Hali hii imesababishwa na mgogoro wa madeni *(sovereign debt crisis)* kwenye baadhi ya nchi zilizopo katika eneo linalotumia sarafu ya *Euro*. Mgogoro huo umeziathiri nchi kama vile Italia, Ureno, Uhispania na Ugiriki ambazo zimelazimika kutekeleza sera za kubana matumizi na kukopa zinazosimamiwa na Umoja wa Ulaya ili kuhakikisha kuwa chumi zao zinaimarika. Hali hiyo inaathiri misaada na mikopo kwa nchi zinazoendelea. Hata hivyo, inatarajiwa kwamba katika mwaka wa fedha 2013/2014 kutakuwa na mabadiliko ya kiuchumi na hivyo kuimarika kwa mahusiano katika sekta za utalii, uwekezaji na biashara.

Mheshimiwa Naibu Spika, uchumi wa Marekani umeanza kurudi katika hali nzuri baada ya kukumbwa na hali mbaya wakati wa mdororo wa uchumi uliosababishwa na udhibiti hafifu wa masoko ya mitaji na nyumba. Hatua zilizochukuliwa na Serikali ya Marekani chini ya uongozi wa Mheshimiwa Rais Obama zimesaidia kuanza kurejesha uchumi wa Taifa hilo kubwa duniani katika hali ya utulivu. Kuimarika kwa uchumi wa Marekani ni jambo jema kwa kuwa ukuaji wa uchumi huo unachochea biashara za kimataifa na uchumi wa dunia kwa ujumla.

Mheshimiwa Naibu Spika, msimamo wa Tanzania katika masuala muhimu ya Kimataifa, Palestina na Israel; Mgogoro wa Israeli na Palestina umekuwa ukiendelea kwa miongo mingi sasa. Mgogoro huo ulichukua sura mpya katika Mkutano Mkuu wa 67 wa Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa wa mwaka 2012 ambapo Palestina iliweza kupigiwa kura za kutosha na hivyo kuifanya kutambuliwa na Umoja wa Mataifa kama *Non-Member Observer*. Kwa ushindi huo, Palestina sasa inaweza kushiriki kwa masharti kwenye vikao mbalimbali vya Umoja wa Mataifa na Taasisi zake.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na ushindi huo wa Palestina, mwishoni mwa mwaka 2012, yalizuka mapigano makali kwenye Ukanda wa Gaza. Chanzo cha mapigano hayo ni kutokana na kitendo cha Israeli kuendelea kujenga makazi ya kudumu ya Walowezi katika maeneo ya Wapalestina na kujitanua ndani ya mipaka ya nchi hiyo. Mazungumzo ya kumaliza mgogoro huo kwa njia ya amani yalivunjika mwaka 2010.

Mheshimiwa Naibu Spika, msimamo wa Tanzania katika mgogoro kati ya Palestina na Israel unaeleweka. Sisi tunaunga mkono maazimio yote ya Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa la kuitaka Israel kuheshimu mipaka iliyochorwa mwaka 1967 ambayo inaipa Palestina hadhi ya kuwa nchi huru, kamili na inayoeleweka. Tunaunga mkono azimio linalotaka Israel na Palestina kuwa na suluhisho la nchi mbili huru na zinazoheshimiana, yaani *A Two States Solution.*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa Syria, hali ya kisiasa bado ni tete ambapo kuna mapigano makali kati ya majeshi ya Serikali na majeshi ya waasi. Mgogoro huu ulioanza tarehe 15 Machi, 2011 kwa maandamano ya nchi nzima yalilenga kumshinikiza Rais aliyepo madarakani Mheshimiwa Bashar Al-Assad kuachia madaraka.

Baada ya jitihada ya kumwondoa Rais Assad kwa njia ya maandamano kushindikana, waasi walianzisha mapigano. Umoja wa Nchi za Kiarabu, Marekani na Umoja wa Ulaya walikuwa miongoni mwa nchi za kwanza kukemea matumizi ya silaha kali dhidi ya waandamanaji na baadaye waasi. Serikali ya Rais Assad imeendelea kuungwa mkono na nchi za Urusi, China na Iran ambazo zimekuwa zikisisitiza umuhimu wa kutumia njia za kidiplomasia ili kufikia suluhu ya mgogoro huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, hadi kufikia katikati ya mwaka 2012, mapigano hayo yalisambaa katika miji mikubwa ya Damascus na Aleppo na kusababisha vifo vya watu takriban 90,000; watu milioni nne kubaki bila makazi kama ilivyoripotiwa na Umoja wa Mataifa; na pia watu milioni

1.5 kukimbilia nchi za jirani kama wakimbizi. Katika juhudi za kutatua mgogoro wa Syria, Umoja wa Mataifa ulimteua Bw. Lakhdar Brahimi kuwa mjumbe maalum wakusimamia amani nchini humo. Hatua nyingine iliyochukuliwa na Umoja wa Mataifa hivi karibuni ni kuzileta pande zote mbili zinazohasimiana katika meza ya mazungumzo.

Mheshimiwa Naibu Spika, msimamo wa Tanzania katika mgogoro huu wa Syria ni kuhakikisha kuwa kunapatikana utatuzi wa amani wa kudumu bila kutumia nguvu. Tanzania haikubaliani kabisa na mataifa yanayotaka kutumia nguvu ili kumtoa Rais Assad madarakani njia ambayo ilitumika na kuleta matatizo makubwa katika nchi za Libya, Tunisia na Misri. Tunaunga mkono juhudi za Umoja wa Mataifa, Marekani na Urusi za kuzikutanisha pande mbili kwa mazungumzo ya amani.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu matatizo ya Sahara Magharibi na Morocco; Sahara Magharibi lilikuwa koloni la Hispania, baada ya Mataifa Makuu kugawana Afrika huko Berlin, mwaka 1884.

Mheshimiwa Naibu Spika, kati ya mwaka 1966 hadi 1973, Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa lilipitisha maazimio saba, yaliyosisitiza umuhimu wa Sahara Magharibi kujiamulia hatima yake. Aidha, hukumu iliyotolewa na Mahakama ya Kimataifa ya Haki *(ICJ)* mwishoni mwa mwaka 1975 haikubaini ushahidi wowote kuwa Sahara Magharibi ilikuwa sehemu ya Morocco.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuondoka kwa Hispania pasipo kukabidhi madaraka kwa watu wa Sahara Magharibi kulitoa mwanya kwa Morocco kuikalia Saharawi kwa mabavu, ikidai kuwa eneo hilo ni sehemu ya himaya yake kwa sababu ukoo wa Kifalme wa Morocco ulitokea eneo hilo kabla ya ukoloni. Hatua hiyo ya Morocco ilipelekea wananchi wa Saharawi kuingia katika harakati za ukombozi kwa kuanzisha kikundi cha *POLISARIO* cha kudai uhuru kwa njia ya mapambano.

Mheshimiwa Naibu Spika, kufuatia jitihada zilizofanywa na Jumuiya ya Kimataifa, hususan Umoja wa Mataifa na *OAU* wakati ule au *AU* sasa, Mwaka 1991, mapambano kati ya POLISARIO na Morocco yalisitishwa, baada ya kusainiwa kwa Mkataba wa Amani *(Settlement Plan).* Umoja wa Mataifa uliandaa mpango wa kura ya maoni ili kuamua hatima ya Taifa hilo; lakini utambuzi wa wanaostahili kupiga kura ikawa kikwazo na kura hiyo haikupigwa. Morocco ilitaka wavamizi wake katika eneo hilo nao waruhusiwe kupiga kura.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika jitihada za kutekeleza mpango wa kura ya maoni, kati ya mwaka 1997 hadi 2012, Umoja wa Mataifa uliwatumia Bw. James Baker, Bw. Peter Van Walsum na Bw. Christopher Ross kama wawakilishi maalum katika juhudi za kutafuta suluhu ya kudumu ya mgogoro huo. Jitihada zilizochukuliwa na wasuluhishi hao hazikuweza kuzaa matunda kutokana na kila upande kung'ang'ania msimamo wake. Kwa sasa Morocco inapinga jitihada zozote za Wananchi wa Saharawi kujipatia uhuru wao na badala yake inataka nchi hiyo kuwa sehemu ya Majimbo yake ya Kusini.

Mheshimiwa Naibu Spika, siku zote Tanzania imejikita katika misingi ya kulinda uhuru wa kujiamulia mambo wenyewe, kuheshimu mipaka ya nchi na uhuru wa kisiasa, kulinda uhuru, haki za binadamu, usawa, demokrasia na utawala bora. Hivyo, tumeungana na nchi za Umoja wa Afrika na juhudi za Umoja wa Mataifa katika kuunga mkono Wananchi wa Sahara Magharibi kupewa haki ya kuamua hatima yao, kupitia kura ya maoni chini ya usimamizi wa Umoja wa Mataifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Tanzania haina uhasama na Morocco, lakini inapinga kitendo cha Morocco kuendelea kuikalia Sahara Magharibi kimabavu. Tanzania inaendelea kuishauri Serikali ya Morocco kurejea kwenye Umoja wa Afrika ili suala hili lijadiliwe na wao wakiwa kama sehemu ya Umoja huu. Aidha, tunazidi kuisihi Morocco

itekeleze pendekezo la kura ya maoni ili Wananchi wa Sahara Magharibi waamue hatima yao wenyewe.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kosovo; baada ya Tanzania kufuatilia kwa makini kuhusu kusambaratika kwa iliyokuwa Yugoslavia na nchi zote saba zilizokuwa zinaunda Shirikisho la Yugoslavia kujitangazia Uhuru wao na kuunda Serikali zao na Mahakama ya Kimataifa ya Haki *(ICJ)* ya kuruhusu Kosovo kuwa na haki ya kutangaza Uhuru wake kama nilivyoripoti katika Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama mwezi Aprili, 2012. Tanzania kama ilivyofanya kwa Polisalio au Sahara Magharibi, inaungana na nchi 98 Duniani kuitambua Kosovo, kwani, mazingira ya mgogoro wa Kosovo yanafanana na yale ya mgogoro wa Jamhuri ya Sahara Magharibi na tunaziomba nchi zingine pia kufanya hivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Somalia; baada ya takriban miongo miwili ya vita vya wenyewe kwa wenyewe, hali ya amani na usalama imeanza kurejea nchini Somalia. Serikali ya Mpito ya Somalia iliyoongoza nchi hiyo tangu mwaka 2004 ilifikia ukomo mwezi Agosti, 2012. Bunge jipya la Somalia lilipitisha Katiba mpya mwezi Agosti, 2012 na mwezi Septemba, 2012 lilimchagua Mheshimiwa Hassan Sheikh Mohamud kuwa Rais mpya wa nchi hiyo. Tangu kuingia madarakani kwa Serikali mpya, hali ya amani na usalama imeendelea kuimarika kutokana na kazi kubwa inayofanywa na Vikosi vya Umoja wa Afrika *(AMISOM),* ambavyo vimeendelea kufanya kazi nzuri na kubwa ya kuhakikisha nchi hiyo inapata amani ya kudumu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Tanzania inaipongeza Serikali mpya ya Somalia kwa kazi nzuri ya kuleta amani nchini humo. Tanzania itaendelea kushiriki katika vikao mbalimbali vinavyojaribu kuinusuru Somalia kutoka katika wimbi la matatizo ya vita vya wenyewe kwa wenyewe, uharamia na njaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wimbi la Mapinduzi Kaskazini mwa Afrika na Mashariki ya Kati nalo linapaswa

kusemwa. Kuanzia mwezi Desemba, 2010, nchi kadhaa za Kaskazini mwa Afrika na baadhi ya nchi za Mashariki ya Kati, zilikumbwa na mlolongo wa maandamano yenye kutaka mabadiliko ya kiutawala. Baadhi ya nchi zilizokumbwa na misukosuko hiyo ni Tunisia, Misri, Libya, Yemen, Bahrain na Syria. Aidha, misukosuko hiyo ilishinikiza kuondoka madarakani kwa baadhi ya tawala katika maeneo hayo. Nchi ambazo watawala wake waliachia ngazi ama kwa kuacha wenyewe au kwa kuondolewa kwa nguvu ni Tunisia, Misri, Libya na Yemen.

Mheshimiwa Naibu Spika, Tanzania haikuunga mkono mikakati ya kuondoa uongozi uliopo madarakani kwa nguvu na kwa kweli tulikuwa miongoni mwa nchi chache zilizosimama na kulaani vitendo hivyo. Hivi sasa tumeutaka Umoja wa Afrika kushughulikia kwa bidii juhudi za kurejesha Amani na Usalama nchini Libya, Tunisia na Misri.

Mheshimiwa Naibu Spika, nizungumzie pia kuhusu Madagascar. Nchi za *SADC* zimeendelea na juhudi zake za kusuluhisha mgogoro wa kisiasa nchini humo ambao umedumu kwa muda wa miaka mine sasa. Katika Kikao cha Troika cha Wakuu wa Nchi na Serikali wa *SADC* mwezi Desemba, 2012 Jijini Dar es Salaam, Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete, ambaye ni Mwenyekiti wa Troika aliombwa azungumze na Rais aliyeondolewa madarakani Mheshimiwa Marc Ravalomanana pamoja na Mheshimiwa Andry Rajoelina, Rais wa sasa wa Mpito wa Madagascar kuwasihi wasigombee katika Uchaguzi wa Rais utakaofanyika Mwezi Julai, 2013.

Mheshimiwa Naibu Spika, juhudi madhubuti za Mheshimiwa Rais Kikwete zilisaidia kuwashawishi Viongozi hao Wakuu wa kisiasa na wakaridhia ombi la kutogombea katika Uchaguzi Mkuu ili kusaidia mchakato wa kurejesha nchi yao katika utawala wa kikatiba. Hata hivyo, Mheshimiwa Ravalomanana alikiuka maelewano hayo kwa kumteua mke wake Bi. Lalao Ravalomanana kuwa Mgombea wa Chama cha Ravalomanana Mouvance katika Uchaguzi wa Rais. Aidha, naye Mheshimiwa Rajoelina

alipoyaona hayo naye alikiuka maelewano na kuamua kugombea Urais katika uchaguzi huo. Uamuzi wa Viongozi hao wawili unakinzana na Katiba pamoja na Sheria na Kanuni za Uchaguzi za Madagascar.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Mkutano wa Wakuu wa Nchi wa *SADC (SADC Organ Troika Summit)* uliofanyika tarehe 10 Mei, 2013 Jijini Cape Town, Afrika Kusini, chini ya Uenyekiti wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete, Mkutano ulilaani vikali uamuzi huo na pia kuilaani Mahakama Maalum ya Uchaguzi *(Special Electoral Court*) kwa kuidhinisha majina ya wagombea hao kinyume na Sheria na Kanuni za Uchaguzi. Aidha, iliwataka Viongozi watatu, hususan Mheshimiwa Andry Rajoelina, Lalao Ravalomanana na Didier Ratsiraka, ambaye alikuwa Rais wa zamani wa Madagascar, wasisimame tena katika uchaguzi ujao. Uchaguzi huo umepangwa kufanyika tarehe 24 Julai, 2013 kulingana na kalenda ya Uchaguzi nchini Madagascar. Tanzania ina matumaini kwamba, Viongozi hao wataheshimu ushauri waliopewa.

Mheshimiwa Naibu Spika, msimamo wa Tanzania ni kwamba, hakukuwa na busara kwa Viongozi wa zamani, Rais wa Serikali ya mpito Mheshimiwa Andry Rajoelina, Bw. Didier Ratsiraka na Mama Lalao Ravalomanana mke wa Rais aliyetolewa madarakani kugombea urais. Kujiingiza kwa Viongozi hao kwenye uchaguzi, kutaleta matatizo makubwa ya kiusalama.

Mheshimiwa Naibu Spika, hali ya eneo la Mashariki ya Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo (DRC) imeendelea kuwa tete kwa majeshi ya kundi la waasi la M23 kuendelea kushambulia Wananchi na hivyo kusababisha kuanza kuongezeka kwa wimbi la wakimbizi. Kundi hili la waasi limeendelea kushambulia Wananchi wasio na hatia kwa kuua watoto, kulazimisha watoto kujiunga na kundi hilo, kubaka akina mama, kuiba na kufanya vitendo vingi vya kinyama visivyokubalika na Jumuiya ya Kimataifa. Hali hii imesababisha uvunjifu mkubwa wa haki za binadamu. Nchi

za Afrika na Dunia kwa ujumla zimeshindwa kuendelea kuvumilia kuona maovu hayo yakitendeka na hivyo kufanya maamuzi ya kuimarisha Jeshi la Umoja wa Mataifa la kulinda amani.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na hali hiyo na historia ya nchi yetu kwenye harakati za ukombozi Duniani, Tanzania imeshiriki kikamilifu katika kufikia uamuzi wa kutuma Kikosi cha Kulinda Amani cha *SADC* nchini DRC. Tanzania ilikuwa ni nchi ya kwanza kujitolea kutoa Kikosi Kimoja cha Wanajeshi ambao watashiriki katika zoezi la kulinda amani nchini DRC na hivi ninavyozungumza vijana wapo kule.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa, tarehe 28 Machi, 2013, Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa lilipitisha Azimio Namba 2098 la mwaka 2013 linaloruhusu kuundwa na kupelekwa Kikosi Maalum *(Force Intervention Brigade - FIB)* huko Mashariki ya DRC. Kwa kuanzia, *FIB* inatarajiwa kutekeleza jukumu lake kwa kipindi cha mwaka mmoja hadi tarehe 31 Machi, 2014 ambapo Baraza la Usalama litajadili tena uwezekano wa *FIB* kuendelea na majukumu yake, kulingana na hali ya amani itakavyokuwa imefikia wakati huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kikosi hicho chenye Wanajeshi 3,069 kinaundwa na nchi za Tanzania, Afrika Kusini na Malawi. *FIB* itaongozwa na Tanzania, ambayo jumla ya Wanajeshi wake katika kikosi hicho watakuwa takriban 1,283. Gharama za kupeleka vikosi hivyo DRC zitalipwa na Umoja wa Mataifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na masuala mengine, malengo makuu ya *FIB* yanajumuisha; kudhibiti kujipanua kwa M23 na vikundi vingine vya waasi Mashariki ya DRC; kuvinyang'anya silaha vikundi hivyo; na hatimaye kutokomeza harakati za uasi katika eneo hilo la DRC ili kuwezesha kurejea kwa muunganiko wa kijamii na majadiliano yatakayopelekea kufikiwa amani ya kudumu nchini humo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Tanzania imechukua hatua hizo kwa kuwa inaamini amani na usalama ndiyo msingi wa maendeleo, bila amani na usalama hakuna maendeleo. Vilevile, kukosekana kwa amani kwenye nchi jirani kama ilivyo DRC kuna athari kubwa za kiuchumi, kisiasa, kiusalama na kijamii kwa nchi yetu. Majeshi yetu sasa yapo Kongo na kutokana na nidhamu yao ya hali ya juu yamepokelewa kwa shangwe kubwa huko Goma mara yalipowasili. Ni matumaini yetu kuwa, msimamo na uamuzi huo utaleta amani ya kudumu nchini Kongo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nizungumzie kuhusu Zimbabwe. Kwa muda mrefu Tanzania imekuwa mstari wa mbele katika juhudi za kusuluhisha mgogoro wa kisiasa nchini Zimbabwe. Baada ya kumalizika kwa zoezi la kutengeneza Rasimu ya Katiba Mpya, Timu ya Waangalizi wa Uchaguzi ya *SADC* ilipelekwa nchini humo kusimamia zoezi la upigaji wa kura ya maoni kuhusu Katiba Mpya. Nikiwa Kiongozi Mkuu wa Timu ya Uangalizi, niliizindua rasmi tarehe 10 Machi, 2013 Jijini Harare, Zimbabwe. Zoezi la upigaji wa kura ya maoni lilifanyika tarehe 16 Machi, 2013 ambapo matokeo yalionesha kuwa asilimia 95 ya Wananchi wa Zimbabwe wanaunga mkono Katiba Mpya. Kwa ujumla, zoezi hili lilifanyika katika mazingira ya amani na usalama. Hivi sasa, mchakato wa Uchaguzi Mkuu umeanza na uchaguzi huo unatarajiwa kufanyika mwaka huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, msimamo wa Tanzania ni kwamba, kwa kuwa Katiba mpya ya Zimbabwe sasa imepatikana baada ya Kura ya Maoni kufanyika na Mheshimiwa Robert Mugabe, Rais wa Zimbabwe kuipitisha rasmi, Tanzania na nchi zote za *SADC* zitaheshimu matokeo yoyote ya uchaguzi huo ambao tunategemea utakuwa huru na wa haki.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Sudan Kusini; licha ya kuwepo kwa changamoto kadhaa hususan zinazohusu umiliki wa Jimbo la Abyei, uhusiano kati ya Sudan na Sudan Kusini umeanza kuimarika. Mwezi Machi, 2013, Sudan Kusini ilianza tena kusafirisha mafuta yake kupitia Port Sudan

baada ya kusitisha usafirishaji mwezi Desemba, 2011. Pamoja na mafanikio haya, Umoja wa Afrika kwa kupitia Jopo lake Maalum *(AUHIP),* umeendelea na jitihada za kutafuta ufumbuzi wa changamoto zilizobaki, hususan mizozo kuhusu Majimbo ya Abyei, Southern Kordofan na Blue Nile.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunapongeza hatua ya hivi karibuni ya Jenerali Omar Al Bashir, Rais wa Sudan, kumtembelea Mheshimiwa Salva Kiir, Rais wa Sudan Kusini na kufanya nae mazungumzo ya amani. Aidha, tunaunga mkono jitihada za Mheshimiwa Thabo Mbeki, Rais mstaafu wa Afrika Kusini za kuzipatanisha nchi hizo ili zimalize uhasama na kuishi pamoja kama jirani wema.

Mheshimiwa Naibu Spika, nchini Mali nako, kufuatia mapinduzi ya mwezi Machi, 2012 na kuibuka kwa vitendo vya kigaidi vilivyotishia umoja wa kitaifa wa nchi hiyo, Umoja wa Afrika kwa kushirikiana na Jumuiya ya Uchumi ya Nchi za Afrika Magharibi *(ECOWAS)*, zilipeleka ombi kwenye Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa (UM) la kutumwa Kikosi cha Kulinda Amani nchini Mali. Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa lilikubali ombi hilo na mwezi Januari, 2013, Kikosi cha Kimataifa kutoka nchi za Afrika *(African-led International Support Mission to Mali-AFISMA)*, kilipelekwa nchini Mali kusaidiana na Majeshi ya Ufaransa yaliyoingia nchini humo mwanzoni mwa mwezi Januari, 2013.

Mheshimiwa Naibu Spika, tangu kupelekwa kwa *AFISMA* kushirikiana na Majeshi ya Ufaransa, maeneo yaliyokuwa yametekwa na magaidi yamerejeshwa kwenye himaya ya Serikali. Hali hii imetoa fursa ya kuendelea kwa mchakato wa amani na kurejesha utawala wa kidemokrasia, ambapo uchaguzi wa Rais unatarajiwa kufanyika mwezi Julai, 2013.

Mheshimiwa Naibu Spika, Tanzania iliunga mkono hatua ya Ufaransa kupeleka majeshi nchini Mali kupambana na waasi. Tulisisitiza pia umuhimu wa Umoja wa Afrika kupeleka majeshi yake badala ya kutegemea

majeshi ya nje kuleta amani na utulivu wa kudumu Barani Afrika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama Bunge lako Tukufu linavyoelewa, tujikumbushe wenzetu wa Malawi wanadai kuwa Ziwa Nyasa lote ukiacha sehemu waliyokubali kugawana na Msumbiji ni mali yao. Tanzania kwa upande mwingine tunadai Ziwa hilo ni mali yetu wote na kwamba mpaka wake upo katikati ya Ziwa kama ulivyo mpaka wa Msumbiji na Malawi kwenye Ziwa hilo hilo. Huu ndiyo msimamo wa Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi sasa suala la mgogoro huo lipo mikononi mwa Jukwaa la Marais Wastaafu wa Afrika na wa *SADC* likiongozwa na Mheshimiwa Joaquim Chissano, Rais Mstaafu wa Msumbiji. Hatua hiyo ilifikiwa kufuatia mchakato wa majadiliano ya awali kati ya nchi zetu mbili kutokuzaa matunda. Tanzania imekwishawasilisha andiko lenye hoja zake kuhusu mgogoro huo kwa Mwenyekiti wa Jukwaa hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, pande mbili zote zimekubaliana hatutafanya shughuli yoyote kwenye mpaka huo na hasa katikati ya mpaka huo mpaka mgogoro huu utakapopatiwa ufumbuzi. Tanzania tunaamini kuwa tutashinda katika kesi hii kwa sababu tuna kila aina ya ushahidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi cha Mwaka wa Fedha wa 2012/2013, Wizara ikishirikiana na Balozi za Tanzania, Taasisi nyingine za Serikali, Sekta Binafsi na Washirika wa Maendeleo, imeendelea kuratibu utekelezaji wa Sera ya Mambo ya Nje katika kuvutia wawekezaji, watalii na kutafuta fursa za masoko ya bidhaa zetu mbalimbali duniani ili kukuza uchumi na kuleta maendeleo. Utekelezaji wa Diplomasia ya Uchumi unazingatia kwa kiasi kikubwa vipaumbele vya Mpango wa Kwanza wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano (2011/2012 – 2015/2016).

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nitumie fursa hii kueleza kwa mifano michache kutoka katika Sekta za Afya, Kilimo, Mifugo na Uvuvi, Viwanda, Miundombinu na Uchukuzi jinsi Wizara yangu inavyotekeleza diplomasia ya uchumi katika kufanikisha Mpango wa Kwanza wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano (2011/2012 – 2015/2016).

Mheshimiwa Naibu Spika, Sekta ya Afya: Napenda kulifahamisha Bunge lako Tukufu kuwa, Wizara imeendelea kutetea masuala ya afya, hususan afya ya uzazi katika ngazi ya kimataifa. Kutokana na niliyoyaeleza mwanzo wa hotuba yangu, Wizara yangu inaamini hali ya Dunia itaimarika zaidi kama kutakuwepo na sekta madhubuti ya Afya. Katika kuendeleza jitihada hizi, Mheshimiwa Rais Jakaya Mrisho Kikwete, pamoja na mambo mengine mengi, alishiriki kwenye uzinduzi wa ufadhili wa Dola za Marekani milioni nane kutoka kwa *Bloomberg Philanthropies* na Bwana na Bibi Bengt Agerup mwezi Oktoba mwaka 2012 mjini New York, Marekani. Fedha hizo zitatumika kuboresha vituo vya afya vijijini. Lengo la mpango huu, ni kuongeza na kuboresha upatikanaji wa huduma za afya za dharura kwa Wanawake wajawazito na pia kuendesha mafunzo kwa maafisa tabibu wasaidizi na wakunga kwenye maeneo ya upasuaji wa dharura kwa akina mama wanaojifungua. Natumia fursa hii kwa mara nyingine kuwashukuru *Bloomberg Philanthropies* na Bwana na Bibi Bengt Agerup kwa ushirikiano wao.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Sekta ya Kilimo, pamoja na mambo mengine, Wizara yangu imeendelea kutafuta fursa za masoko kwa bidhaa za kilimo. Katika Mwaka wa Fedha wa 2012/2013, tumefanikiwa kushawishi mamlaka za Chakula za Jamhuri ya Watu wa China kukubali tumbaku inayozalishwa nchini kwetu kuingia kwenye soko la China, ambalo ndilo soko kubwa kuliko yote duniani katika matumizi ya tumbaku. Vilevile, China hununua tumbaku kwa bei ya juu kuliko nchi nyingine ambazo hununua asilimia 46 ya tumbaku yote duniani.

Mheshimiwa Naibu Spika, hizi ni habari njema kwa wakulima wa tumbaku nchini. Hivyo, nawaomba Waheshimiwa Wabunge wa maeneo yanayolimwa tumbaku nchini, kuwahamasisha wakulima wa maeneo yao watumie fursa hiyo kuongeza uzalishaji na ubora wake maana tumepata soko kubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sekta ya Mifugo na Uvuvi: Wizara yangu, pamoja na mambo mengine, iliratibu ziara ya ujumbe wa wataalam kutoka Wizara ya Kilimo na Uvuvi ya Oman uliokuja kutafuta fursa za biashara ya nyama na mazao yake hapa nchini. Mazungumzo kati ya Kampuni ya Ranchi za Taifa na wenzao wa Oman yanaendelea ili kufikia makubaliano ya uzalishaji, uboreshaji wa mifugo na uuzwaji wa nyama. Kufikiwa kwa makubaliano hayo, kutafungua fursa kwa nchi yetu kufaidika na biashara ya mifugo na hivyo kuboresha maisha ya wafugaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sekta ya Viwanda: Wizara yangu, pamoja na mambo mengine, imewezesha ujio wa kampuni ya Nitori ya Japan kuwekeza katika Sekta ya Viwanda. Kampuni hiyo itakayojenga kiwanda cha nguo nchini, imeshapatiwa eneo la kulima pamba huko Handeni, Tanga na eneo la kujenga kiwanda cha nguo katika Ukanda Maalum wa Uwekezaji uliopo Bagamoyo. Ofisi ya Waziri Mkuu na Wizara ya Viwanda na Biashara, wanaendelea kuratibu uwekezaji huo mkubwa nchini wenye thamani ya Dola za Kimarekani milioni 500, unaotarajiwa kutoa ajira kwa maelfu ya Watanzania. Vilevile Mradi huo utawahakikishia Wakulima wa Pamba nchini soko la pamba yao kwani kiwanda hicho kitakapokamilika kitahitaji kiasi cha tani laki moja za pamba kwa mwaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara kwa kushirikiana na Ubalozi wetu New Delhi, India, inalisaidia Shirika la Maendeleo ya Viwanda Vidogo Vidogo *(SIDO)* kupata fedha za msaada *(grant)* za kiasi cha Dola za Marekani milioni mbili kutoka Serikali ya India kwa ajili ya miradi ya kuvumbua na kuendeleza teknolojia ya viwanda vidogo vidogo itakayotumika nchini. Serikali imeomba msaada huo

utoke kama sehemu ya fedha za msaada kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo zilizoahidiwa na Waziri Mkuu wa India, Mheshimiwa Dkt. Manmohan Singh wakati alipofanya ziara hapa nchini mwezi Mei, 2011. Kwa hivi sasa, Wizara kupitia Ubalozi wetu New Delhi inaendelea kufuatilia kwa karibu upatikanaji wa fedha hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara yangu imeendelea kuvutia uwekezaji kutoka nchi mbalimbali katika Sekta za Miundombinu na Uchukuzi. Katika Mwaka wa Fedha wa 2012/2013, pamoja na mambo mengine, tumeivutia Kampuni ya *China Merchant Holding International* kuja kujenga bandari kubwa ya kisasa (*4th generation port)* huko Bagamoyo. Sambamba na ujenzi wa bandari, kampuni hiyo itajenga eneo la Ukanda Maalum wa Uwekezaji *(Export Processing Zone - EPZ),* mji wa kisasa pamoja na miundombinu ya barabara na reli.

Mheshimiwa Naibu Spika, tayari kampuni hiyo imefanya mazungumzo na Serikali kuhusu uwekezaji huo na wakati wa ziara ya Mheshimiwa Xi Jinping, Rais wa Jamhuri ya Watu wa China nchini, Serikali ilisaini Mkataba wa Mwongozo *(Framework Agreement)* na Kampuni hiyo ya *China Merchant* kwa ajili ya kukamilisha majadiliano na kuanza kutekeleza Miradi hiyo. Ofisi ya Waziri Mkuu ndiyo inayoratibu mchakato wa mazungumzo hayo. Pamoja na mambo mengine, Mradi huo utatoa ajira za moja kwa moja kwa maelfu ya Watanzania, kuliingizia Taifa mapato kwa njia ya kodi na mrabaha na kwa kiasi kikubwa kutapunguza foleni katika Jiji letu la Dar es Salaam.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika hotuba yangu ya mwaka jana, nililiarifu Bunge lako Tukufu kuwa, tunaendelea kuishawishi Serikali ya Japan kukubali ombi la Serikali yetu kuhusu ufadhili wa ujenzi wa barabara za kupita juu *(flyovers)* katika makutano ya Barabara za Nyerere na Mandela katika eneo la *TAZARA.* Hatimaye katika Mkutano uliofanyika Arusha mwezi Mei, 2012 kati ya Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Rais wa *JICA,* Japan ilikubali ombi hilo. Tayari

Serikali kupitia Wizara ya Fedha, imeingia Mkataba na Serikali ya Japan wa kufanya maandalizi ya awali ya barabara hizo za juu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara yangu imeweza kushawishi nchi mbalimbali rafiki kuweza kusaidia ujenzi wa Miradi ya Maji kwa Wananchi. Mtakumbuka kwa mfano, wakati wa ziara ya Mheshimiwa Jose Manuel Barroso, Rais wa Kamisheni ya Umoja wa Ulaya hapa nchini mwezi Julai, 2012 Mheshimiwa Rais Kikwete alifungua Mradi wa Maji wa Swaya Mkoani Mbeya, ambao utasaidia idadi ya Wananchi wapatao 490,000 hadi mwaka 2017. Thamani ya Mradi huo ni kiasi cha shilingi bilioni 79.5, kati ya fedha hizo shilingi bilioni 36.9 zilichangiwa na Umoja wa Ulaya, shilingi bilioni 13.5 zilitoka Serikali ya Ujerumani na kiasi kilichobaki cha shilingi bilioni 29.1 zilichangiwa na Serikali ya Tanzania yenyewe. Aidha, Wizara yangu imefanikisha upatikanaji wa mkopo wa Dola za Marekani 178.25 milioni kwa ajili ya Mradi wa Kusambaza Maji Safi katika Mikoa ya Dar es Salaam na Pwani. Tayari Mkataba wa mkopo huo umekwishasainiwa tarehe 2 Oktoba, 2012 baina ya Serikali na Benki ya Dunia.

Mheshimiwa Naibu Spika, natumia fursa hii kuzishukuru nchi zote na Mashirika yote ya Kimataifa kwa kusaidia ujenzi wa miradi mbalimbali katika Sekta ya Maji nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara imeendelea kuandaa, kuratibu na kusimamia ushiriki wa nchi yetu katika Mikutano ya Kikanda na Kimataifa, kuimarisha mahusiano ya kimataifa hususan, Umoja wa Mataifa na Taasisi zake pamoja na Mashirika ya Kimataifa ya Maendeleo na yale ya kifedha duniani. Katika Mwaka wa Fedha wa 2012/2013, Wizara yangu iliratibu ushiriki wa Tanzania kwenye mkutano wa Baraza la Uchumi na Jamii la Umoja wa Mataifa *(ECOSOC);* Mkutano wa 67 wa Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa *(UNGA);* Mkutano wa kujadili uanzishwaji wa Malengo ya Maendeleo Endelevu; Mkutano wa kuanzisha Mkataba wa Biashara ya Silaha Duniani; na Mkutano wa

Kamisheni ya Hali ya Wanawake ya Umoja wa Mataifa. Mikutano hiyo ilifanyika Makao Makuu ya Umoja wa Mataifa, New York, Marekani.

Mheshimiwa Naibu Spika, mikutano mingine ni ile ya Kilele cha Uzazi wa Mpango *(Family Planning Summit)* iliyofanyika London, Uingereza; na ule wa Umoja wa Mataifa kuhusu Mabadiliko ya Tabianchi *(COP18)* uliofanyika Doha, Qatar. Katika Mkutano wa Kilele cha Uzazi wa Mpango, Nchi Wahisani na Makampuni ya Kimataifa yaliahidi kuchangia utekelezaji wa mipango ya uzazi wa mpango kwa jumla ya Dola za Marekani bilioni 2.6 kwa kipindi cha miaka minane.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kuratibu ushiriki wa Tanzania kwenye mikutano mbalimbali nje ya nchi, Wizara pia iliratibu, kuandaa na kusimamia mikutano iliyofanyika hapa nchini na ziara zilizofanywa na viongozi wa mashirika na taasisi mbalimbali za Umoja wa Mataifa na Mashirika mengine ya Maendeleo ya Kimataifa. Katika Mwaka wa Fedha wa 2012/2013, Tanzania ilikuwa mwenyeji wa Mkutano wa Tano wa Kimataifa wa Masuala ya Kinga na Chanjo *(GAVI);* Mkutano wa Kuzuia Mauaji ya Kimbari na Jukumu la Nchi Kulinda Wananchi wake; Mkutano wa Miliki Ubunifu kwa Kanda ya Afrika uliojulikana kama *'African Conference on the Strategic Importance of Intellectual Property (IP) Policies to foster Innovation, Value Creation and Competitiveness;* na Mkutano wa Baraza la Uchumi na Jamii la Umoja wa Mataifa katika ngazi ya Afrika uliojulikana kama *"ECOSOC Regional Preparatory Meeting for Africa".* Mikutano hii ilifanyika katika Jiji la Dar es Salaam.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na faida nyingine, mikutano hiyo imechangia sana katika kuitangaza Tanzania na vivutio vyake vya utalii, kuiingizia nchi fedha za kigeni na kuchochea ukuaji wa Sekta ya Utalii na huduma ambazo ndiyo yenye kutoa ajira kwa wingi na haraka.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Mwaka wa Fedha wa 2012/2013, Wizara yangu imefanikiwa kufungua Ubalozi

mmoja mpya na kurejesha moja ya Balozi zetu zilizofungwa mwanzoni mwa miaka ya tisini. Ubalozi mpya uliofunguliwa ni katika Visiwa vya Comoro na Ubalozi uliorejeshwa upo The Hague nchini Uholanzi. Tayari, Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, amekwishateua Mabalozi katika vituo hivyo. Vituo hivyo vitaongeza uwakilishi wetu, kutoa huduma mbalimbali kwa Watanzania waliopo ughaibuni na kuimarisha mahusiano na nchi hizo. Ni azma ya Serikali kuendelea kuongeza maeneo zaidi ya uwakilishi ili kudumisha mahusiano na kuendeleza masilahi ya Taifa letu nje.

Mheshimiwa Naibu Spika, Tume za Pamoja za Kudumu za Ushirikiano *(Joint Permanent Commissions - JPC),* zimeendelea kuwa chombo muhimu katika kutetea masilahi ya Tanzania kiuchumi na mengineyo nje. Kwa kutambua mchango wake katika kutekeleza Diplomasia ya Uchumi, Wizara imeendelea kuratibu vikao vya wadau wa ndani na nje ya nchi ili kutekeleza makubaliano mbalimbali yanayofikiwa kupitia Tume hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi cha Mwaka wa Fedha wa 2012/2013, Wizara kwa kushirikiana na wadau kutoka Wizara, Idara na Taasisi nyingine za Umma pamoja na Sekta Binafsi, ilifanikiwa kuratibu vikao vya Tume za Ushirikiano na nchi mbalimbali kama ifuatavyo:-

(i) Tanzania na Kenya: Kikao cha Pili cha Tume ya Kudumu ya Pamoja ya Ushirikiano kati ya Tanzania na Kenya kilifanyika kuanzia tarehe 9 hadi 10 Septemba, 2012 mjini Nairobi, Kenya. Kikao hicho kilipata fursa ya kutathmini hatua mbalimbali za utekelezaji wa maeneo ya ushirikiano yaliyokubaliwa katika Kikao cha Kwanza cha *JPC* cha mwaka 2009. Aidha, maeneo mapya ya ushirikiano yaliibuliwa. Nchi hizi mbili zinatarajia kunufaika na kikao hicho kupitia utekelezaji wa makubaliano yaliyofikiwa katika masuala yanayohusu Uhamiaji; Usalama; Menejimenti ya Utumishi wa Umma; Afya; Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto; Kilimo; Miundombinu; Viwanda; Biashara na Masoko;

(ii) Tanzania na Uturuki: Mkutano wa Tume ya Ushirikiano wa Kibiashara kati ya Tanzania na Uturuki ulioratibiwa kwa pamoja kati ya Wizara yangu na Wizara ya Viwanda na Biashara ulifanyika jijini Dar es Salaam tarehe 23 hadi 26 Novemba, 2012. Mkutano huo ulikuwa ni sehemu ya utekelezaji wa makubaliano ya Mkataba mama wa Ushirikiano wa Kibiashara kati ya Tanzania na Uturuki uliosainiwa tarehe 18 Novemba, 2010. Tume hiyo ya Pamoja ya Ushirikiano wa Kibiashara ina jukumu la kuainisha na kupendekeza maeneo ya ushirikiano yenye lengo la kuhamasisha ukuaji wa biashara, utalii na uwekezaji kati ya Tanzania na Uturuki;

(iii) Tanzania na Oman: Kikao cha kwanza cha *JPC* kati ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Oman kilifanyika jijini Dar es Salaam kuanzia tarehe 24 hadi 25 Februari, 2013. Kikao hicho kilijadili fursa mbalimbali za uwekezaji na ushirikiano kati ya nchi hizo mbili. Maeneo ya ushirikiano yaliyokubaliwa ni pamoja na Kilimo, Uvuvi na Mifugo, Nishati na Madini, Viwanda, Biashara, Miundombinu, Usafirishaji, Elimu, Afya, Maji na Utamaduni. Vilevile, Mkataba wa Ushirikiano katika masuala ya kisiasa kati ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Oman ulisainiwa. Mkataba huo utaziwezesha nchi hizi kushirikiana katika masuala ya Kidiplomasia na Kimataifa yenye maslahi kwa pande zote mbili;

(iv) Tanzania na Kuwait: Tanzania na Kuwait zimeendelea kuwa na uhusiano mzuri, ambapo miradi mikubwa ya miundombinu kama barabara, nishati na viwanda ilifadhiliwa na Mfuko wa Maendeleo wa Kuwait *(Kuwait Fund).* Barabara inayounganisha Mikoa ya Kusini na Daraja la Mkapa zilijengwa kwa msaada wa fedha za Mfuko huo. Aidha, viwanda vya *MWATEX, SPM Mgololo*, Bwawa la Mtera na miradi mbalimbali ilifadhiliwa na Mfuko huu kati ya mwaka 1975 na 2010. Mfuko huu ulichangia takribani Dola za Marekani milioni 192 katika kipindi hicho.

Kufuatia ziara ya Mheshimiwa Rais hivi karibuni nchini Kuwait, nchi zetu mbili zimeingia ukarasa mpya kwa kuweka

saini Makubaliano ya Kuanzisha Tume ya Pamoja ya Kudumu ya Ushirikiano *(JPC).* Makubaliano hayo yanatoa fursa za uwekezaji, biashara na ushirikiano katika Sekta za Elimu na Afya.

Tayari Kuwait imeidhinisha kiasi cha Shilingi milioni 815 kwa ajili ya kugharamia upembuzi yakinifu wa Barabara ya Chaya – Nyahua ambayo ni kiungo muhimu cha barabara inayounganisha Mikoa ya Tabora, Katavi na Kigoma. Mfuko huo utagharamia ujenzi wa barabara hiyo kwa kiwango cha lami punde upembuzi yakinifu utakapokamilika. Aidha, Mfuko utatoa bakaa ya Dola za Marekani milioni 20 kwa ajili ya kukamilisha Mradi wa Maji wa Same – Mwanga – Korogwe. Vilevile, zipo fursa za ushirikiano katika Sekta ya Gesi na Mafuta ambapo Kuwait ina uzoefu mkubwa, hususan mafunzo kwa wataalam wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, *JPC* hizi zimekuwa na manufaa mbalimbali kwa nchi yetu hususan, kuongezeka kwa biashara, kubadilishana wataalam na kupatikana kwa nafasi za masomo. Kwa mfano, takwimu za Benki Kuu ya Tanzania zinaonesha kuwa biashara kati ya Tanzania na Kenya iliongezeka kutoka Dola za Marekani milioni 497.4 mwaka 2009 hadi kufikia milioni 561.2 mwaka 2011. Aidha, kwa upande wa Algeria, kila mwaka nchi yetu imekuwa ikipata ufadhili wa masomo hususan, fani ya sayansi katika vyuo vikuu nchini humo. Hivi sasa kuna takriban wanafunzi 200 wa Tanzania nchini Algeria.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi cha Mwaka wa Fedha wa 2012/2013, Wizara yangu iliratibu majadiliano kadhaa yaliyopelekea uwekwaji saini makubaliano ya mikataba mbalimbali kama ifuatavyo:-

(i) Makubaliano kuhusu Ushirikiano katika Sekta ya Usafiri wa Anga *(Bilateral Air Services Agreement – BASA)* kati ya Tanzania na Ujerumani. Mkataba huo ulisainiwa tarehe 18 Septemba, 2012. Kusainiwa kwa Mkataba huo kutaleta faida kubwa kwa Tanzania, ikiwemo ukusanywaji wa kodi itokanayo na ongezeko la abiria na mizigo, fursa

za kuingiza na kusafirisha bidhaa mbalimbali nje, ajira pamoja na kukuza utalii.

(ii) Mkataba wa Uenyeji kati ya Tanzania na Umoja wa Afrika kuhusu uanzishaji wa Makao Makuu ya Bodi ya Rushwa ya Umoja wa Afrika *(African Union Advisory Board on Corruption - AUABC).* Mkataba huo ulisainiwa wakati wa Mkutano wa Wakuu wa Nchi na Serikali Jijini Addis Ababa, Ethiopia mwezi Januari, 2013. Taasisi hii itakuwa na Makao yake Makuu Jijini Arusha.

(iii) Mkataba wa Uenyeji kati ya Tanzania na Taasisi ya Afrika ya Sheria za Kimataifa *(African Union Institute of International Law).* Mkataba huo ulisainiwa tarehe 12 Machi, 2013 Jijini Dar es Salaam. Taasisi hii itakuwa na Makao yake Makuu Jijini Arusha. Kwa Makao Makuu ya taasisi hizo kuwepo Jijini Arusha ni dhahiri kuwa, Arusha itaendelea kujitangaza vizuri kama kitovu cha utalii Tanzania na hivyo kuendelea kuvutia watalii wengi zaidi nchini.

(iv) Mkataba wa Kudhibiti Biashara ya Silaha za Kawaida. Napenda kulifahamisha Bunge lako Tukufu na Wananchi kuwa, Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ilishiriki kikamilifu katika mazungumzo ya Umoja wa Mataifa, New York, yaliyofikia makubaliano ya kuwa na Mkataba wa kudhibiti biashara ya silaha za kawaida *(Conventional Weapons-CWs)* unaojulikana kama *"Arms Trade Treaty."* Mkataba huo hautahusisha silaha za maangamizi, yaani silaha za nyuklia, kemikali na biolojia. Mazungumzo hayo ya mkataba wa silaha yalifanyika kuanzia tarehe 18 hadi 28 Machi, 2013 baada ya takriban miaka tisa ya majadiliano ambayo hayakuzaa matunda tangu mwaka 2004.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wataalam wetu kutoka Wizara, Idara na Taasisi mbalimbali za Serikali, vikiwemo Vyombo vyetu vya Ulinzi na Usalama, walihakikisha silaha ndogo ndogo na nyepesi, vipuri na risasi zinaingizwa kwenye mkataba na kupewa umuhimu stahiki.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa, ujenzi wa Kituo cha Mikutano cha Kimataifa cha Julius Nyerere *(Julius Nyerere International Convention Centre - JNICC)* umekamilika. Mheshimiwa Xi Jinping, Rais wa Serikali ya Jamhuri ya Watu wa China, alikabidhi rasmi Kituo hicho kwa Mheshimiwa Rais Jakaya Mrisho Kikwete wakati wa ziara yake ya Kitaifa nchini tarehe 25 Machi, 2013. Kituo hiki kitavutia mikutano mingi ya kimataifa nchini na hatimaye kuleta fursa mbalimbali za biashara.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kituo hiki kitakuwa chachu ya kukuza Utalii wa Mikutano *(Conference Tourism),* ambao ni moja ya nyenzo muhimu ya kutangaza na kukuza utalii. Kituo cha Mikutano cha Mwalimu Nyerere pia kitachochea ajira nyingi za moja kwa moja na nyingine zinatarajiwa kutengenezwa katika sekta mbalimbali za huduma.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara imeendelea kuratibu uhamasishaji na ushirikishwaji wa Watanzania waishio nje ya nchi *(Diaspora)* kuchangia maendeleo ya nchi. Napenda kukumbusha Bunge lako Tukufu kwamba, kama ilivyo katika nchi nyingine, suala la watu wenye asili ya nchi hii waishio ughaibuni tunaliangalia katika muktadha wa Uhamiaji na Maendeleo *(Migration and Development).* Kama nilivyotamka katika hotuba yangu mwaka uliopita, kipaumbele cha Wizara katika mchakato huu ni uwepo wa Sera ya *Diaspora* ili kuhakikisha Serikali na Taasisi zote husika zinakuwa na uelewa wa pamoja kuhusu mikakati bora itakayofanikisha lengo hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kulijulisha Bunge lako Tukufu kwamba, zoezi la kuandaa Sera hii limeanza. Mashauriano na wadau yanaendelea yakihusisha wadau wa ndani na wa nje ya nchi yetu, wakiwemo *Diaspora* wenyewe kupitia Jumuiya zao. Tunatarajia kulikamilisha zoezi hili mwaka ujao wa fedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka huu wa fedha, Wizara yangu imechukua jitihada za makusudi za

kupanua wigo kwa kuwafikia *Diaspora* waishio Canada na Oman. Mikutano na Watanzania hao iliandaliwa sanjari na ziara za Mheshimiwa Rais Jakaya Mrisho Kikwete katika nchi hizo mwezi Oktoba, 2012. Nchi hizi mbili, kwanza zina Watanzania wengi wanaojizatiti kiuchumi, kijamii na hata kisiasa. Pili, Serikali za nchi hizo zinaunga mkono jitahada zetu na zipo tayari siyo tu kuwawezesha ila kushirikiana na *Diaspora* hao kuchangia maendeleo ya nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo kubwa tunaloendelea kujifunza ni kwamba, Watanzania wengi waliopo Ughaibuni wanaathirika sana na suala la uraia wa nchi mbili. Kutokuwa na uraia wa nchi mbili kunawafanya wakose ajira za kueleweka, huduma za afya na elimu na kukosa kukopesheka katika nchi wanazoishi tofauti na wenzao. Wizara yangu katika maoni yake kwa Tume ya Katiba, ililipa suala la uraia pacha *(Dual Citizenship)* kipaumbele kwa kuwa tunaamini kabisa kwamba kufanya hivyo kutawawezesha Watanzania waliopo nje kuchangia kwa kiwango kikubwa maendeleo ya nchi yetu. Naomba Bunge lako Tukufu liunge mkono juhudi hizi.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi karibuni Mheshimiwa Rais alipata fursa ya kuhamasisha Watanzania waishio Ufaransa na Uholanzi na kuwahakikishia kuwa Serikali yake inatambua na kuthamini michango yao na hivyo, kuwahimiza wakumbuke nyumbani, wawekeze kadiri ya uwezo wao na wavutie washirika wao kuwekeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, Tanzania kwa mara nyingine tena imepata heshima kubwa baada ya Mtanzania, Luteni Jenerali Ignace Mella, kuteuliwa kuwa Mkuu wa Jeshi la *UNAMID* huko Darfur, nafasi ambayo ilikuwa inakaimiwa na Mtanzania mwingine Meja Jenerali Wynjones Kisamba. Itakumbukwa kuwa, kabla ya kukaimu nafasi hiyo iliyoachwa wazi na aliyekuwa Mkuu wa Jeshi hilo, Luteni Jenerali Patrick Nyamvumba kutoka Rwanda, Meja Jenerali Kisamba alikuwa ni Naibu Mkuu wa Jeshi hilo na napenda kumpongeza kwa kazi nzuri sana aliyoifanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, uteuzi wa Luteni Jenerali Ignace Mella unazidi kudhihirisha jinsi wapiganaji wa Jeshi letu wanavyofanya kazi kwa weledi na uhodari mkubwa ndani ya Jeshi hilo, suala ambalo lilithibitishwa na Mwakilishi Maalum na Mpatanishi Mkuu mpya wa *UNAMID,* Dkt. Mohamed Ibn Chambas, alipotembelea Tanzania mwezi Mei, 2013. Siyo jambo la kawaida kwa viongozi kutoka nchi moja kupokezana madaraka makubwa kama hayo kwenye Vikosi vya Ulinzi na Amani kwenye Umoja wa Mataifa, lakini kutokana na weledi wa kazi na utumishi uliotukuka, Tanzania imevunja utamaduni huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kulikumbusha Bunge lako Tukufu kuwa, tarehe 22 Desemba, 2010, Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa liliruhusu kuanzishwa Kituo cha Kumbukumbu za Mauaji ya Kimbari ya Rwanda Tawi la Arusha. Kituo hicho kina jukumu la kuhifadhi kumbukumbu na kuhitimisha kesi zitakazosalia baada ya iliyokuwa Mahakama ya Mauaji ya Kimbari ya Rwanda *(ICTR)* kumaliza kipindi chake mwaka 2014.

Mheshimiwa Naibu Spika, mafanikio ya *ICTR* bila shaka yameliongezea heshima Taifa letu katika Jumuiya ya Kimataifa. Siyo tu tuna haki ya kujivunia kuwa mwenyeji wa Mahakama ya *ICTR* bali pia tunawajibika kuienzi heshima hiyo. Msimamo huu ulipewa baraka zote na Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa kupitia Azimio Na. A/66/240A na B la mwaka 2012, ambayo yote kwa pamoja yaliainisha ulazima na uharaka wa kuanzisha makazi ya kudumu ya Kituo cha Kumbukumbu za Mauaji ya Kimbari ya Rwanda Tawi la Arusha *(International Residual Mechanism for International Criminal Tribunals - IRMCT)*, ikiwa ni pamoja na ujenzi wa Ofisi, Chumba cha Mahakama na jengo maalum la utunzaji nyaraka na kumbukumbu za *ICTR.*

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kulifahamisha Bunge lako Tukufu kuwa, tarehe 28 Machi, 2013, Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa liliidhinisha Mradi wa Ujenzi baada ya kukamilika kwa michoro ya awali na taratibu zote za awali za ujenzi. Tayari Baraza hilo limeshapokea na

kuidhinisha bajeti ya ujenzi wa Mradi huu ya kiasi cha Dola za Marekani milioni 8.7 na linategemea kutenga fedha zilizobaki Dola za Marekani milioni 5.7 katika Mwaka wa Fedha wa 2013/2014.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa uwekezaji huo, ni dhahiri kuwa, kiasi hicho cha fedha kitaingia kwenye uchumi wa nchi yetu. Hakuna shaka hata kidogo kuwa ujenzi huo utatoa ajira mpya rasmi na zisizo rasmi, utafungua fursa nyingine za uwekezaji pamoja na kutoa fursa kwa taasisi nyingine za Umoja wa Mataifa kujenga Ofisi zao katika eneo hilo. Ujenzi huo pia utaufanya Mkoa wa Arusha kuendelea kuwa kitovu cha utalii hususan, kwa wanataaluma kujifunza na kufanya tafiti mbalimbali kuhusiana na mauaji ya kimbari ya Rwanda na hivyo kuendelea kuifanya Arusha iwe Geneva ya Afrika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyoliarifu Bunge lako Tukufu mwaka jana kuwa, moja ya lengo letu kwa Mwaka wa Fedha wa 2012/2013 litakuwa ni kutoa kipaumbele katika maeneo ya ulinzi na ujenzi wa amani duniani kama sehemu ya utekelezaji wa Sera yetu ya Mambo ya Nje. Hivyo, Tanzania imeendelea kushiriki kikamilifu katika jitahada za kulinda amani duniani chini ya mwamvuli wa Umoja wa Mataifa. Mchango wetu katika ulinzi wa amani umeijengea nchi yetu sifa kubwa kutokana na nidhamu ya hali ya juu inayooneshwa na majeshi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nchi yetu ina askari wa kulinda amani nchini Lebanon kupitia *(UNIFIL),* Sudan ya Kusini kupitia *(UNMISS),* Cote d'Ivoire *(UNOCI),* Jimbo la Abyei kupitia *(UNISFA),* Jimbo la Darfur kupitia *(UNAMID)* na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo (DRC) kupitia *(MONUSCO).* Ushiriki wa nchi yetu kwenye shughuli za kulinda amani una manufaa mengi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni dhahiri kuwa, ushiriki wetu katika jitihada za kujenga na kulinda amani katika maeneo mbalimbali duniani, umeendelea kuipatia heshima kubwa nchi yetu mbele ya Jumuiya ya Kimataifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara imeendelea kuratibu na kusimamia masuala ya mahusiano kati ya nchi yetu na nchi mbalimbali duniani na mashirika ya kikanda na ya kimataifa. Viongozi mbalimbali wa nchi za China, Denmark, Liberia, Kenya, Uganda, Burundi, Madagascar, DRC, Zimbabwe, Saharawi, Benin, Somalia, Afrika Kusini, Msumbiji na Iran walitembelea Tanzania.

Vilevile, Viongozi wa Mashirika ya Kimataifa kama vile Shirika la Programu ya Chakula Duniani (*WFP*), Shirika la Nguvu za Atomiki Duniani *(IAEA),* Shirika la Haki Miliki Duniani *(WIPO),* Shirika la Wakimbizi Duniani *(UNHCR),* Shirika la Umoja wa Mataifa la Elimu, Sayansi na Utamaduni (*UNESCO*) na Umoja wa Ulaya *(EU)* walitembelea Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, ziara hizi zimechochea na kuimarisha ushirikiano kati ya nchi yetu na Mashirika ya Maendeleo ya Umoja wa Mataifa na mengineyo duniani hususan, katika sekta mbalimbali za kiuchumi na kijamii. Mathalan, ziara ya Bw. Yukiyo Amano, Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Nguvu za Atomiki Duniani iliambatana na uzinduzi wa *simulator* yenye thamani ya *Euro* 300,000.00 na *gamma camera* yenye thamani ya *Euro* 350,000.00 zilizonunuliwa na *IAEA* kwa kushirikiana na Serikali kwa ajili ya matibabu ya saratani katika Taasisi ya Saratani ya Ocean Road.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, Mkurugenzi huyo alikubali ombi la Serikali la kuchangia ununuzi wa mashine ya kisasa na ambayo itasaidia kupima na kutambua ugonjwa wa saratani kwa uhakika kabisa ijulikanayo kama *Liner Accelerator* ambayo itagharimu jumla ya Dola za Marekani milioni mbili.

Mheshimiwa Naibu Spika, mahusiano kati ya Tanzania na nchi za Umoja wa Ulaya, yameendelea kuimarika. Mahusiano haya mazuri yanathibitika kufuatia ziara ya Mheshimiwa Jose Manuel Barroso, Rais wa Kamisheni ya Umoja wa Ulaya, aliyoifanya nchini tarehe 21 na 22 Julai, 2012. Akiwa nchini, Mheshimiwa Barroso

alishuhudia utiaji saini wa mikataba sita kati ya Tanzania na Umoja wa Ulaya kwa ajili ya utekelezaji wa miradi katika sekta mbalimbali yenye jumla ya thamani ya *Euro* milioni 126.

Mheshimiwa Naibu Spika, miradi hiyo inahusisha Sekta ya Usafirishaji kwa njia ya Barabara *(Road Transport Sector and Policy Support Programme) Euro* milioni 45; Mradi wa Maji ambao uko katika utekelezaji wa Mpango wa Malengo ya Milenia *Euro* milioni 51; kuboresha Barabara za Vijijini Nchini *(Improvement of Rural Roads in Tanzania) Euro* milioni 22; Mpango wa kuzisaidia Taasisi za Kiraia katika kuleta maendeleo Zanzibar *(The Zanzibar Non-State Actor Support Programme) Euro* milioni 3; kuisaidia Ofisi ya Afisa Taifa *(Support to Office of the National Authorizing Office Phase II) Euro* milioni 2.5; na Mkataba wa Ushirikiano wa Kitaalam *(Technical Cooperation Facilities IV) Euro* milioni 2.5.

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na ziara za Viongozi wa Nchi na Mashirika mbalimbali kuja hapa nchini, Viongozi wetu wa Kitaifa pia walifanya ziara katika nchi za Ufaransa, Canada, Iran, Umoja wa Falme za Kiarabu *(UAE),* Kuwait, Rwanda, Burundi, Ghana, Uingereza, Uganda, Kenya, Korea Kusini, Zambia, Zimbabwe, Malawi, DRC, Cuba, Brazil, Oman, Mexico, Marekani, Uswizi, Ethiopia, Msumbiji, Uholanzi, Afrika Kusini na Italia. Ziara hizo zimefungua milango mipya ya mashirikiano kati ya nchi yetu na nchi hizo, kati ya Wananchi wa nchi zetu na kati ya sekta binafsi kutoka pande zote. Aidha, ziara hizo pia zimechochea na kukuza biashara na kuimarisha mahusiano.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara imetekeleza majukumu yake kwa ushirikiano na wadau wa maendeleo kutoka nchi na asasi mbalimbali za Kitaifa, Kikanda, Kimataifa pamoja na sekta binafsi. Naomba nitumie fursa hii kuwashukuru washirika wetu wote wa maendeleo ikiwa ni pamoja na Marekani, Uswisi, Ujerumani, Sweden, Ufaransa, Uholanzi, Uingereza, Ubelgiji, Japan, Finland, Norway, Italia, Ureno, Uhispania, Umoja wa Ulaya, Cuba,

Brazil, Urusi, China, Uturuki, Ireland, Canada, Kuwait, Australia, Oman, *UAE,* India, Malaysia, Korea Kusini, *UNDP, FAO, UNEP, UN-HABITAT, UNWTO, UNHCR, IOM, ILO, WHO, UNICEF, UNFPA, UNESCO, UNIDO, World Bank, IMF, IAEA* na *WWF.*

Kwa mwaka 2012/2013, pamoja na majukumu ya moja kwa moja ya utekelezaji wa Sera ya Mambo ya Nje, Tanzania pia inao wajibu wa kutekeleza majukumu ya Kikanda na Kimataifa ikiwa kama Mwanachama wa Jumuiya ya Kimataifa. Haya yote yamechangia kwa kiasi kikubwa katika kudumisha amani, ulinzi na usalama. Miongoni mwa majukumu hayo ni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Uenyekiti wa Tanzania katika Asasi ya Siasa, Ulinzi na Usalama ya *SADC* – Troika: Katika Mkutano wa Wakuu wa Nchi na Serikali wa Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Afrika *(SADC)* uliofanyika mwezi Agosti, 2012 nchini Msumbiji, Tanzania ilichaguliwa rasmi kuwa Mwenyekiti wa Asasi ya Siasa, Ulinzi na Usalama ya *SADC* kwa kipindi cha mwaka mmoja. Tangu uteuzi huo, kama ambavyo nimeeleza, Tanzania inashiriki kwa dhati katika juhudi za kusuluhisha migogoro ya kisiasa na usalama nchini Jamhuri ya Demokrasia ya Kongo (DRC), Madagascar na Zimbabwe. Baada ya kipindi cha mwaka mmoja, Tanzania itaendelea kuwa katika Asasi hiyo kwa kipindi kingine cha mwaka mmoja kama Mwenyekiti aliyemaliza muda wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ushiriki wa Tanzania katika Baraza la Ulinzi na Usalama la Umoja wa Afrika*;* mwezi Januari, 2012, Tanzania ilichaguliwa kuwa Mjumbe wa Baraza la Ulinzi na Usalama la Umoja wa Afrika kwa kipindi cha miaka miwili hadi mwaka 2014. Nchi yetu ilianza rasmi kutekeleza jukumu hilo tarehe 1 Aprili, 2012. Katika kipindi cha mwaka mmoja cha ujumbe wetu katika Baraza hilo, nchi yetu imeweza kushiriki kikamilifu katika jitihada mbalimbali za kutafuta suluhu ya migororo inayozikabili nchi za Sudan na Sudan Kusini, Somalia, DRC, Madagascar, Mali, Jamhuri ya Afrika ya Kati na Guinea Bissau.

Mheshimiwa Naibu Spika, Tarehe 22 Aprili, 2013, nchi yetu ilikuwa mwenyeji wa Mkutano wa Mawaziri wa Baraza la Amani na Usalama la Umoja wa Afrika ambao ulijadili hali ya siasa na usalama nchini Madagascar wakati ikielekea kwenye Uchaguzi Mkuu mwezi Julai, 2013. Lengo la Mkutano huo lilikuwa ni kuhakikisha kuwa, uchaguzi huo unafanyika kama ulivyopangwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, sanjari na ushiriki wetu kwenye Baraza la Ulinzi na Usalama la Umoja wa Afrika, nchi yetu imeendelea kuchangia harakati za kutatua migogoro Barani Afrika kwa kutuma vikosi vyake kwenye nchi mbalimbali. Hivi sasa nchi yetu ina kikosi kimoja *(battalion)* kwenye Vikosi vya Umoja wa Mataifa na Umoja wa Afrika vya Kulinda Amani huko Darfur *(UNAMID)* nchini Sudan. Nitumie fursa hii tena kulifahamisha Bunge lako Tukufu kwamba, Vikosi hivyo sasa vinaongozwa na Kamanda Mtanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, Tanzania imekuwa Mjumbe wa Kikundi Kazi cha Mawaziri wa Jumuiya ya Madola *(CMAG)* tangu Oktoba, 2011 wakati wa Mkutano wa Wakuu wa Nchi na Serikali wa Jumuiya ya Madola *(CHOGM)* uliofanyika Perth, Australia kwa kipindi cha miaka miwili.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama Mjumbe wa *CMAG*, Tanzania imeshiriki kikamilifu kwenye kutafuta ufumbuzi wa migogoro nchini Maldives ambapo kulikuwa na Mapinduzi Baridi na nchini Fiji ambapo kulikuwa na Mapinduzi ya Kijeshi. Usuluhishi unaendelea na tuna imani nchi hizi hatimaye zitarejea katika Utawala wa Kidemokrasia.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mkutano mkubwa wa Kimataifa wa Ushirikiano kwa Manufaa ya Wote *(Smart Partnership Dialogue - Global 2013)*, unaotarajiwa kufanyika hapa nchini kuanzia tarehe 28 Juni hadi tarehe 1 Julai, 2013 ni mwendelezo wa mikutano kama hii ambayo ilianza miaka kumi na tano iliyopita. Mikutano hii ilianzishwa na Jumuiya ya Madola kupitia taasisi yake inayoitwa *Commonwealth*

*Partnership for Technology Management (CPTM)* na kwa ushiriki mkubwa wa aliyekuwa Waziri Mkuu wa Malaysia, Dkt. Mahathir Mohammed.

Mheshimiwa Naibu Spika, mchakato wa majadiliano haya ulizinduliwa na Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, mwezi Mei, 2012 na tangu kipindi hicho mpaka sasa mikutano mbalimbali ya maandalizi imeendelea kufanyika kwa kuwashirikisha wadau kutoka Serikalini, Wafanyabiashara na Sekta Binafsi.

Mheshimiwa Naibu Spika, majadiliano hayo yanalenga kutoa fursa kwa jamii kukaa pamoja na kuzungumzia masuala mbalimbali ya maendeleo. Dhana hii ya majadiliano ya wazi kwa manufaa ya wote ni muhimu sana hasa kwa Viongozi kwa kuwa kadiri Kiongozi anavyopata maoni ya watu wengi, ndivyo maamuzi yake yatakavyokuwa sahihi zaidi na yatazingatia mahitaji ya makundi mbalimbali katika jamii. Kwa mfano, maamuzi ya Serikali yatakubalika kwa urahisi na Wananchi kwa sababu watakuwa wameshiriki katika kuyaandaa. Majadiliano kama haya ni fursa nyingine ya kushirikisha Wananchi katika kupanga mikakati ya utekelezaji wa Mpango wa Taifa wa Miaka Mitano na Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025 kwa kuzingatia maoni ya Wananchi ambayo yataleta faida kwa kila kundi la kijamii.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kitaifa, majadiliano haya yatahusisha makundi mbalimbali kutoka Serikalini, Wanasiasa, Wafanyabiashara, Wasomi, Wafanyakazi, Vijana, Wasanii na Wakulima ambao watakaa pamoja na kujadili masuala mbalimbali yanayohusu namna ya kutumia Sayansi na Teknolojia kwa ajili ya kuleta maendeleo katika sekta zote. Makundi haya yalipata fursa hiyo kupitia Mabaraza ya Mikoa na yale ya Wilaya yanayoratibiwa na Baraza la Taifa la Biashara *(TNBC)* ambako majadiliano yalifanyika kuanzia huko hadi ngazi za kitaifa kabla ya majadiliano ya kimataifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nitumie fursa hii kuwahimiza wadau wote wakiwemo Waheshimiwa Wabunge, kushiriki katika Jukwaa la Majadiliano ya Ushirikiano kwa Manufaa ya Wote.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nitumie fursa hii kuzungumzia ugeni mkubwa wa Kimataifa ambao nchi yetu imepokea na inatarajia kupokea katika historia ya miaka ya hivi karibuni. Ugeni huu umeonesha mafanikio makubwa ya kidiplomasia na mahusiano yetu na mataifa makubwa duniani. Nimpongeze Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kazi nzuri ya kufanikisha haya.

Mheshimiwa Naibu Spika, tarehe 24 na 25 Machi, 2013, Mheshimiwa Xi Jinping, Rais wa Jamhuri ya Watu wa China, alifanya ziara ya kitaifa nchini kwa lengo la kuimarisha uhusiano uliopo na wa muda mrefu kati ya Mataifa haya mawili. Ziara hiyo ilikuwa na umuhimu mkubwa hususan katika kuimarisha zaidi Ushirikiano na Urafiki wetu wenye historia ya udugu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Miradi mikubwa inayoendelea hivi sasa nchini kwa msaada wa China ni ujenzi wa bomba la gesi kutoka Mtwara hadi Dar es Salaam; utandazaji wa mkongo wa mawasiliano katika wilaya zote nchini; ujenzi wa Kituo cha kisasa cha tiba ya magonjwa ya moyo katika Hospitali ya Muhimbili; Ujenzi wa Kiwanda cha Chuma Liganga; na Ujenzi wa Kiwanja cha Ndege cha kimataifa Zanzibar. China pia imekuwa ikileta wataalam mbalimbali kufanya kazi nchini na imetoa nafasi mbalimbali za masomo na mafunzo kwa Watanzania. Kibiashara, Tanzania imenufaika kwa kupata soko la uhakika la bidhaa zake nchini China. Tunachohitaji kufanya ni kuongeza kasi ya uzalishaji ili tuweze kuuza bidhaa nyingi zaidi kwenye soko hilo kubwa duniani.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati wa ziara ya Mheshimiwa Rais Xi Jinping nchini, mikataba mbalimbali ipatayo 16 ilisainiwa katika maeneo ya Ushirikiano wa

Kiuchumi na Kitaalam kati ya China na Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kati ya China na Zanzibar; Misaada na Mikopo isiyo na riba na yenye riba nafuu kwa ajili ya uendelezaji wa miradi mbalimbali; Ujenzi wa Mkongo wa Taifa awamu ya tatu; Kukuza na Kulinda Uwekezaji; Ujenzi wa bandari na uendelezaji wa eneo maalum la uwekezaji wa viwanda Bagamoyo; Uhusiano wa kiutamaduni na uanzishaji wa Kituo cha Utamaduni cha Watu wa China nchini Tanzania. Kati ya mikataba 16 iliyosainiwa, mikataba miwili ilikuwa ya Zanzibar na ilihusu ukarabati wa Hospitali ya Abdullah Mzee; na ununuzi wa vifaa vya kukagua makontena bandarini.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa, nchi yetu itapata tena fursa nyingine ya kutembelewa na Mheshimiwa Barack Obama, Rais wa Marekani, ambaye anatarajia kufanya ziara nchini kuanzia tarehe 1 hadi 2 Julai, 2013. Hii ni ziara ya kwanza kwa kiongozi huyo kuifanya nchini Tanzania na pia ni ziara yake ya kwanza kutembelea Bara la Afrika katika kipindi cha awamu ya pili ya uongozi wake. Ziara ya Rais Obama nchini, itakuwa ni fursa nyingine kwa Tanzania kuimarisha uhusiano wake na Marekani ambao kwa sasa ni mzuri kuliko wakati wowote katika historia ya nchi zetu mbili. Ziara hiyo pia itasaidia nchi yetu kujitangaza Duniani na kujiweka mahali pazuri katika kukuza Uchumi, Biashara, Utalii na Uwekezaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, nchi yetu inatarajia pia kupokea wageni katika ngazi ya Wakuu wa Nchi na Serikali kutoka nchi za Uganda, Zimbabwe, Sudan Kusini, Swaziland, Benin, Lesotho, Sri-Lanka, Namibia, Malaysia, Gabon, Botswana, Zambia, Comoro na Afrika Kusini, waliothibitisha kushiriki kwenye Mkutano mkubwa wa Kimataifa wa Ushirikiano kwa Manufaa ya Wote *(Smart Partnership Dialogue - Global 2013).* Aidha, Wizara inaendelea kufuatilia kwa karibu kuhusu uthibitisho wa Wakuu wengine wa Nchi na Serikali katika Mkutano huo. Vile vile, kati ya Mwezi Juni na Julai mwaka huu, Rais wa Sri-Lanka Mheshimiwa Mahinda Rajapaksa na Waziri Mkuu wa Thailand, Mheshimiwa Yungluck Shinawatra, watafanya ziara rasmi nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, maadhimisho ya miaka hamsini ya Umoja wa Afrika. Tarehe 25 Mei 2013, Umoja wa Afrika uliadhimisha miaka hamsini (50) tangu kuanzishwa kwa uliokuwa Umoja wa Nchi Huru za Kiafrika *(Organization of African Unity – OAU).* Katika kipindi hicho Bara la Afrika limepiga hatua kubwa kijamii, kiuchumi na kisiasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ikumbukwe kwamba Baba wa Taifa Mwalimu Julius Kambarage Nyerere alikuwa ni miongoni mwa viongozi waanzilishi wa Umoja wa Afrika mwanzoni mwa miaka ya sitini na alitumia muda wake mwingi katika harakati za ukombozi na Dar es Salaam ikawa ndio Makao Makuu ya ukombozi wa Afrika. Hivyo, Tanzania tuna kila sababu ya kujivunia na kusherehekea kazi na mafanikio ya Umoja huo katika kipindi cha miaka hamsini iliyopita. Katika kilele cha maazimisho ya miaka hamsini ya Addis Abbab, Mzee wetu Baba wa Taifa, Mwalimu Julius Kambarage Nyerere na Mzee wetu Simba wa Vita, Rashid Mfamu Kawawa na Mzee Sebastian Chale, walitambuliwa kwa mchango wao katika harakati za ukombozi kwa kupewa Tuzo Maalum. Wizara yangu kwa kushirikiana na Jumuiya ya Mabalozi wa Afrika waliopo hapa nchini tuliadhimisha siku hiyo kwa maandamano, mihadhara na maonesho ya vitu mbalimbali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, utawala na maendeleo ya watumishi Wizarani na kwenye Balozi zetu. Pamoja na majukumu mengine, Wizara pia imeendelea kutekeleza jukumu la kusimamia utawala na maendeleo ya watumishi Wizarani na katika Balozi za Tanzania kwa lengo la kuboresha maslahi, elimu na kuweka mazingira mazuri ya kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hivi sasa, Wizara yangu kwa upande wa rasilimali watu ina jumla ya watumishi mia nne ishirini na moja (421) ambapo kati yao watumishi mia mbili thelathini na tano (235) wapo Makao Makuu ya Wizara; watumishi kumi na sita (16) wapo Ofisi ya Mambo ya Nje, Zanzibar; na watumishi mia moja hamsini na saba (157) wapo kwenye Balozi zetu. Aidha, watumishi kumi na watatu (13) wapo likizo bila malipo wengi wao wakiwa katika utumishi wa Mashirika ya Kikanda na Kimataifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi cha mwaka 2012/2013, jumla ya watumishi tisini na watano (95) walihudhuria mafunzo ndani na nje ya nchi. Kati ya hao, arobaini (40) walihudhuria mafunzo ya muda mrefu na watumishi hamsini na watano (55) walihudhuria mafunzo ya muda mfupi. Mafunzo hayo yameongeza ujuzi kwa watumishi hao na hivyo kuboresha utendaji wa kazi Wizarani.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi hicho, jumla ya watumishi ishirini na mmoja (21) walipandishwa vyeo baada ya kutekeleza majukumu yao vizuri pamoja na kutimiza masharti ya Miundo ya Utumishi inayosimamia kada zao. Vilevile, watumishi sitini na sita (66) walithibitishwa kwenye vyeo walivyopandishwa baada ya kumaliza muda wa majaribio na mtumishi mmoja mmoja alibadilishwa cheo baada ya kupata sifa za kumwezesha kubadilisha kada.

Mheshimiwa Naibu Spika, watumishi watano (5) walibadilishwa vyeo baada ya kuhamishia utumishi wao Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kutoka Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na kumaliza muda wa miaka minne (4) wa kipindi cha kuazimwa. Kati ya watumishi hao watatu (3) ni miongoni mwa watumishi ishirini na wanane (28) waliopandishwa vyeo kwa mwaka wa fedha 2012/2013. Watumishi wawili (2) waliobakia watapandishwa vyeo kabla ya mwisho wa mwaka ambapo watakuwa wametimiza masharti ya Muundo wa kada ya Maafisa Mambo ya Nje.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara yangu inamiliki majengo na viwanja mbalimbali nje. Nia na madhumuni ya kuwa na majengo/viwanja hivyo ni kuiondolea Wizara adha kubwa ya kulipa pango ya majengo ya Ofisi na makazi ya Maafisa. Aidha, baadhi ya majengo yatakayojengwa au kununuliwa yatatumika kama vitega uchumi ambapo yataongeza mapato ya Serikali na hivyo kutuwezesha kuendesha Balozi zetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kuwa na usimamizi mzuri na madhubuti wa majengo haya, Wizara yangu ipo katika mchakato wa kuunda chombo kitakachosimamia majengo

hayo (*Special Purposes Vehicle*) kwa kushirikiana na Wizara ya Ujenzi. Tayari rasimu ya Makubaliano ya kuunda chombo hicho yamekwishaandaliwa kwa hatua za mapitio ya pande zote mbili.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara yangu pia imeziagiza Balozi zetu kuwasilisha andiko la miradi ya Ujenzi na Ununuzi wa Majengo ya Ofisi na Makazi itakayotekelezwa kwa kutumia mikopo kutoka katika mabenki au taasisi za fedha kwa kupitia utaratibu wa *Mortgage Financing.*

Mheshimiwa Naibu Spika, Taasisi zilizo chini ya Wizara. Chuo cha Diplomasia *(CFR).* Baada ya kupata usajili wa Baraza la Ithibati ya Elimu ya Ufundi (*National Council of Technical Education-NACTE),* Chuo kimezidi kutambulika na kuimarika katika utoaji taaluma, tafiti na ushauri katika masuala ya utatuzi wa migogoro, itifaki, diplomasia ya uchumi, mkakati na menejimenti ya mahusiano ya nje. Idadi ya wanafunzi imeongezeka kutoka 510 mwaka wa masomo 2012/2013 hadi kufikia 590 katika mwaka wa masomo 2013/ 2014. Aidha, Chuo kimeendelea kuishauri Wizara yangu katika masuala ya kidiplomasia na pia kutoa mafunzo maalum kwa watumishi wa Wizara, mabalozi na wenza wao.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kujiimarisha, Chuo kimejikita katika kutekeleza Mpango Mkakati wa Miaka Mitano 2012/2013-2016/2017 kwa kuboresha miundombinu. Miundombinu hiyo ni pamoja na ujenzi wa majengo yatakayotumika kufundishia, ofisi za wanataaluma na maktaba. Lengo kuu likiwa nikuongeza ufanisi katika utoaji taaluma, kuajiri wataalam wenye sifa, tafiti na utoaji ushauri wa kitaaluma katika fani za mahusiano ya kimataifa, diplomasia ya uchumi na mafunzo ya kimkakati na mahusiano ya kimataifa. Mipango hiyo inatarajiwa kukiwezesha Chuo kujitegemea katika utekelezaji wa majukumu yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kituo cha Kimataifa cha Mikutano cha Arusha *(AICC).* Kituo cha Kimataifa cha Mikutano cha Arusha *(AICC),* kimeendelea kufanya kazi vizuri

na kutoa mchango wake katika kuitangaza nchi na kulipatia taifa mapato. Katika kipindi cha miaka mitatu iliyopita, Kituo kimeweza kuvutia mikutano 64 kwa mwaka. Kwa mwaka wa fedha ulioishia Juni 2012, Kituo kiliweza kuwa mwenyeji wa mikutano ya kimataifa 22 na ya kitaifa 49 iliyoingiza nchini wageni wanaokadiriwa kufikia 42,000.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa kwa mara nyingine tena, Kituo kimeendelea kupata hati safi ya hesabu zake zilizoandaliwa na kukaguliwa kwa wakati kwa kipindi kilichoishia tarehe 30 Juni 2012. Kituo kilipata faida ghafi ya shilingi 232,218,223.00 na kinaendelea kufanya shughuli zake kwa ufanisi bila kutegemea ruzuku kutoka Serikali Kuu. Kwa mwaka wa fedha 2011/2012, Kituo kilitunukiwa tuzo ya uandaaji bora wa Hesabu inayotolewa na Bodi ya Wahasibu na Wakaguzi wa Hesabu *(NBAA).*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi cha mwaka 2013/2014, Kituo kimepanga kuingiza mapato ya shilingi 10,361,275,621.00 kutokana na vyanzo vyake mbalimbali vya mapato na kinategemea kukopa shilingi bilioni 3.25 kwa ajili ya miradi ya maendeleo na mali za kudumu zenye thamani ya shilingi 3,265,170,000.00. Baada ya kutoa gharama za uendeshaji, Kituo kinategemea kupata ziada ghafi ya shilingi 117,258,436.00.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara yangu itaendelea kuhakikisha kuwa *AICC* inatimiza moja ya jukumu lake la kupangisha Asasi za Kimataifa. Taasisi mbili za Umoja wa Afrika (*AU Advisory Board on Corruption* na *African Institute of International Law*) zilizoanzishwa hivi karibuni, makao makuu yao yapo katika kituo hiki cha *AICC*. Kwa kuzingatia upatikanaji wa nafasi baada ya Mahakama ya Mauaji ya Kimbari ya Rwanda *(UN-ICTR)* kupunguza shughuli zake na Jumuiya ya Afrika Mashariki *(EAC)* kurudisha baadhi ya ofisi zake na kuhamia kwenye jengo lao jipya, Kituo kitaendelea kupokea taasisi nyingine za kimataifa zitakazopenda kuweka makao yake jijini Arusha.

Mheshimiwa Naibu Spika, natumia fursa hii

kuipongeza Bodi mpya ya Wakurugenzi wa Kituo, Menejimenti na wafanyakazi wote wa *AICC* na pia kuwatakia mafanikio mema katika kazi zilizo mbele yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mpango wa Kujitathmini kwa Utawala Bora Barani Afrika *(APRM).* Katika Mkutano wa Wakuu wa Nchi na Serikali wa Umoja wa Afrika uliofanyika Januari 2013 jijini Addis Ababa, kulikuwepo na matukio mawili makubwa kwa nchi yetu ambayo ni; kuchaguliwa kuwa mjumbe wa Kamati ya Marais ya kusimamia Utekelezaji wa Mpango wa *New Partnership for African Development (NEPAD);* na Dkt. Edward Hoseah, Mkurugenzi Mkuu wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa Nchini (TAKUKURU) kuchaguliwa kwa kipindi cha pili kuwa mjumbe wa Bodi ya Ushauri ya Kupambana na Rushwa Barani Afrika.

Mheshimiwa Naibu Spika, shughuli kubwa iliyofanyika katika kipindi cha mwaka wa fedha 2012/2013 ilikuwa ni kukamilisha taarifa ya tathmini ya nchi yetu katika eneo la Utawala Bora na hatimaye kuiwasilisha kwa Wakuu wa Nchi na Serikali wa Umoja wa Afrika wanaoshiriki Mpango huo. Ninayo furaha kubwa kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa tarehe 26 Januari 2013, Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania aliwasilisha taarifa hiyo kwenye Kikao cha Wakuu wa Nchi na Serikali ambao nchi zao zinashiriki katika Mpango wa Kujitathmini *(APRM)* huko Addis Ababa, Ethiopia.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa Taarifa ya *APRM* kuhusu Tanzania ilipokelewa vizuri na Wakuu wa Nchi na Serikali wanaoshiriki Mpango wa Kujitathmini. Nchi yetu ilitajwa kuwa mfano wa kuigwa katika kudumisha amani, kujenga umoja, demokrasia na uhuru wa watu, muungano na utatuzi wa migogoro ya ndani ya nchi. Vilevile, nchi yetu ilihimizwa kuzifanyia kazi changamoto za migogoro ya wakulima na wafugaji, imani za kishirikina, kuhakikisha manufaa ya kukua kwa uchumi yanawafikia wananchi na kutoa elimu kwa umma kuhusu Mipango na Sera za Serikali. Hatua iliyo mbele yetu ni kuisambaza taarifa hiyo kwa wadau na kutekeleza ushauri uliotolewa wakati wa uwasilishaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kukamilika kwa tathmini ya awali ya nchi na taarifa kuwasilishwa kwa Wakuu wa Nchi na Serikali wa Umoja wa Afrika wanaoshiriki Mpango wa *APRM*, kwa sasa *APRM* Tanzania inatarajiwa kutekeleza kazi zifuatazo:-

(i) Kuingiza Mpango Kazi wa Kitaifa wa *APRM* kwenye Mpango wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano na Mipango ya Muda wa Kati ya Wizara, Idara na Taasisi za Serikali katika maeneo mahsusi ya utawala bora yanayohitaji mabadiliko ya Kisera, Kisheria na Kitaasisi;

(ii) Kuwafahamisha Wananchi kupitia programu mbalimbali kuhusu matokeo ya Taarifa ya Nchi ya Utawala Bora (*Country Review Report* - *CRR*);

(iii) Kufuatilia utekelezaji wa Mpango Kazi wa Kitaifa wa kuondoa changamoto za utawala bora zilizobainishwa;

(iv) Kuandaa taarifa za kila mwaka za utekelezaji wa hatua mbalimbali za kuondoa changamoto zilizojitokeza kwa ajili ya kuziwasilisha katika vikao vya Umoja wa Afrika vinavyohusu masuala ya *APRM*; na

(v) Kufanya maandalizi ya kufanyika tathmini ya utawala bora nchini baada ya miaka minne.

Mheshimiwa Naibu Spika, mapato na matumizi ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2012/2013. Katika mwaka wa fedha wa 2012/2013, Wizara yangu ilipangiwa kutumia kiasi cha shilingi bilioni tisini na nane, mia tatu thelathini na tisa milioni na mia saba na saba elfu (98,339,707,000.00). Kati ya fedha hizo, shilingi bilioni themanini na moja, milioni mia sita themanini na sita, mia tano na tatu elfu (81,686,503,000.00) ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na shilingi bilioni kumi na sita, mia sita hamsini na tatu milioni na mia mbili na nne elfu (16,653,204,000.00) ni kwa ajili ya shughuli za maendeleo. Katika fedha zilizotengwa kwa Matumizi ya Kawaida (*Recurrent Budget)*, shilingi bilioni sabini na sita, milioni mia

tano arobaini na mia tano ishirini na moja elfu (76,540,521,000.00) ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo *(OC)* na bilioni tano, milioni mia moja arobaini na tano na mia tisa themanini na mbili elfu (5,145,982,000.00) ni kwa ajili ya mishahara.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara kupitia Balozi zake ilitarajia kukusanya kiasi cha shilingi bilioni kumi na sita, milioni mia nane themanini na mbili, mia mbili thelathini moja elfu, mia tatu na thelathini (16,882,231,330.00) kama maduhuli ya Serikali. Hadi kufikia tarehe 30 Machi 2013, Wizara imefanikiwa kukusanya kiasi cha shilingi bilioni kumi na tatu, milioni mia tano kumi na tatu, mia saba hamsini na nne elfu na mia moja arobaini na nne (13,513,754,144.00) ikiwa ni makusanyo ya maduhuli Balozini. Kiasi hicho cha makusanyo ya maduhuli ni sawa na asilimia 80 ya makisio ya makusanyo yote ya maduhuli kwa mwaka wa fedha 2012/2013.

Mheshimiwa Naibu Spika, hadi kufikia tarehe 30 Machi 2013, Wizara ilikuwa imepokea kutoka Hazina jumla ya shilingi bilioni tisini na tatu, milioni mia sita hamsini na moja, mia sita kumi na nne elfu na mia moja sabini na saba (93,651,614,177.00). Kati ya fedha hizo kiasi cha shilingi bilioni themanini, milioni mia tatu tisini, mia tatu thelathini na mbili elfu na mia tano sabini na saba (80,390,332,577.00) ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na kiasi cha shilingi bilioni kumi na tatu, milioni mia mbili sitini na moja, mia mbili themanini na moja elfu na mia sita (13,261,281,600.00) ni kwa ajili ya bajeti ya maendeleo. Kiasi hiki ni sawa na asilimia 79.63 ya bajeti yote ya Maendeleo iliyotengwa kwa Wizara kwa mwaka wa fedha 2012/2013.

Mheshimiwa Naibu Spika, changamoto mbalimbali zilizojitokeza katika utekelezaji wa majukumu ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2012/2013. Wizara imekuwa ikikabiliwa na changamoto mbalimbali katika utekelezaji wa majukumu yake. Baadhi ya changamoto hizo ni za kiutawala na nyingine ni za kibajeti kama mlivyosikia hivi karibuni kupitia Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali. Mathalan, Balozi zetu za Abu Dhabi na Muscat zilipata Hati

zenye Shaka (*Qualified Audit Opinion*) kufuatia matumizi mabaya ya fedha zilizotokana na makusanyo ya maduhuli.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa Abu Dhabi, Hati hiyo yenye shaka ilisababishwa na Mhasibu *(Local staff)* wa Ubalozi mdogo Dubai kupeleka kiwango pungufu Benki kwa kiasi cha Dola za Marekani 20,000.00 (sawa na shilingi milioni thelathini na tatu) katika kipindi cha Julai 2011 hadi Desemba, 2012. Aidha, kwa upande wa Muscat, maduhuli ya kiasi cha Reale za Oman 20,965.00 hayakupelekwa Benki ndani ya wakati uliostahili kama kanuni za fedha zinavyoelekeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kukabiliana na changamoto hizo, Wizara ilimtuma Mkaguzi wa Ndani kwenda kufanya ukaguzi wa kina na baada ya taarifa yake kuthibitisha matumizi mabaya ya fedha hizo, hatua za kinidhamu zimechukuliwa kwa mujibu wa Sheria za U.A.E. za kukata mshahara wa Mhasibu huyo kila mwezi ili kufidia fedha zilizopotea. Mara zoezi hilo litakapomalizika, Wizara itachukua hatua ya kumwachisha kazi mtumishi huyo ambaye ni raia wa U.A.E.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa Muscat, Mkaguzi wa Ndani wa Wizara baada ya Uchunguzi wake, ilibainika kuwa maduhuli hayo ya Dola za Marekani 50,000.00 yalitumika na Ubalozi kulipia matumizi muhimu ya Ubalozini kama vile maji, umeme na mafuta. Iwapo fedha hizo zingaliingizwa benki katika kipindi hicho wasiwasi ilikuwa kwamba benki ingezichukua fedha hizo kufidia madeni mengine ya riba ambayo benki hukata kila fedha zinapoingia. Pamoja na tatizo hilo lililitokana na ufinyu wa Bajeti, Wizara imesisitiza umuhimu wa Ubalozi kuweka fedha benki na kuzingatia kanuni za fedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, Balozi zetu za Brussels, Geneva, London, Tokyo na Stockholm zilipata Hati Safi zenye Masuala ya Msisitizo (*Unqualified Opinion With Matters of Emphasis*) kutokana na matumizi nje ya ukomo wa bajeti uliowekwa. Matumizi hayo kwa kiasi kikubwa yalitokana na

ufinyu wa bajeti ikilinganishwa na mahitaji halisi ya Balozi hizo hususan katika maeneo ya kimkataba ambayo Balozi hazina budi kulipa. Hivyo, badala ya kusubiri zifungiwe huduma hizo muhimu au kufukuzwa katika ofisi na makazi na hivyo kuharibu taswira ya Tanzania nje, ililazimu kutumia sehemu ya maduhuli kulipia huduma za kimkataba ikiwemo kulipia kodi za pango la Ofisi na Makazi, Maji, Umeme, huduma za simu na bima ya afya.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na changamoto hizo za matumizi ya fedha zaidi ya ukomo uliowekwa Balozini, Balozi 11 zilipata Hati Safi za Ukaguzi (*Unqualified Opinion Without Matters of Emphasis*) ikilinganishwa na Balozi tatu tu zilizopata Hati kama hiyo kwa mwaka 2010/2011.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kulihakikishia Bunge lako Tukufu kwamba, Wizara kwa kushirikiana na Taasisi nyingine za Umma ikiwemo Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali inachukua hatua mbalimbali ili kuhakikisha inaboresha miundombinu katika Balozi zetu pamoja na maslahi ya watumishi Balozini. Moja ya hatua hizo ni kushirikiana na Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, Wakala wa Majengo wa Serikali, Wizara ya Ujenzi, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali na Wizara ya Fedha ili Balozi zetu ziweze kutumia utaratibu wa *Mortgage Financing* kwa ajili ya kuboresha majengo ya Ofisi na Makazi Balozini na hivyo kupunguza matumizi ya fedha za bajeti kwa ajili ya kulipia pango za Majengo ya Ofisi na Makazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya mazungumzo ya muda mrefu hatimaye Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma imepitisha Kanuni Mpya za Utumishi wa Nje ambazo zitaanza kutumika Julai, 2013. Ni matumaini ya Wizara yangu kuwa, matumizi ya Kanuni hizo yataboresha maslahi ya watumishi Balozini na hivyo kuongeza uwajibikaji na tija katika majukumu yao ya kila siku.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kuhakikisha changamoto hizo zinapungua, Wizara yangu imeendelea

kushirikiana na Wizara ya Fedha kuhakikisha kuwa kodi za nyumba, bili za simu, maji, umeme, bima na huduma mbalimbali katika Balozi zetu zinalipwa kwa wakati. Vilevile, ukomo wa bajeti ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2013/2014 umeongezeka. Fedha zilizoongezeka kwa kiasi kikubwa zitatumika kulipia maeneo muhimu na ya kimkataba yaliyopo Balozini na kulipa mafao ya watumishi wenyeji waliomaliza muda wao katika Balozi zetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, malengo ya Wizara katika mwaka wa fedha 2013/2014. Katika mwaka wa fedha 2013/2014, Wizara itaendelea kutekeleza majukumu yake ya msingi kama yalivyoainishwa katika hotuba hii. Aidha, Wizara itaendelea kutekeleza malengo yake iliyojiwekea kulingana na Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2010-2015. Msisitizo utakuwa ushiriki wa Wizara katika utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano 2011/2012 – 2015/2016. Naomba kusisitiza na kukumbusha Wizara nyingine kuwa Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa ni Wizara unganishi na hivyo inahusika na uratibu wa miradi mingi inayotekelezwa na Wizara, Idara na Taasisi nyingine mbalimbali za Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyoeleza hapo awali, Wizara yangu itaendelea kuratibu utekelezaji wa mipango mbalimbali ya maendeleo ya Taifa kwa kufuatilia na kuchambua hali ya kisiasa, kiuchumi na kiusalama ilivyo duniani kwa lengo la kuimarisha mahusiano ya kisiasa, kiuchumi na kibiashara kati yetu na mataifa mengine. Vilevile, Wizara yangu itaendelea kuutumia uzoefu iliyoupata katika utekelezaji wa Diplomasia ya Uchumi kuendelea kutafuta fursa mbalimbali za kiuchumi na biashara huko nje.

Mheshimiwa Naibu Spika, maelekezo ya Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi, hotuba mbalimbali za Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania pamoja na Dira ya Taifa vyote vimetoa kipaumbele cha juu katika suala la kukuza uchumi na kuondoa umaskini nchini. Hivyo, diplomasia yetu kwa mwaka wa fedha ujao, pamoja

na mambo mengine itajielekeza zaidi katika kutekeleza mambo yafuatayo:-

(i) Kuitangaza nchi yetu kama moja ya nchi duniani zenye mazingira mazuri kwa ajili ya uwekezaji kutokana na historia yake ya miaka mingi ya amani, umoja, utulivu na mshikamano wa kitaifa;

(ii) Kuendelea kufuatilia utekelezaji wa ahadi mbalimbali zilizotolewa kwa nchi yetu na nchi wahisani, mashirika ya kikanda na ya kimataifa katika kusaidia utekelezaji wa mipango yetu ya maendeleo;

(iii) Kuendelea kuratibu Wizara, Idara na Taasisi nyingine za Serikali katika kuvutia wawekezaji na watalii, kutafuta nafasi za masomo, ajira na nafasi za kubadilishana uzoefu na kutafuta masoko;

(iv) Kusimamia, kufuatilia na kuratibu utekelezaji wa mikataba mbalimbali iliyosainiwa kati ya nchi yetu na nchi nyingine na ile ya mashirika ya kikanda na kimataifa;

(v) Kufuatilia utekelezaji wa maelekezo ya viongozi mbalimbali wa kitaifa;

(vi) Kuendelea kusimamia balozi zetu katika kutekeleza majukumu ya uratibu hasa kutafuta wawekezaji, fursa za ajira, nafasi za masomo na masoko kwa bidhaa zetu;

(vii) Kuendelea kufuatilia kwa karibu sana mageuzi kwenye taasisi za Umoja wa Mataifa kama vile Baraza la Kiuchumi na Kijamii (ECOSOC); Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa (UNGA); kuanzishwa kwa Malengo Endelevu ya Maendeleo (*Sustainable Development Goals* – SDGs) na agenda ya maendeleo baada ya kumalizika kwa kipindi cha Malengo ya Milenia 2015. Tutaendelea kufuatilia kwa karibu masuala yote yanayogusa maslahi yetu kama Ujenzi wa Kituo cha Kumbukumbu ya Mauaji ya Kimbari ya Rwanda kitakachojengwa Arusha;

(viii) Kuongeza uwakilishi wetu nje kwa kufungua Balozi mpya na Balozi ndogo na kuendelea kununua, kujenga na kukarabati majengo kwa ajili ya makazi na ofisi za Balozi kwa kadri hali ya fedha itakavyoruhusu;

(ix) Kuendeleza ujirani mwema;

(x) Kujenga mahusiano ya kirafiki na ushirikiano wa kiuchumi kati ya vyombo mbalimbali vya Kikanda na Kimataifa, unaozingatia maslahi ya Taifa letu;

(xi) Kuendelea kutetea na kusimamia maslahi ya nchi maskini kwenye mikutano yote mikubwa na hasa ile ya Umoja wa Mataifa na taasisi zake. Vilevile, tutaendelea kufanya mazungumzo na nchi tajiri duniani ili kuhakikisha zinatekeleza ahadi mbalimbali zilizotoa ili kuharakisha maendeleo ya nchi maskini. Kwa mfano, ahadi za G8 na ile ahadi ya kila nchi tajiri kutoa asilimia 0.7 ya pato lake la Taifa kwa nchi maskini kama msaada; na mwisho lakini siyo kwa umuhimu; na

(xii) Kukamilisha mchakato wa kuitambua jumuiya ya watanzania wanaoishi ughaibuni na kuweka utaratibu utakaowawezesha kuchangia maendeleo ya taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka wa fedha 2013/2014. Ili kuweza kutekeleza kikamilifu kazi zilizotajwa hapo juu, Wizara yangu imepangiwa kiasi cha shilingi bilioni mia moja na thelathini na nane, milioni mia tatu hamsini na tisa, mia tisa arobaini na nne elfu na mia mbili ishirini na moja (138,359,944,221.00) kwa mwaka wa fedha 2013/2014. Kati ya fedha hizo, shilingi bilioni mia moja na kumi, milioni mia tatu hamsini na tisa, mia tisa arobaini na nne elfu na mia mbili ishirini na moja (110,359,944,221.00) ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na shilingi bilioni ishirini na nane (28,000,000,000.00) ni kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo. Aidha, katika bajeti ya Matumizi ya Kawaida, shilingi bilioni mia moja na nne, milioni mia tisa na sita, mia mbili themanini na nne elfu na mia saba kumi na tisa (104,906,284,719.00) ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo

na shilingi bilioni tano, milioni mia nne hamsini na tatu, mia sita hamsini na tisa elfu na mia tano na mbili (5,453,659,502.00) ni kwa ajili ya Mishahara.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika bajeti ya Matumizi Mengineyo, shilingi bilioni moja na milioni mia sita sitini na tano (1,665,000,000.00) ni kwa ajili ya Mpango wa Kujitathmini kwa Utawala Bora Tanzania *(APRM);* shilingi bilioni moja, milioni mia tano na nne, mia tano sabini na nne elfu na mia nne sabini na nane (1,504,574,478.00) ni kwa ajili ya Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu na shilingi bilioni tatu, milioni mia saba sabini na tatu, mia moja na nane elfu na mia nne sitini na mbili (3,773,108,462.00) ni kwa ajili ya fedha za mishahara na Matumizi Mengineyo ya Chuo cha Diplomasia.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara yangu, kupitia Balozi zake, inatarajia kukusanya kiasi cha shilingi bilioni kumi na sita, milioni mia tisa sitini na sita, mia saba ishirini na tisa elfu na mia tatu (16,966,729,300.00) kama maduhuli ya Serikali. Kwa maana ya utekelezaji wa bajeti, kiasi hiki cha maduhuli tayari kimejumuishwa kama sehemu ya bajeti ya Matumizi Mengineyo ya Wizara.

Mheshimiwa Naibu Spika, hitimisho. Ili Wizara yangu iweze kutekeleza malengo yake iliyojiwekea kwa mwaka wa fedha 2013/2014, naomba Bunge lako Tukufu liidhinishe jumla ya shilingi bilioni mia moja na thelathini na nane, milioni mia tatu hamsini na tisa, mia tisa arobaini na nne elfu na mia mbili ishirini na moja (138,359,944,221.00). Kati ya fedha hizo shilingi bilioni mia moja na nne, milioni mia tisa na sita, mia mbili themanini na nne elfu na mia saba kumi na tisa (104,906,284,719.00) ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo, shilingi bilioni tano, milioni mia nne hamsini na tatu, mia sita hamsini na tisa elfu na mia tano na mbili (5,453,659,502.00) ni kwa ajili ya mishahara na shillingi bilioni ishirini na nane (28,000,000,000.00) ni kwa ajili ya miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa, tunakushukuru sana kwa hotuba yako na imeungwa mkono. Nikujulishe tu kwamba hotuba hii imesikilizwa vilevile na vijana wanaochipukia katika kusomea masuala ya uhusiano wa kimataifa kutoka Chuo Kikuu cha *UDOM*, naomba wasimame na nitawaomba Makatibu wangu wakati wanaondoka mtawapatia kitabu cha Mheshimiwa Waziri waone namna gani masuala ya mahusiano ya kimataifa yamewekwa katika hotuba ya leo. *(Makofi)*

Basi baada ya hapo, naomba nimwite mwanafunzi mwingine wa *UDOM* ambaye anasomea masuala ya uhusiano wa kimataifa, Mheshimiwa Juma Nkamia, aje asome taarifa kwa niaba ya Kamati. Mheshimiwa Juma Nkamia. *(Makofi)*

**MHE. JUMA S. NKAMIA (K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA):** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mwenyekiti wa Kamati ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa, Mheshimiwa Edward Lowassa na kwa mujibu wa Kanuni ya 99(9) na 117(11) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la 2013, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa kuhusu Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa kwa mwaka wa fedha 2012/2013; pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hii kwa mwaka wa fedha 2013/2014 na kuliomba Bunge lako Tukufu liipokee taarifa hii na kuikubali, kisha kuidhinisha Bajeti ya Wizara hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote naomba kulijulisha Bunge lako Tukufu kuwa utaratibu huu mpya wa namna ya kuchambua taarifa za Serikali na Mapendekezo

ya Bajeti za Wizara umeiwezesha Kamati kufuatilia kwa undani zaidi utekelezaji wa shughuli za Serikali. Ili kujiridhisha kuhusu utekelezaji wa mpango wa bajeti ya mwaka 2012/2013, baadhi ya mambo ya msingi yaliyozingatiwa na Kamati ni kama ifuatavyo:-

(i) Uhusiano baina ya utekelezaji wa majukumu ya Wizara na mipango iliyopangwa kwa mwaka wa fedha 2012/2013;

(ii) Uhusiano baina ya dhima na dhamira na namna malengo yalivyotekelezwa;

(iii) Uhusiano baina ya fedha zilizotengwa kwa mipango ya Wizara na fedha zilizopatikana kutoka Hazina;

(iv) Uhusiano uliopo kati ya fedha zilizopatikana na malengo yaliyotekelezwa;

(v) Uwiano wa fedha zilizotumika ikilinganishwa na fedha zilizopatikana na kubaki hadi mwezi Machi, 2013; na

(vi) Azma ya Serikali katika eneo la utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa ujumla Kamati ilitafakari kuhusu uhusiano baina ya mipango kwa maana ya fedha na malengo na utekelezaji kwa maana ya shughuli zilizotekelezwa ikilinganishwa na fedha zilizopatikana na kutumika. Lengo kubwa la kufanya hivyo, ni kuliwezesha Bunge lako Tukufu kufuatilia kwa karibu zaidi utekelezaji wa shughuli za Serikali kama ilivyoainishwa katika Ibara ya 63(3)(b) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977.

Mheshimiwa Naibu Spika, zipo namna nyingi za Bunge kufuatilia utekelezaji wa shughuli za Serikali kwa lengo la kukidhi matarajio ya wananchi. Moja ya njia hizo, ni kupitia

Kamati zake za kudumu zilizoanzishwa chini ya Kanuni ya 118 ikisomwa pamoja na Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Aprili, 2013. Katika kufuatilia utekelezaji wa shughuli za Wizara hii, Kamati hii imepewa pamoja na majukumu mengine, jukumu la kuisimamia Wizara hii. Naomba kulihakikishia Bunge lako Tukufu kuwa Kamati imeanza kutekeleza wajibu huu mara tu baada ya kuteuliwa kwa Wajumbe wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la kwanza katika kufuatilia lilihusu wajibu wa Wizara kuhusu Ushirikiano na uhusiano wa Kimataifa na Diplomasia ya Uchumi kwa mwaka wa Fedha 2012/2013. Miongoni mwa mambo ya msingi katika dhamira ya Wizara hii ni dhima yake katika diplomasia inayopaswa kuchangia kwenye shughuli za kiuchumi. Kwa msingi huo, Kamati ilitaka kujiridhisha kuhusu jinsi diplomasia inavyotumika kuchangia maendeleo ya Uchumi wetu. Kutokana na taarifa zilizowasilishwa, Kamati ilibaini mambo makuu yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na umuhimu mkubwa wa dhana ya diplomasia ya uchumi kwa maendeleo ya taifa, bado kuna dosari za kimkakati na kiutendaji zinazopaswa kurekebishwa. Kwa mfano, ili kutumia vema fursa zilizopo katika uhusiano wa kimataifa hususan kwenye nyanja za uchumi na biashara, Ofisi za Balozi zetu duniani zinapaswa kuwa na Waambata Biashara (*Commercial Attaché*).

Mheshimiwa Naibu Spika, umuhimu wake unatokana na ukweli kuwa diplomasia ya Biashara (*Commercial Diplomacy*) haiwezi kufanikiwa kwa kuwatumia wanadiplomasia ya uhusiano wa kimataifa pekee. Kama ilivyosemwa katika Tasinifu iitwayo "*Commercial Diplomacy and the role of Embassies*"

*"Business support is not a job for traditional diplomats; rather, the job finds its roots and challenges in marketing, financial techniques which are in general not expected from traditional career diplomats.* Mwisho wa kunukuu. (Tazama

ukurasa wa 17 wa Tasinifu ya Shahada ya Pili, iliyosimamiwa na Dkt. H.J.M. Ruel wa Chuo Kikuu cha Twente.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa Kwa tafsiri isiyo rasmi, "Uwezeshaji katika biashara si kazi ya Wanadiplomasia wanaofuata mrengo wa kale, bali ni kazi inayotokana; na yenye changamoto katika utafutaji wa masoko, maarifa kuhusu masoko, mbinu za kibiashara na kifedha ambazo kwa ujumla hazitarajiwi kutekelezwa kwa ufanisi na Wanadiplomasia wa mrengo wa kale *(Traditional Diplomats)".*

Mheshimiwa Naibu Spika, utekelezaji wa malengo ya bajeti kwa mwaka wa fedha 2012/2013. Utekelezaji wa malengo ya Wizara, baada ya Bunge kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hii, Jukumu la kufuatilia liliendelea kuwa muhimu ili kutumia madaraka ya Bunge yaliyoelezwa katika Ibara ya 63(3) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kwa kutumia uwezo wake chini ya Ibara ya 96(1) na (2) Bunge limekasimu jukumu hilo kwa Kamati hii. Katika utekelezaji wa majukumu yake, tarehe 19 Machi, 2013 Kamati ilipokea na kujadili taarifa ya utekelezaji wa majukumu ya Wizara hii kwa mwaka wa fedha 2012/ 2013.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika taarifa hiyo, Kamati ilielezwa kuhusu makisio na makusanyo ya maduhuli, kiasi cha fedha zilizopokelewa kutoka Hazina na majukumu yaliyotekelezwa kwa mwaka wa fedha 2012/2013. Kutokana na Taarifa hiyo, yapo mambo yaliyojitokeza katika maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Mpango wa nchi za Afrika Kujitathmini zenyewe katika vigezo vya Utawala Bora *(APRM),* kwa upande wa shughuli za Mpango wa nchi za Afrika kujitathmini zenyewe katika vigezo vya Utawala Bora *(APRM),* Kamati ilibaini kuwa Ufinyu wa Bajeti kwa ajili ya masuala ya APRM Tanzania umeendelea kuwa changamoto kwa shughuli zilizopangwa kutekelezwa kwa kipindi cha Julai, 2012 hadi Juni, 2013.

Mheshimiwa Naibu Spika, chanzo kikubwa cha changamoto hii ni tofauti kubwa kati ya fedha zilizoombwa na zile zilizotengwa na Wizara kwa mwaka wa fedha 2012/2013. Maombi ya *APRM* yalikuwa Sh.5.194 bilioni, lakini kiasi kilichotengwa ni Sh.1.280 Bilioni sawa na asilimia 54.3 ya maombi. Kwa hali hiyo, shughuli zilizopangwa kutekelezwa kwa mwaka wa fedha 2012/2013, zimeathirika kwa asilimia 45.4. Athari za changamoto hiyo zinajitokeza katika mambo matatu:-

(i) Shughuli nyingi hazikuweza kutekelezwa jambo linalozaa hoja za kiukaguzi *(audit query)* kuhusu malengo ya kuundwa kwa taasisi hii;

(ii) Kusuasua kwa utekelezaji wa mkakati wa uhamasishaji wa umma (*Communication Strategy*). Hali hii imeathiri dhana nzima ya miongozo ya *APRM* inayotaka Mchakato huu utangazwe nchini na kuiwezesha Serikali kupata mrejesho wa haraka, kuhusu utekelezaji wa Sera, Sheria, mipango na mikakati yake; na

(iii) Kuahirishwa kwa mikutano mingi kwa ajili ya maoni ya Wadau wa masuala ya *APRM*, jambo lililoathiri malengo ya kuanzishwa kwa Taasisi hii na tija iliyotarajiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ushirikishwaji wa Diaspora katika maendeleo ya Taifa. Kwa kuwa raia wa nchi zinazoendelea waishio ughaibuni wameridhika kuwa sehemu ya wabia wa Maendeleo pale walipoandaliwa mazingira wezeshi, Sera ya Mambo ya Nje inaonekana kuzingatia hilo. Wasiwasi uliopo ni kuhusu utaratibu wa mawasiliano baina ya Wizara na taasisi za ndani na Balozi zetu nje ya nchi. Ili kufanikisha ushirikishwaji wa Watanzania waishio ughaibuni katika maendeleo, mawasiliano ni suala linalohitaji kuboreshwa zaidi. Hata hivyo, taarifa ya ziara ya ufuatiliaji iliyofanywa na Kamati ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama wakati huo, ilibainisha kuwepo kwa tatizo la kusuasua kwa mawasiliano na Balozi zetu nje ya nchi. Hatua zilizotarajiwa kuchukuliwa na Wizara kuboresha hali hiyo bado hazikuwa na tija.

Mheshimiwa Spika, kupitia mikutano ya Diaspora *(Diaspora Conferences and Conventions*) jamii ya Diaspora inapata fursa ya kufahamu mabadiliko ya kisera, kiuchumi na kijamii. Taarifa ya Wizara ilionesha kuwa katika Mkutano uliofanyika Edmonton, Canada na Muscat Oman, Oktoba, 2012, Mheshimiwa Rais alitumia fursa hiyo kuwahakikishia Diaspora kuwa nchi inawathamini katika kuchangia maendeleo ya Taifa. Kamati inampongeza Rais Kikwete kwa juhudi zake za kuwashawishi na kuwahimiza kuwekeza nyumbani kadiri ya uwezo wao unavyoruhusu.

Mheshimiwa Naibu Spika, diplomasia ya uchumi. Pamoja na Sera ya Tanzania kuhusu Mambo ya Nje *(Foreign Policy)* kuweka mkazo katika diplomasia ya uchumi *(Economic Diplomacy),* utekelezaji wa dhana ya diplomasia hiyo haukuridhisha. Kamati ilipotaka kujua undani kuhusu kuzorota kwa utekelezaji wa Diplomasia ya uchumi, sababu iliyoelezwa ilikuwa ni ufinyu wa Bajeti.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu hatua zilizochukuliwa na Wizara kuboresha hali hiyo, Kamati ilijulishwa kuwa Wizara imewasilisha ombi maalum Hazina ili kupatiwa fedha ya Nyongeza ya Bajeti kwa mwaka 2012/ 2013. Maelezo yaliyotolewa yalibainisha kuwa fedha hizo ni kwa ajili ya kugharamia mahitaji muhimu ya kimkataba yaliyopo Balozini. Kamati ilibaini kuwa maombi hayo mapya hayakulenga chochote kuhusu kujiweka sawa na kutumia fursa zilizopo kwa namna ya diplomasia ya uchumi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ushirikiano wa Kikanda. Kwa kuzingatia majukumu na dhima ya Wizara hii katika masula ya ushirikiano wa kikanda, Kamati ilitaka kujua utekelezaji wa shughuli za Serikali kuhusu ushirikiano huo. Taarifa zilionesha kuwa kutokana na kazi nzuri iliyofanywa na Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, nchi yetu imepata heshima kubwa ndani ya *SADC* na Ukanda wa wa Maziwa Makuu *(ICGLR).* Kwa mfano, kuhusu hali ya kisiasa nchini Mdagascar na mgogoro wa Mashariki mwa Kongo, Rais Kikwete amefanya kazi nzuri inayothaminiwa Kimataifa. Kamati inampogeza

kwa kazi yake inayoiletea nchi yetu heshima kubwa ndani na nje ya nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Bunge lako Tukufu kwa upande wake, limeendelea kuhakikisha uwepo wa amani, usalama na demokrasia kwa nchi wanachama wa *SADC* kupitia Jukwaa la Mabunge ya Jumuiya ya Maendeleo ya Kusini mwa Afrika *(SADC - PF)* lililoanzishwa mwaka 1997 Jijini Blantyre, Malawi. Kamati imeendelea kufuatilia taarifa za Wawakilishi wetu kwenye *SADC - PF* ambapo suala la fursa sawa ya uwakilishi kwa wanawake na vyama vya siasa vyenye Wabunge limeendelea kuwa kigezo muhimu. Kamati inasisitiza kuwa Serikali liendelee kutoa ushirikiano kwa wawakilishi wetu ili kuwawezesha kuuwakilisha vema mhimili wa Bunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, Bunge kwa kuthamini umuhimu wa Umoja wa Afrika, limechagua wawakilishi wanaohudhuria Bunge la Afrika ambapo moja ya madhumuni yake ni kukuza amani, usalama na utulivu ndani ya Bara la Afrika. Taarifa zinazopatikana kupitia wawakilishi wetu kwenye Bunge hilo zinaonyesha jinsi Tanzania inavyothamini Umoja huu. Kamati ina maoni kuwa uwakilishi huu wa Wabunge utafanyika vizuri zaidi iwapo Wizara itakuwa na utaratibu bora wa kutoa taarifa za mara kwa mara kuhusu utekelezaji wa uamuzi unaofikiwa katika vikao vya Umoja wa Afrika.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kituo cha Mikutano ya Kimataifa Arusha (AICC). Kama ambavyo wengi wetu tunavyofahamu, Tanzania ni nchi maarufu duniani kwa kuenzi amani, usalama na utengamano, jambo ambalo ni mtaji na kivutio kikubwa kwa upande wa Sekta ya utalii wa mikutano. Hata hivyo, kwa kipindi cha mwaka 2012/2013, changamoto mbalimbali zilijitokeza. Miongoni mwa changamoto hizo ni suala la ukosefu wa eneo la kutosha kwa ajili ya maonyesho *(Convention and Exhibition Centre).*

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, licha ya kuwa rasilimali nyingi za Kituo cha Mikutano ya Kimataifa Arusha

*(AICC)* ziko katika maeneo nyeti ya Jiji la Arusha, hakuna juhudi za kutosha zilizofanyika kuendeleza rasilimali hizo ili kukidhi mahitaji ya sasa na ya baadaye. Kamati ilipohoji zaidi, ilijulishwa kuwa *AICC* imeanza kukabiliana na changamoto hiyo kwa kutekeleza miradi iliyoainishwa katika Mpango Mkakati wa Miaka Mitano ikiwa ni pamoja na kujenga vitega uchumi katika maeneo ya Kaloleni, *Fire* na *Corridor Area*.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kuliwezesha taifa kutumia hali yake ya usalama, amani na utengamano, *AICC* imependekeza na kukubaliwa wazo la kuwa na Kituo cha kisasa cha Kimataifa cha Mikutano *(Mount Kilimanjaro International Covention Centre Mk-ICC)* kitakachokuwa na eneo la kutosha kwa ajili ya *"Convention and Exhibition Centre).* Kamati imeridhishwa na mapendekezo hayo na kwamba yakitekelezwa ipasavyo, yataiwezesha nchi kutumia nafasi na umaarufu wake kuchangia kukua kwa uchumi wa Taifa kupitia Sekta ya Utalii wa mikutano.

Mheshimiwa Naibu Spika, upatikanaji wa fedha kutoka Hazina. Kama tunavyofahamu, kuidhinisha bajeti ya Wizara ni jambo moja na upatikanaji wa fedha ni jambo lingine. Kwa sababu hiyo, Kamati ilitaka kujua mwenendo wa upatikanaji wa fedha kutoka Hazina na matumizi yake. Taarifa zilionyesha kuwa hadi kufikia tarehe 28 Februari, 2013, Fungu 34 lilipokea jumla ya Sh. 83,615,867,746/- ambazo ni sawa na asilimia 85 ya fedha iliyoidhinishwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ilipopitia na kuchambua takwimu za upatikani wa fedha ilibaini kuwa Kifungu *(Subvote)* 1010 kiliongoza kwa kupokea asilimia kubwa ya fedha zilizoidhinishwa kikifuatiwa na Kifungu 1008. Tafsiri ya mtiririko huo ni kuwa shughuli zilizotekelezwa kwa kiasi kikubwa zilihusiana na masuala ya itifaki pamoja na shughuli za Idara ya Afrika. Ili kujiridhisha, Kamati ilihoji takwimu hizo na kubaini kuwa hali hiyo ilitokana na namna fedha zilivyopatikana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu upatikanaji wa

fedha zilizoidhinishwa na Bunge kwa Balozi zetu zenye jumla ya vifungu thelathini na mbili, (kuanzia Kifungu 2001 cha ubalozi wa Adis Ababa hadi Kifungu 2032 cha Ubalozi uliopo Kuala Lumpur), Kamati ilibaini kuwa jumla ya fedha zilizopokelewa kutoka Hazina hadi Februari, 2013 ni Sh.23, 532, 861,790 sawa na asilimia 55 ya fedha iliyoidhinishwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa takwimu hizo, ni dhahiri kuwa wakati kipindi cha bajeti kikielekea robo ya tatu, asilimia 45 ya fedha iliyoidhinishwa ilikuwa haijapatikana jambo ambalo ni shida kwa watumishi walio katika Balozi zetu nje ya nje.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, Balozi zote kwa ujumla zilikusanya jumla ya Sh.12,179,297,099.85 sawa na asilimia 34 ya fedha zilizotumika Balozini. Takwimu hizi zinadhihirisha kuwa Hazina ilipeleka asilimia 66 ya fedha zilizotumika hadi tarehe 28 Februari, 2013.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kutekeleza vema jukumu la Kamati kwa niaba ya Bunge, mchanganuo wa jumla ya Sh. 15,878,527,320.00 zilizopokelewa kutoka Hazina ulifuatiliwa. Awali, Randama ya Wizara hii haikufafanua matumizi ya fedha kwa kila kifungu na Kasma zake, jambo liliosababisha Kamati kuhoji na kutaka randama ya maelezo ya kina. Baadaye Wizara iliwasilisha randama nyingine yenye ufafanuzi zaidi kwa kila Kifungu na Kasma kama ilivyoagizwa na Kamati.

Mheshimiwa Naibu Spika, utekelezaji wa maoni na ushauri, wakati wa kupitia na kuchambua Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hii kwa mwaka wa Fedha 2012/2013, iliyokuwa Kamati ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama ilipendekeza Bungeni jumla ya mambo kumi na moja. Kwa kuwa ushauri huo ulitarajiwa kuanza kutekelezwa katika mwaka wa fedha 2012/2013, Kamati hii ilitaka kujua namna Wizara ilivyofanyia kazi maoni na ushauri huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa zilizotolewa kwenye kikao cha Kamati tarehe 3 Aprili, 2013 zilionyesha kuwa Wizara

inaendelea na utekelezaji wa ushauri huo na kwamba pamoja na kuthamini ushauri uliotolewa, changamoto kubwa ni ufinyu wa bajeti. Licha ya kukubali manufaa ya kutekeleza ushauri uliotolewa Bungeni mwaka jana, mambo mengi hayakufanyiwa kazi kabisa. Kwa mfano, Kamati ilishauri kuhusu kufanyika kwa mikutano ya Mabalozi ili kufanya tathmini na kuboresha masuala mbalimbali ya utekelezaji Balozini. Taarifa ya Wizara ilionyesha kuwa kwa mara ya mwisho Mkutano wa Mabalozi Tanzania ulifanyika Zanzibar, mwaka 2008. Ni takriban miaka mitano sasa mikutano hiyo haijafanyika, jambo ambalo si jema katika azma ya kufaidika na dhana ya Diplomasia ya uchumi na utekelezaji bora wa Sera ya Mambo ya Nje.

Mheshimiwa Naibu Spika, mfano mwingine wa ushauri uliotolewa ni kuhusu kuanzisha chombo maalumu kitakachoshughulikia uamuzi wa kukarabati na kununua majengo kwa ajili ya Balozi zetu nje ya nchi. Wizara ilieleza kuwa Serikali haijakamilisha mchakato wa kuunda chombo hicho licha ya umuhimu wake. Ni maoni ya Kamati kuwa kasi ya utekelezaji wa jambo lolote lenye manufaa inapaswa kuongezwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa tathmini na uhakiki wa Watumishi Balozini kama ilivyokuwa imeshauriwa, Kamati ilielezwa kuwa ni Watumishi wachache tu waliomaliza muda wao na kustaafu, waliweza kurejeshwa nyumbani. Aidha, Mheshimiwa Waziri alieleza kuwa ufinyu wa bajeti umesababisha Wizara kushindwa kupeleka Watumishi kwa ajili ya kuziba mapengo ya lazima. Hali hii inahitaji kupatiwa ufumbuzi unaolingana na umuhimu wa majukumu ya Balozi zetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu kasoro ya Hati za Utambulisho na Hati za Wito, Kamati iliishauri Wizara kuhakikisha kuwa Kasoro zote kwenye Hati za Wito na Hati za Utambulisho zinarekebishwa. Maelezo yaliyotolewa na Wizara yanaonyesha kuwa bado tatizo la Hati za Utambulisho kutowasilishwa linaendelea. Tazama Jedwali linalooonesha Balozi za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Taarifa za Uwakilishi na uwasilishaji wa Hati za Utambulisho.

**KIAMBATISHO CHA TAARIFA**

**BALOZI ZA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA NA TAARIFA ZA UWAKILISHI NA UWASILISHWAJI WA HATI ZA UTAMBULISHO HADI TAREHE 28 MACHI, 2013**

| SN | UBALOZI | ENEO LA UWAKILISHI | HATI ZILIZOWASILISHWA | HATI AMBAZO HAZIJAWASILISHWA |
|---|---|---|---|---|
| 1. | ABUJA, NIGERIA | NIGERIA, BENINI, TOGO, COTE D'IVOIRE, GHANA, GUINEA, SENEGAL, BURKINA FASO, MALI, SIERRA LEONE, LIBERIA, GUINEA BISSAU, MAURITANIA, ADB NA ECOWAS | HAKUNA | NIGERIA, BENINI, TOGO, COTE D'IVOIRE, GHANA, GUINEA, SENEGAL, BURKINA FASO, MALI, SIERRA LEONE, LIBERIA, GUINEA BISSAU, MAURITANIA, ADB NA ECOWAS (HATUNA BALOZI KWA SASA) |
| 2. | ABUDHABI, UAE | UAE, PAKISTRAN, IRAN NA BAHRAIN | UAE, PAKISTRAN, URAN NA BAHRAIN | HAKUNA |

1

| SN | UBALOZI | ENEO LA UWAKILISHI | HATI ZILIZOWASILISHWA | HATI AMBAZO HAZIJAWASILISHWA |
|---|---|---|---|---|
| 3. | ADDIS ABABA, ETHIOPIA | ETHIOPIA, DJIBOUT, YEMEN, UMOJA WA AFRIKA, ECA | ETHIOPIA, UMOJA WA AFRIKA, ECA | DJIBOUTI NA YEMEN |
| 4. | BEIJING, CHINA | CHINA, VIETNAM, MONGOLIA, THAILAND NA DPRK | CHINA, VIETNAM, NA DPRK | MONGOLIA NA THAILAND |
| 5. | BEIJING, UJERUMANI | UJERUMANI, USWISSI, JAMHURI YA CZECH, SLOVAKIA, POLAND, HUNGARY, BULGARIA, ROMANIA, AUSTRARIA NA VATICAN | UJERUMANI, USWISSI, AUSTRIA NA VATICAN | JAMHURI YA CZECH, SLOVAKIA, HOLAND, HUNGARY, BULGARIA NA ROMANIA |
| 6. | BUJUMBURA, BURUNDI | BURUNDI | BURUNDI | HAKUNA |
| 7. | CAIRO, MISIRI | MISRI, ISRAEL, , LEBANON, PALESTINA, LIBYA, IRAQ, | MISRI | ISRAEL, LEBANON, PALESTINA, LIBYA, |

| SN | UBALOZI | ENEO LA UWAKILISHI | HATI ZILIZOWASILISHWA | HATI AMBAZO HAZIJAWASILISHWA |
|---|---|---|---|---|
| | | SYRIA NA JORDAN | | IRAQ, SYRIA NA JORDAN |
| 8. | GENEVA, USWISSI | OFISI ZA UN GENEVA NA VIENNA | OFISI ZA UN GENEVA NA VIENNA | HAKUNA |
| 9. | HARARE, ZIMBABWE | ZIMBABWE NA MAURITIUS | ZIMBABWE NA MAURITIUS | HAKUNA |
| 10. | KAMPALA, UGANDA | UGANDA | UGANDA | HAKUNA |
| 11. | KIGALI, RWANDA | RWANDA | RWANDA | HAKUNA |
| 12. | KINSHASA, DRC | DRC, GABON, CENTRAL AFRICAN REPUBLIC, CAMEROON NA CONGO BRAZAVILLE | HAKUNA | DRC, GABON, CENTRAL AFRICAN REPUBLIC, CAMEROON NA CONGO BRAZAVILLE (HATUNA BALOZI KWA SASA) |

| SN | UBALOZI | ENEO LA UWAKILISHI | HATI ZILIZOWASILISHWA | HATI AMBAZO HAZIJAWASILISHWA |
|---|---|---|---|---|
| 13. | LILONGWE, MALAWI | MALAWI | MALAWI | HAKUNA |
| 14. | LONDON, UINGEREZA | UINGEREZA, IRELAND NA COMMONWEATH | COMMONWEATH | HAKUNA |
| 15. | LUSAKA, ZAMBIA | ZAMBIA, ANGOLA, SAOTOME NAPRINCIPE | ZAMBIA, ANGOLA | SAOTOME NA PRINCIPE |
| 16. | MAPUTO, MSUMBIJI | MSUMBIJI, SWAZILAND, MADAGASCAR, NA COMOROS | COMOROS | MADAGASCAR |
| 17. | MOSCOW, URUSI | RUSSIA, BELARUS, GEORGIA, UKRAINE NA NCHI NYINGINE ZA CIS | UKRAINE | NCHI NYINGINE ZA CIS |
| 18. | MUSCAT, OMAN | OMAN | OMAN | HAKUNA |
| 19. | NAIROBI, KENYA | KENYA, SUDAN, SEYCHELLES, SOMALIA, ERITREA, UNEP NA HABITAT | KENYA, UNEP NA HABITAT | SUDAN, SEYCHELLES, SOMALIA NA |

| SN | UBALOZI | ENEO LA UWAKILISHI | HATI ZILIZOWASILISHWA | HATI AMBAZO HAZIJAWASILISHWA |
|---|---|---|---|---|
| | | | | ERITREA |
| 20. | NEW DELHI, INDIA | NEPAL NA BANGLADESH | BANGLADESH | SRI LANKA NA NEPAL |
| 21. | NEW YORK, UN | OFISI ZA UMOJA WA MATAIFA | OFISI ZA UMOJA WA MATAIFA | HAKUNA |
| 22. | OTTAWA, CANADA | CANADA, CUBA, ICAO | CANADA, CUBA, ICAO | HAKUNA |
| 23. | PARIS, UFARANSA | UFARANSA, HISPANIA,PORTUGAL, ALGERIA, MOROCCO, SAHARA WI TUNISIA NA UNESCO | MOROCCO, SAHARA WI NA UNESCO | ALGERIA NAI TUNISIA |
| 24. | PRETORIA, AFRIKA KUSINI | AFRIKA KUSINI, NAMIBIA, LESOTHO, BOTSWANA NA SADC | AFRIKA KUSINI, NAMIBIA, LESOTHO, BOTSWANA NA SADC | HAKUNA |
| 25. | RIYADH, SAUDI ARABIA | SAUDI ARABIA, QATAR NA KUWAIT | SAUDI ARABIA, QATAR NA KUWAIT | HAKUNA |

| SN | UBALOZI | ENEO LA UWAKILISHI | HATI ZILIZOWASILISHWA | HATI AMBAZO HAZIJAWASILISHWA |
|---|---|---|---|---|
| 26. | ROMA, ITALIA | ITALY, CROATIA, GREECE, MACEDONIA, SLOVENIA, ALBANIA, BOSNIA-HERZEGOVINA, SERBIA, MONTTENEGRO,TURKEY, MAITA, FAO, IFAD NA WFP | ITALY, GREECE, TURKEY, FAO, IFAD NA WFP | ICROATIA, MACEDONIA, SLOVENIA, ALBANIA, BOSNIA-HERZEGOVINA, SERBIA, MONTTENEGRO NA MALTA |
| 27. | STOCKHOLM, SWEDEN | SWEDEN, DENMARK, FINLAND, NORWAY, ICELAND, ESTONIAL, LATVIA NA LITHUANIA | SWEDEN, DENMARK, NORWAY, ICELAND, | FINLAND, ICELAND, ESTONIAL, LATVIA NA LITHUANIA |
| 28. | TOKYO, JAPAN | JAPAN, SOUTH KOREA, AUSTRALIA, NEW ZEALAND, PAPUA NEW GUINEA | JAPAN, SOUTH KOREA, AUSTRALIA | NEW ZEALAND NA PAPUA NEW GUINEA |

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa ujumla, kuhusu utekelezaji wa ushauri Kamati ina maoni kuwa si jambo jema kwa Wizara kutofanyia kazi ipasavyo, ushauri mzuri unaotolewa na Bunge lako Tukufu. Haipendezi kurudia ushauri wa jambo moja kila mwaka wa fedha pasipo kutekelezwa ipasavyo. Kwa mfano, ni muda mrefu sasa Wizara imekuwa ikishauriwa kuhusu utaratibu wa ujenzi wa majengo yetu kwa ajili ya Balozi zetu nje ya nchi kwa utaratibu wa "*Mortagage financing*" na Wizara haionekani kuchukua hatua yoyote inayofaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, mpango na makadirio ya mapato ya matumizi kwa mwaka 2013/2014. Malengo makuu. Katika Kikao chake na Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa, kilichofanyika 3 Aprili, 2013, Kamati ilielezwa malengo makuu kumi yaliyopangwa kulingana na majukumu ya msingi ya Wizara hii. Kati ya hayo, lengo mojawapo ni kukamilisha mchakato wa kuitambua Jumuiya ya Watanzania wanaoishi ughaibuni na kuweka utaratibu utakaowezesha kuchangia maendeleo ya Taifa lao. Kutokana na maelezo ya Wizara, Kamati iliridhika na malengo hayo ingawa mengine yalipangwa kwa mwaka wa fedha 2012/2013 bila kutekelezwa ipasavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, makadirio ya mapato na matumizi, maduhuli. Kamati ilijulishwa kuhusu makadirio ya mapato ya Sh.17,231,232,172.00 kupitia Balozi zetu. Hata hivyo kwa utaratibu wa utekelezaji, kiasi hicho cha maduhuli kimetajwa kuhesabiwa kama sehemu ya Bajeti ya Matumizi ya kawaida katika Fungu 34 la Wizara hii. Kamati ililinganisha makadirio hayo na Maduhuli yaliyopangwa kwa mwaka wa fedha 2012/2013 na kubaini ongezeko la asilimia mbili. Hali hii inawezekana kuwa inatokana na kutoongezeka kwa vyanzo vya mapato kwa kiasi kikubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, matumizi. Katika Randama ya Fungu 34, Bunge linaombwa kuidhinisha jumla ya Sh.138,356,944,221/-. Kiasi hiki kikilinganishwa na makadirio ya mwaka 2012/2013, ni ongezeko la Sh.40,020,237,221 sawa na asilimia 41. Katika ongezeko hilo, bajeti ya maendeleo

imeongezeka kwa asilimia 68 kutoka Sh.16, 653,204,000/- mwaka wa fedha 2012/2013 hadi Sh. 28,000,000,000/-, wakati matumizi ya kawaida yameongezeka kwa asilimia 37. Kwa uchambuzi huo, Wizara inatarajiwa kuongeza juhudi ya kuboresha hali ya Balozi zetu kwa zaidi ya asilimia 40, jambo ambalo Bunge litatakiwa kufuatilia kwa karibu zaidi juu ya utekelezaji wake.


Mheshimiwa Naibu Spika, katika uchambuzi zaidi, Kamati ilibaini kuwa sehemu kubwa ya fedha zinazoombwa kwa ajili ya miradi ya maendeleo, zinalengwa kutumika kwa ajili ya ununuzi wa jengo la Ofisi na makazi ya Balozi jijini Paris Ufaransa. Kiasi kilichotengwa ni Shilingi 24,188,000,000/- ambacho ni sawa na asilimia 86 ya Bajeti yote ya maendeleo kwa Fungu 34. Aidha, Jumla ya ShT. 3,812,009,000/- zinaombwa kwa ajili ya ukarabati wa majengo matatu katika ubalozi wetu Maputo nchini Msumbiji, kiasi ambacho ni asilimia 14 ya Bajeti yote ya miradi ya Maendeleo katika Fungu 34.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na maelezo hayo ya matumizi kwa ajili ya miradi ya maendeleo, ni dhahiri kuwa hali ya majengo ya Balozi zetu nyingi inaachwa kuendelea kuwa mbaya na mengine kiasi cha kuaibisha. Kwa mfano, jengo la Ofisi ya Ubalozi wetu huko Brussels Ubelgiji lililonunuliwa mwaka 2004 kwa gharama ya Euro Milioni moja na nusu, limechakaa na kuvuja kiasi cha kusababisha baadhi ya kuta kutoa harufu mbaya na kuiaibisha nchi yetu Kimaitafa.

Mheshimiwa Naibu Spika, mfano mwingine ni hali ya majengo ya ubalozi wetu uliopo Stockholm – Sweden. Jengo la Afisa ubalozi lipo katika hali mbaya sana kiasi cha kutotumika kwa miaka sita sasa. Hali hii inasababisha Ubalozi wetu kushutumiwa kutokana na nyumba hiyo kupunguza thamani ya eneo husika kwa sababu ya uchakavu wake mkubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kupata picha halisi ya mwenendo wa makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara hii, Kamati ilichambua kwa kina makadirio ya matumizi kwa

ajili ya uendeshaji kwa miaka minane mfululizo, kuanzia mwaka 2006/2007 hadi 2013/2014. Katika uchambuzi huo, Kamati ilibaini kuwa makadirio ya matumizi mengineyo yanaongezeka kila mwaka kama inavyoonekana katika Histogramu ifuatayo:-




**Chanzo:** Uchambuzi wa Kamati kupitia Takwimu zilizowasilishwa na Wizara kwenye Kikao cha Kamati.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati pia ilibaini kuwa Wizara haikulipa kipaumbele suala la Mkutano wa Mabalozi lililopaswa kupangiwa bajeti katika Kifungu cha 1004 kiitwacho "*Policy and Planning*". Kwa kuzingatia umuhimu wa mkutano huo, Kamati ilihoji kiasi cha fedha kinachotakiwa kufanikisha shughuli hiyo kwa mwaka wa fedha 2013/2014 na kuelezwa kuwa zinatakiwa jumla ya shilingi bilioni moja. Kamati iliwasilisha mapendekezo yake kwa Kamati ya Bajeti ambayo pia iliafiki umuhimu wa kiasi hicho kwa shughuli za Mkutano wa Mabalozi.

Mheshimiwa Naibu Spika, maoni na ushauri. Kwa kuzingatia majukumu ya msingi ya Wizara hii pamoja na hali halisi ya kiuchumi, kisiasa na kijamii ndani na nje ya nchi, Kamati ina maoni na ushauri kuhusu eneo la Diplomasia ya Uchumi, huduma za Kikonsuli, uhusiano na ushirikiano, *APRM* Tanzania, *AICC* na Chuo cha Diplomasia kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuzingatia majukumu ya msingi ya Wizara hii pamoja na halisi halisi ya kiuchumi, kisiasa na kijamii ndani na nje ya nchi, Kamati ina maoni na ushauri ufuatao:-

Mheshimiwa Naibu Spika, diplomasia na uchuvi. Dhana ya diplomasia ya uchumi katika Nchi zinazoendelea, (Tanzania ikiwemo), ina misingi na taratibu zake kwa manufaa ya Taifa husika. Katika utafiti uliofanywa na Mchumi aitwae *Kishan Srana – Economic Diplomacy: The Experience of Developing Countries,* yapo mambo ya msingi tunayoweza kuyafanyia kazi. Katika utafiti huo, ilibainika kuwa baadhi ya nchi zinazoendelea zimemudu kuendesha mahusiano yao ya kiuchumi na nchi nyingine duniani kiasi kwamba zinatumia vema fursa za Kiuchumi Kimataifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili nchi yetu iweze kufaidika na dhana hii kuna mambo ya msingi kama alivyobainisha mtaalamu huyu. Mambo hayo ni kama ifuatavyo:-

(i) Mbali ya Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa na Wizara ya Viwanda na Biashara,

wadau wengine ndani na nje ya Serikali wahusishwe ipasavyo katika juhudi za pamoja za kuvuna fursa ya kiuchumi zinazopatikana kwa utekelezaji wa dhana ya diplomasia.

(ii) Kwa kuwa vipaumbele pacha katika utekelezaji wa dhana ya diplomasia ya uchumi ni kukuza na kuinua mauzo ya bidhaa zetu nje ya nchi pamoja na kushawishi uwekezaji wa wageni ndani ya nchi, Kamati inashauri kuwa Serikali iongeze juhudi za kushawishi, kuelimisha na kuwezesha Jumuiya ya Wafanyabiashara nchini kushiriki katika Mikutano ya Kimataifa *(International Trade Fairs).*

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, Balozi zetu ziwezeshwe kwa rasilimali na watumishi ili zimudu kusaidia upatikanaji wa soko kwa ajili ya bidhaa zetu sambamba na kuchangia kuvutia Wawekezaji kuja nchini. Kufanya hivyo ndio wajibu muhimu kwa maelezo ya kitaalamu kama walivyosema Wataalamu wa Diplomasia ya Uchumi, *Berridge, Keens-Soper na Otte,* (2001). Tazama nadharia ya Diploma ya Uchumi katika Kitabu kiitwacho *Diplomatic Theory from Machiavelli to Kissinger, Palgrave, Basing Stoke* cha mwaka 2011. Naomba kununukuu:-

*"A diplomatic service that is well resourced and above all well staffed, gives a state a significant increment of power and influence".*

Kwa tafsiri isiyo rasmi, tunaweza kusema kuwa "huduma ya kidiplomasia yenye rasilimali za kutosha na Watumishi wenye sifa zinazostahili, huliongezea Taifa uwezo na ushawishi katika medani ya Kimataifa".

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa msingi huo, Kamati inashauri kuwa upangaji wa Watumishi na kiasi cha matumizi ya rasilimali katika Balozi zetu viangaliwe na kufanyiwa tathmini ili kubaini kasoro na kuzirekebisha mapema iwezekanavyo. Aidha, ni muhimu muundo wa Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa uboreshwe zaidi na kuwa na Kitengo cha Diplomasia ya Uchumi kitakachokuwa na wataalam wa masuala ya diplomasia

ya biashara na uchumi kwa ujumla.

Mheshimiwa Naibu Spika, Huduma za Kikonseli. Katika eneo hili Kamati inashauri mambo yafuatayo:-

(i) Kwa kuwa mashine ya kutolea viza iliyonunuliwa mwaka 2007 kwa ajili ya kupelekwa *Melbourne – Australia* ambayo bado ipo Ubalozi wa Japan, haijapelekwa kwa sababu ya kukosa fedha za kuisafirisha, Hazina itoe fedha kwa ajili ya kuisafirisha mashine hiyo na kuipeleka inapotakiwa. Aidha, kwa Balozi ambazo hazitumii utaratibu wa kuweka stika kwenye viza (*visa stiker),* wakati umefika kuhakikisha kuwa utaratibu huo unatumika badala ya ugongaji wa mihuri;

(ii) Kuna umuhimu mkubwa kwa Mkaguzi na Mdhibiti wa Hesabu za Serikali kushughulikia suala la ukaguzi kuhusu mapato yanayotokana na makusanyo ya viza katika Balozi za Heshima *(Honorary Consuls)* ili kujiridhisha na usahihi wa hesabu hizo. Msingi wa ushauri huu ni ukweli kuhusu makusanyo makubwa ya visa yanayofanywa na Mabalozi wa Heshima kwa kutoa visa pasipokutumia "*visa stikers*". Pamoja na Balozi hizo kukusanya maduhuli, Kamati haijawahi kupewa taarifa ya makusanyo ya balozi hizo jambo linalozaa wasiwasi kuhusu upotevu wa maduhuli;

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano, uchambuzi rahisi unaotokana na taarifa zilizopo Idara ya Uhamiaji kuhusu ubalozi wa Heshima uliokuwepo Uholanzi kwamba, kwa kuwa watalii zaidi ya elfu hamsini wanapata visa kupitia Uholanzi, kwa hesabu za haraka ni dhahiri kuna uwezekano wa Ubalozi huo kukusanya zaidi ya Dola za Kimarekeni milioni 2.5. Kamati ina maoni kuwa ni jambo la hatari kukosekana kwa takwimu za makusanyo ya maduhuli kupitia Balozi za Heshima. Ni vema Serikali imuelekeze Mdhibiti na Mkaguzi wa Hesabu za Serikali kufanya ukaguzi katika balozi hizo;

(iii) Balozi zetu ziongezewe uwezo wa kibajeti kwa ajili ya kutekeleza vema majukumu yake pamoja na kulipia huduma muhimu kwa wakati. Kwa mfano, hali iliyojitokeza katika Ubalozi uliopo Kuala Lumpur, Malaysia ambapo ubalozi

ulishindwa kulipia ankara za umeme, maji, gesi, simu na matibabu haipendezi hata kidogo. Serikali iweke mkakati madhubuti kwa ajili ya kuzuia kutokea kwa dosari hiyo;

(iv) Ili kuepuka aibu na fedheha inayozuilika, Serikali iongeze juhudi za kuwezesha Balozi zetu kuepuka madeni. Kwa mfano kushindwa kulipa Deni la Kampuni ya Ulinzi katika Ubalozi wetu nchini Malaysia kulikosababisha Ubalozi huo kuandikiwa barua na Wakili wa Kampuni hiyo, ni jambo linalodhalillisha Ubalozi wetu. Mkakati wa Serikali kukabiliana na changamoto za aina hii ni muhimu kwa hadhi na ubora wa huduma mbalimbali Ubalozini;

(v) Kuna haja ya kuboresha utayarishaji wa hati za utambulisho na zoezi zima la utumaji wa hati hizo katika Balozi zetu. Kwa mfano, kama utayarishaji wa hati za utambulisho utaboreshwa ipasavyo, kasoro kama zilizotokea kuhusu uchapaji wa Hati za Utambulisho nchini *Sri-Lanka* na kuchelewa kuandaliwa kwa hati mpya zitapungua;

(vi) Aidha, ucheleweshaji wa Hati za Utambulisho wa Balozi na upungufu katika hati hizo ni mambo yanayopaswa kurekebishwa kadiri inavyobainika. Kufanya hivyo kutazuia changamoto za kiutekelezaji wa majukumu mbalimbali. Kwa mfano, changamoto iliyojitokeza kwa ubalozi uliopo *Stockholm – Sweden* kutokana na kukaa muda mrefu bila kuwasilisha Hati za utambulisho nchini Finland isingejitokeza kama kasi na utaratibu wa kutuma hati hizo vingefanyiwa kazi ipasavyo;

(vii) Mishahara na posho ya huduma nje ya nchi kwa ajili ya Watumishi waliopo katika Balozi mbalimbali itumwe kwa wakati;

(viii) Ili kuepuka Balozi zetu kuingia katika mgogoro kuhusiana na sheria za kazi maeneo ya uwakilishi, utaratibu wa ajira za Watumishi wenyeji (*Local based staffs*) usisigane na matakwa ya Sheria za nchi hizo. Kwa mfano, kama ilivyokuwa kwa Ubalozi uliopo Brussels, Watumishi Wenyeji

wanaofanya kazi katika Ubalozi wetu nchini humo, wanapaswa kuwekwa kwenye utaratibu wa kulipwa mafao jambo ambalo halikuwa limefanyika;

(ix) Malipo ya Posho ya Utumishi Ugenini *(Foreign Service Allowances)* kutengwa kwenye Kasma ya matumizi mengineyo *(Other Charges-OC)* ni jambo linalohitaji kurekebishwa. Utaratibu huu unasababisha Watumishi hao kutopata stahili yao, kwa vile Kasma hiyo mara nyingi hukosa fedha za kutosha. Kamati inashauri kuwa posho hiyo itengwe katika Kasma nyingine kwa Balozi zote;

(x) Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa, ishughulikie ipasavyo tatizo la viwanja vya serikali nje ya nchi vilivyonunuliwa kwa muda mrefu bila kuendelezwa. Kwa mfano, kiwanja kilichopo London, Kiwanja Nambari 19 *Denewood Road,* N64AQ kimekaa bila kuendelezwa kwa takriban miaka mine sasa. Kufuatia hali hiyo, Serikali ya Uingereza imeonesha nia ya kukichukua kiwanja hicho kwa kuwa kinahatarisha usalama wa wananchi wa eneo husika kwa jumla. Kutokana na ufinyu wa bajeti ya Fungu 34, Kamati inashauri kuwa kiwanja hicho kiendelezwe kwa nja ya ubia na mifuko ya Jamii ya nchini kwetu; na

(xi) Kwa madhumuni ya kuongeza ufanisi katika utoaji huduma za Kikonseli na utekelezaji wa majukumu mengine, ni vema utaratibu wa matumizi ya *Diplomatic Bag* ukatumika ipasavyo na kuepuka kucheleweshwa mawasiliano kwa utaratibu huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Chuo cha Diplomasia ni Taasisi muhimu kwa taaluma zinazohitajika katika masuala ya msingi kuhusu utekelezaji wa Sera ya Mambo ya Nje. Kamati inashauri kuwa Serikali iandae mpango wa maendeleo ya Chuo hiki sambamba na kukiwezesha kujenga majengo mengine katika eneo jipya.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili malengo ya *APRM* yawe na tija kwa Taifa letu, Sekretarieti ya *APRM* Tanzania

iwezeshwe ipasavyo kukabiliana na changamoto za kiuendeshaji. Aidha, kwa kuwa shughuli za *APRM* Tanzania hazina Fungu *(vote),* Kifungu *(subvote)* wala Kasma *(Item),* Kamati inasisitiza umuhimu wa kuzitengea shughuli hizo Kifungu chake kinachojitegemea kwa ajili ya uendeshaji bora na uwajibikaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa Kituo cha Mikutano cha Kimataifa Arusha, Kamati inashauri kuwa badala ya Kituo hicho kusubiri fedha kutoka Serikalini, utaratibu wa kukopa fedha kutoka Taasisi za Fedha utumike katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Aidha, ili kuepuka changamoto za uvamizi wa maeneo yake ni vema kituo hiki kiwe na utamaduni wa kufanyia kazi changamoto mbalimbali kwa wakati. Kwa mfano, tatizo la uvamizi wa maeneo lililoripotiwa kuwa changamoto halikufanyiwa kazi mapema ilivyopaswa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ushauri wa jumla. Pamoja na maoni na ushauri mahsusi Kamati inashauri kuwa:-

(i) Ili Balozi zetu ziweze kutekeleza majukumu yake ipasavyo, Wizara ihakikishe kuwa Hati za utambulisho na Hati za wito zinazokosekana zinakamilishwa mapema iwezekanavyo.

(ii) Kwa kuwa kuna ufinyu wa bajeti ya maendeleo kwa Balozi zetu na kwa vile Sheria ya Mikopo, Misaada na Dhamana *(The Government Loans, Guaranteees and Grants)* ya mwaka 1974 iliyorekebishwa mwaka 2004 hairuhusu Serikali kutoa udhamini kwa Taasisi za Serikali kuchukua mikopo benki, Kamati inasisitiza umuhimu wa Sheria hiyo kufanyiwa marekebisho. Katika zoezi hilo, ni vema Sheria iruhusu udhamini utakaowezesha Balozi hizo kutumia Mifuko ya Hifadhi ya Jamii na Utaratibu wa *"Mortagage Financing"* katika kutekeleza miradi ya maendeleo.

Licha ya ushauri huu kutolewa Bungeni kwa miaka zaidi ya sita sasa, Wizara haijafanya juhudi ya kutosha kuhakikisha kuwa Sheria ya Mikopo, Misaada na Dhamana

*(The Government Loans, Guaranteees and Grants)* inafanyiwa marekebisho ili kuweza kuwa na majengo ya kutosha kwa ajili ya Balozi zetu. Laiti ushauri huu ungetekelezwa tangu ulipotolewa, kwa sasa Balozi zetu nyingi zingekuwa kwenye majengo ya Serikali na kuipunguzia serikali mzigo wa kulipia pango.

(iii) Ili kuzingatia misingi bora ya uwajibikaji pamoja na kuharakisha upatikanaji wa fedha kwa Balozi zetu, ni vyema Hazina ipeleke fedha moja kwamoja kwenye Balozi hizo kama inavyofanyika kwa Halmashauri nchini bila kupitisha kwa Makatibu Tawala wa Mikoa.

(iv) Katika kutekeleza majukumu yanayohusiana na mambo ya diplomasia, suala la mawasiliano ni jambo muhimu. Kamati inashauri kuwa Wizara iboreshe kasi na namna ya mawasiliano ili kuongeza ufanisi wa majukumu ya kidiplomasia.

(v) Kwa kuwa mikutano ya Mabalozi ni muhimu kwa ajili ya kutathimini na kuboresha utekelezaji wa Sera ya Mambo ya Nje, Wizara hii iwezeshwe zaidi kifedha katika kasma zinazohusika na mikutano hiyo na kuhakikisha kuwa jambo hilo linatekelezwa.

(vi) Pamoja na kuipongeza Serikali kwa kufanikisha ujenzi wa Kituo cha Mikutano ya Kimataifa cha Mwalimu Nyerere, Dar es Salaam, Kamati inashauri kuwa uendeshaji wa kituo hicho uzingatia kupatikana kwa tija.

(vii) Kwa kuwa shughuli za Wizara hii ni suala la Muungano, Kamati inashauri kuwa Wizara izingatie umuhimu wa Watumishi wanaopangiwa kazi za Wizara hii kuwa katika sura ya Muungano. Kwa mfano, Katika Hotuba ya Mheshimiwa Waziri kuhusu bajeti kwa mwaka wa fedha 2012/2013 iliyotolewa tarehe 6 Agosti, 2012 , Tazama Taarifa Rasmi ya Majadiliano ya Bunge *(Hansard)* ya Mkutano wa Nane, Kikao cha Arobaini na Moja, Tarehe 6 Agosti, 2013, alisema:-

*Mheshimiwa Spika, Wizara yangu imeweka mkakati wa kuongeza idadi ya Watumishi kutoka Zanzibar katika kada ya Maafisa Mambo ya Nje kwa kuwapatia fursa wanafunzi 18 kutoka Tanzania Visiwani kuingia kwenye chuo chetu cha Diplomasia...* Mwisho wa Kunukuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, licha ya ahadi iliyotolewa na Mheshimiwa Waziri kuhusu watumishi hao, taarifa zilizopatikana kwenye Kamati zinaonyesha kuwa ahadi hiyo haikutekelezwa.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, natumaini mnafuatilia, usomaji wa Mheshimiwa Nkamia unanikumbusha usomaji wa taarifa ya habari enzi za Redio Tanzania Dar es Salaam, wale Watangazaji wa siku hizi wasikilize vizuri, Mheshimiwa Nkamia endelea. *(Makofi/ Kicheko)*

**MHE. JUMA S. NKAMIA (K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA):** Kamati ina maoni kuwa kuna umuhimu mkubwa kwa Serikali kukamilisha ahadi zinazotolewa Bungeni.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuhitimisha, nachukua fursa hii kumpongeza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dokta Jakaya Mrisho Kikwete kwa kazi nzuri ya kuendeleza heshima ya Tanzania katika diplomasia na mahusiano na nchi nyingine. Kamati inashauri kuwa viongozi na Watendaji wengine wa Serikali wafuate kikamilifu juhudi za Mheshimiwa Rais.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru wewe binafsi kunipatia fursa hii adhimu ili niwasilishe taarifa pamoja na maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hii. Ni mara ya kwanza kwa Kamati hii kutoa Taarifa Bungeni tangu ulipoteua upya Wajumbe wa Kamati za Bunge katika Mfumo huu mpya. Namshukuru pia Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa, Mheshimiwa Bernard K. Membe, kwa ushirikiano alioutoa wakati Kamati ilipokuwa

ikitekeleza kazi zake.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, namshukuru Naibu Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa, Mheshimiwa Mahadhi O. Juma na Katibu Mkuu wa Wizara hii Ndugu John M. Haule, kwa kutoa ufafanuzi uliotakiwa na Kamati wakati wa vikao.

Mheshimiwa Naibu Spika, kipekee kabisa, nawashukuru wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa, chini ya Mwenyekiti wake, Mheshimiwa Edward Lowassa, kwa Ushirikiano wao wakati wa kupitia, kujadili na kuchambua makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara hii. Kwa kuthamini michango yao, naomba kuwatambua kwa majina kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Edward N. Lowassa, Mwenyekiti, Mheshimiwa Mussa A. Zungu, Makamu Mwenyekiti, Mheshimiwa Selemani Saidi Jafo, Mheshimiwa Khalifa Suleiman Khalifa, Mheshimiwa Susan Anselm Jerome Lyimo, Mheshimiwa Betty Eliezer Machangu, Mheshimiwa Eng. Yussuf Hamad Masauni, Mheshimiwa Faith Mohamed Mitambo, Mheshimiwa Thuwayba Idrisa Muhamed, Mheshimiwa Juma Selemani Nkamia, Mheshimiwa Leticia Mageni Nyerere, Mheshimiwa Muhammad Ibrahim Sanya, Mheshimiwa John Magale Shibuda na Mheshimiwa Anastazia James Wambura.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, lakini si kwa umuhimu nawashukuru Ndugu Athuman Hussein, Ramadhani Issa na Nesta Kawamala, Makatibu wa Kamati hii kwa kuratibu vema shughuli za Kamati na kufanikisha taarifa hii kwa wakati. Nawashukuru watumishi wote wa Ofisi ya Bunge chini ya uongozi wa Dokta Thomas D. Kashililah, Katibu wa Bunge kwa kuisaidia Kamati kutekeleza majukumu yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, sasa naliomba Bunge lako Tukufu liipokee Taarifa hii na kuijadili pamoja na kuyakubali Makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara hii, Fungu 34, kama yalivyowasilishwa na Mtoa

Hoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Juma Nkamia, nakushukuru sana kwa usomaji mahiri wa hotuba iliyo mbele yetu.

Sasa naomba kumwita Msemaji wa Kambi ya Upinzani kuhusu Wizara hii ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa, anakuja Mheshimiwa Ezekia Wenje. *(Makofi)*

**MHE. EZEKIA D. WENJE – MSEMAJI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI WIZARA YA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA:** Mheshimiwa Naibu Spika, katika hotuba ya Msemaji Mkuu wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni katika bajeti ya Wizara hii mwaka 2012/2013, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inayoongozwa na CHADEMA ilibaini mapungufu mengi ya kiutendaji na kiuwajibikaji katika wizara hii, na hivyo kuitaka Serikali kufanya mambo yafuatayo ili kuboresha utendaji na ufanisi:-

(1) Kuziwezesha Balozi zetu nje kwa kuzitengea fedha za kutosha ili ziweze kufanya kazi kwa ufanisi.

(2) Kutoa idadi ya majengo ya Balozi zetu nje (nyumba za mabalozi, nyumba za Maafisa wa Balozi na Ofisi za Balozi) kwa mchanganuo wa idadi ya nyumba katika nchi na kama nyumba hizo zina hati miliki au la.

(3) Kutoa taarifa ya namna kila Ubalozi ulivyotekeleza Sera ya Diplomasia ya Uchumi kwa kuzingatia kwamba Balozi nyingi ziko hoi kifedha kiasi cha kwamba Waambata wa Kiuchumi wanakosa fedha za kusafiri kutoka sehemu moja hadi nyingine kwa ajili ya upelelezi wa masuala ya kiuchumi.

(4) Kulikarabati jengo la Ubalozi wa Tanzania huko Msumbiji lililokuwa limechakaa kwa kutofanyiwa ukarabati tangu 1975 ingawa jengo hilo tulipewa bure na

Serikali ya Msumbiji chini ya *FRELIMO*.

(5) Kujenga kitega uchumi katika kiwanja cha Tanzania kilichopo Dubai na kukiendeleza kiwanja namba 19 tulichopewa bure na Serikali ya Uingereza kilichopo Uingereza *(Central London)* ambavyo vimekuwa maficho ya wezi kwa kutoendelezwa kwa muda mrefu na kusababisha Serikali za nchi hizo kutaka kutaifisha viwanja hivyo.

(6) Kufanya uchunguzi kuhusu tuhuma za Balozi zetu nchini China...

## MWONGOZO WA SPIKA

**MHE. MASOUD ABDALLA SALIM:** Mwongozo wa Spika.

**NAIBU SPIKA:** Mwongozo kuhusu suala gani? Mheshimiwa Wenje, nakuomba kidogo samahani, namwona Mheshimiwa Masoud amesimama.

**MHE. MASOUD ABDALLA SALIM:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kutumia Kanuni ya 68 (1) inayoenda sambamba na Kanuni ya 64(1) (a), (f) na (g) naomba kunukuu:-

*"Bila kuathiri masharti ya Ibara ya 100 ya Katiba inayolinda na kuhifadhi uhuru wa mawazo na majadiliano katika Bunge, Mbunge:-*

*(a) hatatoa ndani ya Bunge taarifa ambazo hazina ukweli.*

*(f) hatamsema vibaya au kutoa lugha ya matusi kwa Mbunge au mtu mwingine yeyote. (Makofi)*

*(g) hatatumia lugha ya kuudhi inayodhalilisha watu wengine". (Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika hotuba iliyowasilishwa na inayoendelea kuwasilishwa, ukurasa wa nane, *paragraph* ya tatu ya Kambi ya CHADEMA... *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ina maelezo yafuatayo:-

*“Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa Chama cha CUF kutokana na itikadi zake za mrengo wa Kiliberali ambazo miongoni mwa misingi yake mikuu ni pamoja na kupigania haki za ndoa za jinsia moja, usagaji na ushoga”*

**WABUNGE FULANI:** Aaaaaaaah!

**WABUNGE FULANI:** *Shame, Shame, Shame*!

**MHE. MASOUD ABDALLA SALIM:** Mheshimiwa Naibu Spika, maneno haya hayakubaliki kutolewa ndani ya Bunge hili, maneno haya hayana ukweli, huu ni uzushi, huu ni uongo, huu ni uhuni, huu ni uzandiki …

**MBUNGE FULANI:** Ushenzi.

**MHE. MASOUD ABDALLA SALIM:** Na huu ni ushenzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, imekuwa ni tabia mbaya kama hii, Watanzania ambao wametupa ridhaa ya muda mrefu kuja humu ndani kusikiliza nini ambacho kinatakiwa katika hotuba kama hizi, lakini kwa bahati mbaya sana, leo hii kunatolewa lugha kama hizi ndani ya vitabu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nadhani hotuba hii kwa mtindo huu, kwanza waombe radhi, la pili wafute, la tatu naiomba Kamati ya Maadili ya Bunge ichukue nafasi yake na kama Kamati ya Maadili imeona jambo hili ni dogodogo… *(Makofi)*

**MHE. ALLY K. MOHAMED:** Hana nidhamu kabisa huyo.

**MHE. MASOUD ABDALLA SALIM:** Mheshimiwa Naibu Spika, sisi kama Chama cha Wananchi CUF, tutachukua hatua inayostahili dhidi ya Bunge na dhidi ya CHADEMA. *(Makofi)*

**MHE. ALLY K. MOHAMED:** Kabisa, kabisa jambazi huyo, labda yeye ndiye msagaji huyo.

**MHE. MASOUD ABDALLA SALIM:** Mheshimiwa Naibu Spika, niwaambie waziwazi kwamba hatukubali taarifa hii, uhuni huu, uchafu huu na matusi haya. Huu ni udhalilishaji mkubwa kupita kiasi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nikumbushe tu wale wenzetu wa Serikali ya *Conservative* ya Uingereza ambayo ilikubali na ilikuwa inapigania ndoa ya jinsia moja na pia ilikuwa kishawishi au ikitoa taarifa kwa baadhi kwamba ikiwa hamtaunga mkono jambo hili mnaweza mkanyimwa misaada lakini bado Tanzania ilikuwa na msimamo wake

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Waziri hapa alisema ...

**MHE. MASOUD ABDALLA SALIM:** Na Mheshimiwa Waziri alisema hapa waziwazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nakuomba sana...

**MBUNGE FULANI:** Wachukuliwe hatua.

**MHE. MASOUD ABDALLA SALIM:** Wachukuliwe hatua za kinidhamu, kwanza wakome, wakome mara mia moja... *(Makofi)*

**MHE. ALLY K. MOHAMED:** Wakome kabisa.

**MHE. MASOUD ABDALLA SALIM:** Mheshimiwa Naibu Spika, kama Bunge halikuchukua hatua zinazotakiwa, nasema tena...

**MBUNGE FULANI:** *CUF*.

**MHE. MASOUD ABDALLA SALIM:** *CUF* itachukua hatua kwa Bunge na CHADEMA, sisi tuko tayari kwa mapambano

wakati wowote, nashukuru sana, shenzi! *(Makofi)*

**WABUNGE FULANI:** Toa hoja, toa hoja.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Wenje, una maelezo yoyote kuhusu jambo hilo.

**MHE. EZEKIA D. WENJE:** Mheshimiwa Naibu Spika, *with due respect,* naomba Wabunge wenzangu wanisikilize.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunachozungumzia, tunazungumzia mahusiano ya vyama vilivyoko Tanzania na Vyama vingine vilivyo nje.

**MBUNGE FULANI:** Hayahusu, hayahusu!

**NAIBU SPIKA:** *Order, order!*

**MHE. EZEKIA D. WENJE – MSEMAJI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI WIZARA YA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA:** Tumeeleza Chama cha Mapinduzi kina mahusiano na vyama gani, tumeeleza CHADEMA ina mahusiano na vyama gani na misingi ya mahusiano ya vyama vilivyopo Tanzania na vyama vya nje iko *based* kwenye *ideology.* CCM wako *left,* CHADEMA tuko *centre, CUF* ni *Liberals* na misingi ya *Liberals*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunachozungumza hapa ni *ideology, the ideology which is cherished by Liberals* na *Liberals...*

**WABUNGE FULANI:** Aaaaah!

**MHE. EZEKIA D. WENJE – MSEMAJI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI WIZARA YA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA:** Unaweza ukakataa kunielewa kwa sababu hautaki kunielewa.

**MHE. MASOUD ABDALLA SALIM:** Mheshimiwa Naibu Spika, aondoe.

**MHE. EZEKIA D. WENJE – MSEMAJI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI WIZARA YA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA:** Mheshimiwa Naibu Spika, mimi ndiyo umenipa nafasi, misingi ya *Ideology...*

**MHE. MASOUD ABDALLA SALIM:** Wewe ondoa uchafu wako huu, ondoa uchafu wako huu, wewe!

*(Hapa Mheshimiwa Masoud Abdalla Salim Alichana hotuba ya Upinzani)*

**NAIBU SPIKA:** Nimempa nafasi Mheshimiwa Wenje.

*(Hapa Wabunge wa CUF walikuwa wakiongea kwa sauti za juu wakisisitiza Mheshimiwa Ezekia Wenje kuondoa maneno hayo kwenye hotuba yake)*

**NAIBU SPIKA:** Naomba tuwe na uvumilivu wa kumsikiliza Mheshimiwa.

**MHE. MASOUD ABDALLA SALIM:** Haiwezekani ataondoa, wewe mshenzi ondoa, wewe utaondoa uchafu wako, haiwezekani kabisa, wewe toka.

**MHE. EZEKIA D. WENJE:** Mheshimiwa Naibu Spika...

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Wenje kaa kwanza kidogo.

**MHE. MASOUD ABDALLA SALIM:** Wewe toka.

**MBUNGE FULANI:** Msikubali, leo wako wachache mdundeni Wenje.

**MHE. MASOUD ABDALLA SALIM:** Ukome na mama yako, shenzi.

**MBUNGE FULANI:** Haisomwi!

**MHE. MASOUD ABDALLA SALIM:** Haisomwi hii, hapa

husomi, hata siku moja, husomi taarifa hii.

**MBUNGE FULANI:** Mpigeni Wenje.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, naomba kusitisha shughuli za Bunge hadi saa 11.00 leo jioni. *(Makofi)*

**WABUNGE FULANI:** Shenzi, unatufanya sisi wapumbavu.

**NAIBU SPIKA:** Wakati huohuo, naomba Kamati ya Maadili ikutane mara moja.

**MHE. ALLY K. MOHAMED:** Apigwe!

**WABUNGE FULANI:** Washtakiwe, wewe ukome, iwe mwisho leo, huwezi kututukana namna hii, mwache akasome na jamaa zake, kama hamna nidhamu ni nyie sie tuna nidhamu, kasome huko *shenzi type*, hamna adabu kumbe. Kama ushenzi ni wa Kichadema ni wa Kichadema sio wa kutufanyia sisi.

*(Hapa Wabunge wa CUF waliendelea kuongea kwa maneno ya juu huku wakimsonga Mheshimiwa Ezekia Wenje na wengine wakisisitiza apigwe wakati Naibu Spika akitoka nje ya ukumbi wa Bunge mara baada ya kusitisha Bunge kutokana na fujo zilizotokea)*

*(Saa 6.00 mchana Bunge lilisitishwa hadi Saa 11.00 jioni)*

*(Saa11.00 jioni Bunge lilirudia)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, wakati nimesitisha Bunge kipindi cha asubuhi, tulikuwa tumefika mahali pa sintofahamu kuhusu mambo yaliyotokea humu ndani, nyote mlikuwepo. Nikawa kwa niaba yenu nimeiomba Kamati ya Maadili ikutane na kuiangalia hali hiyo. Sasa naomba kwa niaba yenu nimwombe Mheshimiwa Makamu Mwenyekiti, Mheshimiwa Capt. John Z. Chiligati, ambaye ndiye alikuwa Mwenyekiti wa kikao hicho, kwa dakika chache atupatie picha ya nini kimejiri na nini ushauri wao.

Mheshimiwa Chiligati, tafadhali dakika tano. *(Makofi)*

**MHE. CAPT. JOHN Z. CHILIGATI - MAKAMU MWENYEKITI KAMATI YA HAKI, MAADILI NA MADARAKA YA BUNGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Kamati ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge, nitoe taarifa fupi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kutoa agizo lako, Kamati tumekaa kutazama hali iliyojiri hapa. Tukawaita Mheshimiwa Masoud Abdalla Salim ambaye alikuwa ndiye mlalamikaji na Mheshimiwa Ezekia D. Wenje akiwa ndiye mlalamikiwa. Mheshimiwa Masoud Abdalla Salim aliiambia Kamati kwamba, anacholalamika ni kwamba, ile hotuba ya Kambi ya Upinzani, ukurasa wa nane, ina maneno ya kuudhi, maneno ya kudhalilisha chama cha *CUF* na maneno ambayo hayafai hata kuyaandika kwamba kuna baadhi ya vyama vinafuata sera za ushoga na usagaji na kadhalika. Kwa hiyo, alichoomba Mheshimiwa Masoud Abdalla Salim, ni kwamba, hayo maneno moja yafutwe, halafu aombe radhi na kwamba Kamati itafute adhabu ili vitendo kama hivi visirudiwe na watu wengine. Ni mambo matatu ambayo mheshimiwa Masoud Abdalla Salim, aliwasilisha kwenye Kamati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Ezekia D. Wenje naye alipewa nafasi ya kujieleza na yeye alijieleza kwamba yale maneno yeye hakulenga *CUF*, bali yeye alikuwa anaeleza tu itikadi na misimamo ya vyama vya Uleberali Duniani kwamba, vyama hivyo, sera yao kuu ni uhuru wa mtu mmoja mmoja unalidwa, kwa hiyo, mtu huyo akiwa ni msagaji, ndoa ya watu wenye jinsia moja ni sawa. Hivyo, Mheshimiwa Ezekia D. Wenje anasema, yeye alikuwa anaeleza itikadi ya vyama vya Uliberali wala hakuwa analenga chama fulani. Kwa hiyo, yeye akasema haoni kama kuna kosa lolote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, basi katika mahojiano marefu, ilichukua karibu saa moja na nusu tunahojiana nao, hatimaye Kamati ikashauri na tunalishauri Bunge kupitia kwako. Kwanza, tulishauri yale maneno yafutwe au yaondolewe pamoja na kwamba yeye anasema aliyaweka

kwa nia njema, lakini hiyo nia njema imeleta kichefu kichefu, hivyo ameleta *menu* kwa walaji ambayo imeleta shida, hivyo ayafute. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, tukasema kwa sababu katika kusema maneno yale, ameumiza watu wengine na sisi hapa tunakaa kama familia na kama Watanzania. Hata kama aliyasema kwa nia njema lakini yakawa yameumiza, kuna watu wamepata maumivu, basi tukasema kwamba, pamoja na nia yake njema, lakini maadam yale maneno yameleta maumivu kwa wengine; basi wale ambao maneno yale yamewaumiza kwa namna moja au nyingine, aombe radhi kwamba kama maneno yale baadhi ya watu yamewaumiza sikuwa na nia mbaya basi tusameheane, tusonge mbele, kwa hiyo, tukashauri hayo mambo mawili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, bahati nzuri Mheshimiwa Masoud Abdalla Salim lile la kwamba Kamati iimpe adhabu Ezekia D. Wenje, Mheshimiwa Masoud Abdalla Salim yeye alisema analiondoa. Kwa hiyo, tukabaki na kuondoa yale maneno na kuomba radhi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Ezekia D. Wenje pale alituambia kwamba, anakubali na anakwenda kuondoa maneno yale na hiyo sasa *version* mpya ataileta kwenye Kamati tuitazame. Aidha, alisema lile la kuomba radhi hawezi kuwaomba radhi kwa sababu hakuwa na nia mbaya, wala haoni kama amefanya kosa. Basi tukamwambia hilo alilokubali, aende akalifanye.

**WABUNGE FULANI:** Husomi hapa.

**MHE. CAPT. JOHN Z. CHILIGATI - MAKAMU MWENYEKITI KAMATI YA HAKI, MAADILI NA MADARAKA YA BUNGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa amekwenda ameleta sasa hayo mabadiliko. Hayo mabadiliko aliyoyaleta hayana tofauti na ile *version* ya kwanza…

**WABUNGE FULANI:** Aaah!

**MHE. CAPT. JOHN Z. CHILIGATI - MAKAMU MWENYEKITI KAMATI YA HAKI, MAADILI NA MADARAKA YA BUNGE:** Kabadilisha maneno mengine kaandika kwa Kiingereza lakini mambo ya *homesexuality* bado yamo, *lesbian* bado yamo ambayo ndiyo usagaji. Kwa hiyo, yale yote ambayo tulikuwa tumemwambia hakuyafanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, tukakushauri kwamba moja, sasa Kiti chako kimwamuru Mheshimiwa Ezekia Wenje aondoe yale maneno ili kuleta mshikamano na umoja katika Bunge letu kwa sababu yameudhi chama cha pili. Vilevile, awe tu muungwana aombe radhi, hili jambo litakuwa limekwisha, tunasonga mbele. Kwa hiyo, ndiyo ushauri ambao tunautoa kwako, utoe hiyo *ruling*. Mambo mawili, yale maneno asiyasome, halafu pili aombe radhi, hapo tutapata muafaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. *(Makofi)*

**MWONGOZO WA SPIKA**

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mwongozo wa Spika.

**WABUNGE FULANI:** Kaa chini.

**NAIBU SPIKA:** Naomba ukae, Mheshimiwa Mnyika nakuomba sana ukae, jambo hili ni kubwa.

Mheshimiwa Ezekia Wenje, ulisikia maneno ya asubuhi, ulisikia maneno ya Kamati ya Maadili na Bunge zima limesikia kama nilivyompa Mwenyekiti dakika tano, nakupa na wewe dakika tano ili unisaidie mimi Kiti katika kuona tunaendeleaje. Mheshimiwa Ezekia Wenje, dakika tano!

**MHE. EZEKIA D. WENJE – MSEMAJI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI WIZARA YA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana. Naomba niseme maneno yafuatayo ya utangulizi kwa sababu umenipa dakika tano...

**NAIBU SPIKA:** Husikiki kabisa labda sijui utumie *microphone* nyingine!

**MHE. EZEKIA D. WENJE – MSEMAJI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI WIZARA YA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitoe maneno ya utangulizi yafuatayo kabla sijafikia mwisho kwa sababu umenipa dakika tano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hotuba yangu ukurasa wa nane, ulioleta shida kidogo, ni kweli Chama cha Wananchi *CUF* kilijiunga na *Oxford Congress ya Liberal International* mwaka 1997.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia, ni kweli kwamba, mwaka huo huo terehe 27-30 Novemba, 1997, kuna Mkutano Mkuu, ulifanyika *Oxford* Nchini Uingereza, uliokuwa na kitu kinaitwa *Liberal Manifesto*. Katika Mkutano huo, umoja wa vyama hivyo ulikubaliana msimamo wa pamoja na nanukuu.

*"The extension of rules of equality to sexual minorities and the recognition that homosexuality and lesbianism are legitimate expressions of personal proclivities".*

Kwa tafsiri rahisi, Waliberali hao walipitisha ajenda ya Waliberali katika karne ya 21, *the Liberal Agenda in the 21 century* ya kuutambua ushoga na usagaji kama matendo halali.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema haya, *with due respect* na hili Bunge limebeba Wasomi na Wanasheria, *quotation* niliyofanya, ni kweli kwamba *CUF* ni wanachama wa *Liberals* na nilichosema ni *family values* za *liberals*, *what they believe,* ndicho nilichosema. *(Makofi)*

*(Hapa baadhi ya Waheshimiwa Wabunge wa CUF walikuwa wamesimama wakitaka kupewa nafasi ya kuongea)*

**NAIBU SPIKA:** Nawaombeni sana muwe wavumilivu, nitawapa nafasi ya kuchangia, sasa hivi nimempa nafasi Mheshimiwa Ezekia Wenje, naomba utulivu.

**MHE. EZEKIA D. WENJE – MSEMAJI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI WIZARA YA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA:** Mheshimiwa Naibu Spika, umenipa dakika tano.

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla sijafika mwisho, pia naomba, nimedhalilishwa sana kwenye hili Bunge leo...

**WABUNGE FULANI:** Bado hujadhalilishwa!

**MHE. EZEKIA D. WENJE – MSEMAJI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI WIZARA YA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA:** Nimetukwanwa kwenye hili Bunge, wakafanya na fujo ndani ya hili Bunge, mpaka nikakatisha hotuba yangu lakini hayo nayakubali.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa unahitaji nifute kauli yangu, au nitoe yale maneno...

**NAIBU SPIKA:** Siyo mimi, mimi bado sijasema chochote, nimekuambia ujibu yale ya Kamati ya Maadili kwa sababu ulikuwepo na unajua kila kilichotokea, wamekuomba mambo mawili. Moja, ufute kabisa kauli zote zile ukurasa wa 7, 8 na 9 halafu pili, uombe radhi. Ndicho walichotaka, sasa wewe unasemaje katika haya.

**MHE. EZEKIA D. WENJE – MSEMAJI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI WIZARA YA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA:** Sawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu ushauri wa Kamati, ndiyo maana tulishindwana kwenye Kamati niliwauliza, wanahitaji nifute maneno ambayo ni ya ukweli? Kwa sababu ndiyo ukweli na *Oxford Manifesto* ya 1997 ni hii hapa.

*(Hapa Mheshimiwa Ezekia Wenje alikuwa akionyesha*

*Nyaraka aliyokuwa anaizungumzia)*

**MHE. EZEKIA D. WENJE – MSEMAJI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI WIZARA YA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA:** *What is wrong?* Tatizo liko wapi? Nimefanya kosa gani? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, leo kaambiwa naambiwa niombe msamaha kwa kosa lipi? Kuniambia niombe msamaha ni kama vile mnataka ku-sq*ueeze water out of a stone, something that you will never get!* Siwezi kuomba msamaha kwa sababu sijafanya kosa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana. *(Makofi)*

## MWONGOZO WA SPIKA

**MHE. MASOUD ABDALLA SALIM:** Mwongozo wa Spika.

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mwongozo wa Spika.

**NAIBU SPIKA:** Nimekuona Mheshimiwa Masoud.

**MHE. MASOUD ABDALLA SALIM:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru…

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mwongozo wa Spika.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mnyika nilishasema tangu mapema, mtu yeyote anayewasha *microphone* na kuanza kunihutubia badala ya kusimama mahali pake, simpi nafasi. Mwenzako amesimama mahali peke bila kuwasha *microphone*, Mheshimiwa Masoud!

**MHE. MASOUD ABDALLA SALIM:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru.

Mheshimiwa Naibu Spika, nasimama hapa kwa mwendelezo tu wa yaliyotokea asubuhi, kwa Kanuni ya 68(1),

lengo langu ni 64(1) (a), (f) na (g). kama ilivyo kawaida.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kueleza niliyoeleza kwenye hotuba ya Kambi ya CHADEMA, niliyoyataka kwamba ni busara, kwanza aombe radhi Chama cha Wananchi CUF na pili aondoe maneno haya kama alivyoandika kwa maandishi na la tatu nikasema pia vilevile Kamati ya Maadili ichukue nafasi yake kuweka taratibu ya hukumu gani itaweza kutolewa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya majadiliano na kwa kuwa Kamati ya Maadili imependekeza, mimi bado naweka msimamo wangu palepale kwamba kwanza, Mheshimiwa Wenje, Msemaji wa CHADEMA, aombe radhi Chama cha Wanachi CUF. Pili, Mheshimiwa Wenje Msemaji wa CHADEMA, ni vyema maneno haya ayaondoe kwa maandishi. Bila hivyo, mimi nasema msimamo wangu binafsi kama mtoa hoja, bado uko palepale na nina imani Wabunge wa CUF wataniunga mkono, hotuba hii hapa leo haisomwi. (*Makofi*)

**MBUNGE FULANI:** Kabisa!

**MHE. MASOUD ABDALLA SALIM:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana, tujadili ya Waziri na Kamati.

**MBUNGE FULANI:** Basi!

## MWONGOZO WA SPIKA

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mwongozo wa Spika.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mnyika sasa nimekuona, kwa dakika mbili tu au tatu. Mheshimiwa Lusinde ulisimama au ulikuwa unakaa tu!

**MHE. LIVINGSTONE J. LUSINDE:** Nilisimama.

**NAIBU SPIKA:** Sawa.

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Mwongozo wako kwa mujibu wa Kanuni ya 5 na kwa mujibu wa Nyongeza ya Kanuni ya 118, inayohusu majukumu na kazi za Kamati ya Kinga, Haki na Madaraka ya Bunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, majukumu ya Kamati ya Kinga, Haki na Madaraka ya Bunge ni kuchunguza pale ambapo inapelekewa masuala yanayohusu ukiukwaji wa maadili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tarehe 4, Februari, 2013 katika Bunge hilihili, kulitokea vurugu. Kamati ile ilipewa kazi ya kwenda kutazama mikanda ile ya vurugu zilizotuhumiwa kupitia kumbukumbu kwa maana ya *Hansard* na kutoa taarifa kamili Bungeni na hatua za kuchukuliwa. Tofauti na Kanuni hiyo na utaratibu huo, Kamati ya hii ya jambo hili, ilipokwenda kushughulikia vurugu ama jambo lilojitokeza, ilikwenda kufanya ubaguzi wa kushughuliklia eneo moja, mengine hayajashughulikiwa kabisa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ningeomba Mwongozo wako...

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mnyika, naomba ukae na nitoe Mwongozo wangu moja kwa moja kwa sababu nimeelewa unachoonglea ni nini? Kamati ya Maadili ina namna mbili za kushughulikia mambo. Namna moja ni ya kushughulikia jambo kama kesi na namna ya pili ni ya kushughulikia jambo kwa maana ya *mediation*. Kamati leo ilikaa na kushughulikia jambo hili kwa maana ya *mediation* na ndiyo maana wajumbe wote ambao walienda huko, akina Wenje na wengine hakuna aliyeapishwa. Utaratibu wa Kamati ile kila anayeingia anaapishwa kwanza lakini leo walifanya kazi ya usuluhishi kwa ajili ya kulifanya Bunge liweze kwenda pamoja ili shughuli zetu ziweze kwenda. Tukumbuke

mfano leo ni Wizara ya siku moja, tayari tunatumia muda ambao kwa kweli siyo wa upande wetu. Kwa hiyo, kuna tofauti kubwa sana kati kesi unayoi-*refer* na hili jambo la leo, ni tofauti kubwa kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Lusinde nilikuona!

**MHE. LIVINGSTONE J. LUSINDE:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa ajili ya kuokoa muda wa Bunge hili na kwa ajili ya kuokoa pesa za Watanzania ambazo tunazitumia tunapokuwa hapa, ningeomba Meza yako niishauri jambo moja tu kwamba, hotuba iliyosomwa ya Upinzani inatosha, tuendelee na mjadala wa Wizara hii, badala ya kurudi nyuma kuendelea na hoja zingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuishauri Meza hivyo na naomba kutoa hoja.

**MHE. MASOUD ABDALLA SALIM:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki!

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Kwa Kanuni ipi?

**WABUNGE FULANI:** Hiyo hiyo!

**MHE. MURTAZA A. MANGUNGU:** Wewe unayeuliza Kanuni wewe ni nani?

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusikiliza ushauri wa Kamati ya Maadili na kuwapa nafasi wadau wakuu na baadhi ya wachangiaji wachache, sasa mimi kwa Kiti hiki mlichonipa Waheshimiwa Wabunge, ninamtaka sasa Mheshimiwa Wenje afanye mambo mawili. Kwanza, aombe radhi na pili akubali kuondoa maneno yote

ya fungu la tatu. Kwa hiyo, asome fungu la kwanza, la pili, aliruke la tatu, asome la nne na mengine yote yanayoendelea, kama ushauri wa Kamati ulivyotolewa. Namtaka tu mbele ya Bunge sasa akubaliane na ushauri wa Kamati, aanze na la kwanza la kuomba radhi, kabla ya lingine. Mheshimiwa Wenje, kazi kwako.

**MHE. EZEKIA D. WENJE – MSEMAJI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI WIZARA YA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA:** Mheshimiwa Naibu Spika, unaweza ukarudia unahitaji nifanye nini? Samahani sikukupata vizuri, naomba unipe maelekezo mapya, samahani sikukupata vizuri.

**NAIBU SPIKA:** Maelekezo ninayokupa kama Kiti, ni yaleyale yalitolewa na Kamati, nimekubaliana na Kamati kwa ushauri wao waliotoa. Sasa siyo Kamati iliyokushauri ukakataa, Kamati imekushauri ukakataa, sasa mimi nakutaka uyafanye yale mawili, ili tuweze kuendelea au vinginevyo, yale ambayo mwanzoni uliyakataa yote mawili, kwanza, la kuomba radhi, pili kufuta maneno yote haya ili tuweze kuendelea au vinginevyo. *(Makofi)*

**MHE. EZEKIA D. WENJE – MSEMAJI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI WIZARA YA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza napenda niseme kwamba nimekubali kuruka hayo maeneo uliyosema.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilifikia ukurasa wa tatu...

**WABUNGE FULANI:** Omba radhi kwanza!

**MHE. EZEKIA D. WENJE – MSEMAJI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI WIZARA YA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA:** Mheshimiwa Naibu Spika, suala la kumi...

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Wenje nakushukuru sana,

unaweza ukarudi kwenye Kiti chako, kwa ushirikiano ulionipa.

Waheshimiwa Wabunge, suala hili nalilirudisha tena kwenye Kamati ya Maadili, itatushauri namna ya kuenenda nalo kwa wakati ujao. Kwa maana hiyo ni vigumu sana kwangu kuendelea kuliendesha Bunge hili katika mazingira haya. Kwa jinsi hiyo, nasitisha shughuli za Bunge hadi kesho saa 3.00 asubuhi…

**WABUNGE FULANI:** Aaah!

**NAIBU SPIKA:** Kesho tutaendelea na Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi. *(Makofi)*

**MBUNGE FULANI:** Kila siku wao ndiyo wa kutufanyia hivi!

*(Saa 11.21 jioni Bunge liliahirishwa hadi siku ya Ijumaa,*
*Tarehe 31 Mei, 2013, Saa Tatu Asubuhi)*